SEVENTH-DAY ADVENTISTS CHURCH
SOUTH NYANZA CONFERENCE

# SNC 2022
## MKUTANO MKUU WA NANE



## YESU ANAKUJA UPESI, JIHUSISHE!

@SOUTH NYANZA CONFERENCE, 2022.

# YALIYOMO


MWENYEKITI ........................................ 1
KATIBU ........................................ 32
MHAZINI ........................................ 61
HUDUMA ZA KICHUNGAJI NA FAMILIA ........................................ 84
UWAKILI, MAJENGO, AMANA & ATAPE ........................................ 95
HUDUMA BINAFSI, SHULE YA SABATO NA UCHAPISHAJI.

- HUDUMA BINAFSI ........................................ 114
- SHULE SABATO ........................................ 122
- UCHAPISHAJI ........................................ 125

AFYA NA KIASI ........................................ 133
VIJANA, CHAPLENSIA NA MUZIKI.

- VIJANA ........................................ 143
- CHAPLENSIA ........................................ 151
- MUZIKI ........................................ 155

MAWASILIANO ........................................ 157
WANAWAKE NA WATOTO.

- WANAWAKE ........................................ 167
- WATOTO ........................................ 183

ELIMU, UHURU WA DINI NA MAMBO YA KIJAMII.

- ELIMU ........................................ 188
- UHURU WA DINI NA MAMBO YA KIJAMII........................ 194

TAARIFA ZA TAASISI

- BUPANDAGILA SECONDARY........................................ 199
- NYANZA ADVENTIST SECONDARY........................................ 211
- NGULYATI SECONDARY........................................ 215
- BUPANDAGILA ADVENTIST PRIMARY........................................ 215
- AWM VTC........................................ 222

WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA SNC. ........................................ 234
WACHUNGAJI NA WATUMISHI WA SNC........................................ 241
PICHA MBALIMBALI SNC ........................................ 249

# TAARIFA YA OFISI YA MWENYEKITI



**PR. BEATUS MLOZI**
**MWENYEKITI**
SNC

## UTANGULIZI.

Ndugu Viongozi kutoka Northern Tanzania Union Conference (NTUC), Wajumbe wote wa Session, watumishi wote SNC; nawasalimu katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo.

Nitumie nafasi hii kwa namna ya pekee kuwakaribisha wajumbe wote toka Makanisa yote na Taasisi zote za Conference hii katika Mkutano Mkuu wa Nane (Session). Karibuni sana.

Kwa niaba ya timu yote ya South Nyanza Conference napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uongozi na ulinzi wake kutuwezesha kuifanya kazi ya utume tangu tulipopokea kijiti cha uongozi Juni 2021 hadi hapo tulipofikia. Niwashukuru viongozi waliotutangulia kwa kazi kubwa waliyoifanya, Bwana awabariki. Pamoja na changamoto ya janga la Covid-19 Bwana amekuwa pamoja nasi ni jambo la kumshukuru Mungu.

Napenda kushukuru Uongozi wa Northern Tanzania Union Conference (NTUC) kwa ushauri wao wa busara na kushiriki kufanya kazi pamoja nasi ili kufanikisha utume wa Kanisa na shughuli zote za Conference.

Shukrani za dhati kwa maofisa wenzangu, Katibu wa Conference na Mhazini kwa ushirikiano wao katika kufanikisha mipango ya utume. Niwashukuru wakurugenzi wote wa Idara kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutekeleza majukumu yote muhimu ni pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Conference kuwa tayari kutumia muda wao katika vikao mbalimbali na mashauri juu ya utendaji kazi.

Niwashukuru Wakuu wa Taasisi zote, Wachungaji wote, wafanyakazi wa Conference Watumishi wa Taasisi zote, Wainjilisti, Wazee wa Kanisa na Washiriki wote wa Kanisa kwa mshikamano wenu na maombi yenu katika kutekeleza majukumu yote muhimu ya Kanisa na kaulimbiu isemayo “Nitakwenda (I Will Go)”. Ni matarajio yetu kuwa umoja na mshikamano huu utaendelea kuhakikisha kuwa Conference hii inashiriki kikamilifu katika utume wake.

**Bwana awabariki.**

## KAULIMBIU

**Utume Kwanza (Mission Priority):**

Katika miaka mitano ya awali, tumetembea na kaulimbiu ya Utume kwanza ni Wakati wa Mavuno na kushirikisha kila mshiriki kuwa mwaminifu kwa njozi katika kujitoa kikamilifu kwa utume na kumfanya Mungu kuwa wa kwanza na mengine baadaye.

**Nitakwenda (I Will Go):**

Mwaka 2021, tumekuwa na kaulimbiu isemaya Nitakwenda (I Will Go). Kaulimbiu hii ni ujumbe unaokwenda kwa kasi ambapo kila mmoja wetu anahusika kwenda na kuwafikia mataifa na kuwafanya kuwa wanafunzi wa Yesu. Pamoja na changamoto ya Corona, Bwana ameendelea kuwa pamoja nasi katika kutekeleza kaulimbiu NITAKWENDA (I WILL GO).

## KUTEKELEZA AGIZO LA UTUME

South Nyanza Conference ilipangwa ili kuwaongoza watu wawe wanafunzi wa Yesu Kristo, kutangaza Injili ya milele kwa muktadha wa Ujumbe wa Malaika watatu wa Ufunuo 14:6-12, katika kuwaandaa watu kwa Marejeo yake kwa njia ya kuakisi tabia ya Kristo, kuhubiri, kufundisha, kuponya na kuhudumia.

- SNC katika kuitikia Agizo la Bwana Yesu la kwenda, tulianza kwa uzinduzi maalumu uliofanyika mwezi Dec. 2015 katika mtaa wa Mabatini, Mwanza na mtaa wa Ntuzu – Bariadi mkoani Simiyu.
- Tulianza kwa kujitoa wakfu na kuweka malengo ya Utume Kwanza: Ni Wakati wa Mavuno - “Ushirikishwaji wa Kila Mshiriki”.
- Tulijikumbusha eneo letu la kwenda ni SNC na duniani kote, kwamba tukiamua, tukiomba na kufanya sehemu yetu, tunaweza.

## MIAKA MITANO YA UTUME TULIJIKITA KATIKA MAENEO YAFUATAYO:

1. Ukuaji wa kiroho wa washiriki.
2. Uwezo wa kujitegemea: kugawa Conference.
3. Eneo la Kazi.
4. Rasilimali Watu.
5. Rasilimali Miongozo.
6. Rasilimali Fedha.
7. Ukuaji wa Kanisa.
8. Uinjilisti – Huduma Binafsi
9. Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Conference.
10. Mabadiliko ya taswira (Image Changes): Maendeleo ya majengo.
11. Idara zingine na Taasisi za Kanisa.

### 1. UKUAJI WA KIROHO.

Mungu kwanza, umekuwa ni msisitizo wetu kwamba kila mshiriki Mungu awe nafasi ya kwanza. Njia za kumfahamu Mungu zilizotumika kwa njia ya usomaji wa Biblia kwa mpango, kusoma vitabu vya Roho ya Unabii, kuomba na kufunga, usomaji wa mwongozo wa shule ya sabato, kesha la asubuhi na kitabu cha kila mwaka pamoja na majuma ya maombi ambayo yameendeshwa na idara mbambali katika Conference yetu. Kwa neema ya Mungu alituwezesha kufikia hatua ya kugawa South Nyanza Conference.

### 2. UWEZO WA KUJITEGEMEA: KUGAWA SOUTH NYANZA CONFERENCE.

Eneo la Utume kabla ya kugawa Conference lilikuwa na mikoa 4 Mkoa wa Mwanza kuondoa Wilaya ya Ukerewe, Geita kuondoa Wilaya ya Chato, Simiyu na Shinyanga lenye wakazi 6,920,730 kulingana na sensa ya mwaka 2012.




*Picha 1: Ramani ya Jimbo la Nyanza Kusini (SNC) kabla ya kugawanywa.*

Kazi ya Bwana iliendelea kukua kwa kasi, Februari 20, 2020 SNC iligawanywa rasmi na kutupatia Field inayoitwa Nyanza Gold Belt Field (NGBF) makao makuu yakiwa Kahama. Leo hii tuna SNC yenye mikoa miwili Simiyu na Mwanza ukiondoa Wilaya ya Ukerewe na Sengerema. Field Mpya NGBF ina mikoa miwili Shinyanga, Wilaya ya Sengerema - Mwanza na Mkoa wa Geita ukiondoa Wilaya ya Chato.



*Picha 2:Siku ya tukio la kugawa rasimi SNC na kutupatia Field inayoitwa Nyanza Gold Belt Field iliyofanyika Kahama Feb 20, 2020.*

## 3. ENEO LETU LA KAZI.

Eneo la Utume katika Conference ya South Nyanza linaundwa na mikoa miwili; Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Mwanza ukiondoa Wilaya ya Ukerewe na Sengerema. Eneo la utume lina takribani wakazi 4,011,519 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Uwiano wa mshiriki mmoja kwa wakazi ni 1:24.




*Picha 3:Ramani ya Jimbo la Nyanza Kusini (SNC) baada ya kugawanywa Februari 20, 2020.*

## 4. RASILIMALI WATU.

- Tulianza safari tukiwa na watumishi 629 kufikia Dec. 2019 kabla ya kugawanywa Conference tulikuwa 822 ongezeko la watumishi 193 kwa miaka 4.
- Baada ya kugawanywa SNC Feb. 2020 tulibaki na watumishi wapatao 552, kufikia Jun. 2022 watumishi ni 742 ongezeko la watumishi 190 kufikia Jun. 2022.
- Hapa chini ni jedwali linaloonesha jumla ya idadi ya watumishi wa Conference na Taasisi zake tangu tulipoanza muhula mrefu 2016 hadi Jun. 2022 kabla na baada ya kugawanywa Conference: -

| Watumishi | Kabla ya Kugawa SNC | | Ongezeko | Baada ya Kugawa SNC | | Ongezeko 2020 hadi Sep. 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jan. 2016 | 2019 | Miaka 4 | Jan. 2020 | Jun. 2022 | |
| Idadi ya Wachungaji | 73 | 123 | 38 | 70 | 94 | 24 |
| Wahasibu | 24 | 22 | -2 | 18 | 24 | 6 |
| Wakaguzi wa Ndani | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 1 |
| Walimu | 62 | 64 | 2 | 65 | 75 | 10 |
| Makatibu muhtasi | 10 | 14 | 4 | 11 | 13 | 2 |
| Waganga | 8 | 13 | 5 | 11 | 18 | 7 |
| Wauguzi | 19 | 33 | 14 | 25 | 36 | 11 |
| APD | 5 | 8 | 3 | 4 | 3 | -1 |
| Teknohama (IT) | 1 | 2 | 1 | 4 | 6 | 2 |
| Meneja Milki | 1 | 1 | - | 1 | 1 | - |
| Watumishi wengine | 69 | 75 | 6 | 78 | 78 | - |
| Wainjilisti wa Vitabu | 353 | 463 | 110 | 263 | 391 | 128 |
| **Jumla ya Watumishi wote** | **629** | **822** | **181** | **552** | **742** | **190** |



*Picha 4: Watenda kazi katika moja ya semina zilizoendeshwa katika kipindi cha 2016 - 2022.*

## 5. RASILIMALI MIONGOZO.

Kuridhia mfumo na sera zinazofanikisha umoja wa Kanisa:

- Wachungaji walipata semina na malezi ya kichungaji na kuzingatia ratiba za kazi zao.
- Nyaraka na semina za Uongozi namna ya Kulinda umoja wa Kanisa kwa kuuongoza na kufanya shughuli zake kufuatisha mifumo, Sera, na Miongozo ya Kanisa.
- Watumishi walioajiriwa walipewa South Nyanza Conference workers' handbook.
- Makanisa walinunua miongozo ili kuboresha uongozi ufuatao mfumo wa Kanisa.
- Semina zilitolewa kwa watumishi wote kila mwanzo wa mwaka kwa utumishi bora walioitiwa.
- Semina za uongozi zilitolewa kwa viongozi wote wa makanisa zilizowaita kujitoa kikamilifu kulipenda Kanisa na kulithamini, kutetea Sera, Kanuni, taratibu na miongozo yote ya Kanisa hili.



*Picha 5: Semina za uongozi kwa kanda ya Mwanza iliyofanyika katika kanisa la Mabatini.*

## 6. RASILIMALI FEDHA: UWAKILI.

- Idara ya Uwakili kushiriki kikamilifu katika msukumo wa Mungu Kwanza kwa kuwakumbusha waumini utoaji kwa mpango ni pamoja na majuma ya maombi ya Uwakili yaliyoendeshwa na semina mbalimbali zilitolewa kwa moyo mmoja. Washiriki wamemtolea Bwana mali zao za fedha, mazao, mifugo iliyorudishwa ghalani inaonesha moyo wa kwenda unazidi kukua, ambapo wamejitoa kutumia talanta kwa kazi ya Bwana. Tunamshukuru Bwana kwa mwitikio huu wa kumfanya Mungu kuwa wa kwanza na mengine baadaye.








- Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya matoleo yamekuwa yakiendelea kupanda kila mwaka pamoja na kugawa Conference na kubakia mikoa miwili ya Mwanza na Simiyu bado matoleo kwa ujumla hayakushuka, bali yameongezeka. Hii ni kuonesha kwamba huduma za kiroho zimeimarishwa. Mungu atukuzwe. Hebu fuatilia matoleo katika jedwali hapo chini linaloonesha matoleo ya kila mwaka tangu 2016 hadi June 2022 kabla na baada ya kugawanywa Conference.

**Matoleo ya Zaka, Sadaka na Sadaka ya kambi tangu mwaka 2016 – June 2022 ni kama ifuatavyo:**

| Mwaka | Mikoa | Zaka | Sadaka | Makambi |
|---|---|---|---|---|
| **2016** | 4 | 3,557,880,265.98 | 1,243,094,078.22 | 183,210,371.00 |
| **2017** | 4 | 3,896,501,401.42 | 1,324,502,195.76 | 196,493,191.40 |
| **2018** | 4 | 4,434,941,450.72 | 1,774,233,732.64 | 284,787,527.33 |
| 2019 | 4 | 4,948,271,621.95 | 1,947,041,676.23 | 198,968,672.00 |
| **2020** | 2 | 3,594,542,376.45 | 1,436,010,253.27 | 270,629,567.65 |
| **2021** | 2 | 3,779,091,077.33 | 1,534,894,040.74 | 321,308,598.01 |
| **June 2022** | 2 | 2,052,414,759.35 | 817,135,057.61 | - |
| **JUMLA** | | **26,263,642,953.02** | **10,076,911,034.47** | **1,455,397,927.43** |

- Ofisi ya fedha kwa kushirikiana na Idara ya Uwakili katika msukumo wa Mungu Kwanza, mwaka 2020 tulipokea mfumo mpya wa matoleo ya sadaka Church Financial Management System (CFMS) na kutoa semina kwa washiriki. Januari 2022 tulianza kutumia mfumo huu rasmi ambapo washiriki waliojisajiri kwenye mfumo ni 15% ya washiriki SNC.

## CHAMA CHA ATAPE SNC.

Wanachama wa ATAPE SNC ambao ni wanataaluma na wajasiriamali wamekuwa na mikutano na semina mbalimbali, wametoa huduma mbalimbali ndani na nje ya Conference kama vile kufanya kazi ya utume kwa kutoa mali zao, muda wao, wametoa huduma kwa jamii ndani na nje ya Conference, wamejenga makanisa sehemu mbalimbali za Conference. Baadhi ya huduma hizo ni katika sherehe za jubilee madaktari walipima na kutoa ushauri kwa watu 1785, viongozi wa ATAPE walitembelea mitaa yote ya Kanda ya Bariadi na Dutwa kutoa Semina pamoja na mahubiri yaliyofanyika Bariadi, wameshiriki katika ujenzi wa Hospitali ni pamoja na madakitari kutoa huduma kwa wagonjwa kule Heri Hospital - Kigoma.



*Picha 6: Viongozi wa ATAPE walipoendesha semina ya kuamsha matumizi ya talanta katika Kanda ya Bariadi na Kanda ya Dutwa.*

## 7. UKUAJI WA KANISA:

Ikiwa ni matokeo ya ushirikishwaji wa kila mshiriki katika kutekeleza agizo la utume ni pamoja na Malezi, Utunzaji Wa Washiriki na Kutumia Mfumo Wa ACMS. Kwa pamoja katika kunia mamoja tumeweza kugawa Conference, kugawa mitaa mikubwa ikiwa ni matokeo ya ushirikishwaji.

- Tulianza muhula huu mwaka 2016 tukiwa na mitaa 64 kufikia Dec. 2019 kabla ya kugawa Conference mitaa 91 ongezeko la mitaa 27; makanisa yalikuwa 722 kufikia Dec. 2019 makanisa yalikuwa 862 ongezeko la makanisa 140; tulianza na washiriki 144,111, kufikia Dec. 2019 washiriki walikuwa 248,876 ongezeko la washiriki 104,765 kwa miaka 4.
- Feb, 2020 baada ya kugawanywa tulianza na mitaa 54 kufikia Juni 2022 robo ya pili tuna mitaa 78 ongezeko la mitaa 24; makanisa yalikuwa 473 kufikia Juni 2022 tuna makanisa 639 ongezeko la makanisa 166. Upande wa washiriki walikuwa 138,489 kufikia Juni 2022 washiriki 163,979 ongezeko la washirki 25,490.
- Pamoja na changamoto ya ugonjwa wa CORONA kwa neema ya Bwana waumini wapya waliobatizwa ni 41,355 na washiriki waliorejeshwa na kubatizwa ni 1,158. Jumla ya watu waliobatizwa 2020 – Juni 2022 ni 42,513.
- Uwiano wa mshiriki mmoja kwa wakazi katika Conference yetu ni 1:24 kufikia June 2022. Uwiano huu unahitaji umoja wetu wa kila mshiriki kujitoa kikamilifu katika kutekeleza kaulimbiu NITAKWENDA na kuwafikia watu kwa kusudi la kuwafanya kuwa wanafunzi wa Yesu.
- Kufikia Juni 2022 tumefanikiwa kuingiza washiriki katika mfumo wa ACMS kwa asilimia 96 %.




*Kielelezo 1: Wastani wa mshiriki kwa wakazi katika SNC kufikia June 2022.*




*Kielelezo 2: Takwimu za washiriki katika mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za washiriki (ACMS).*

## 8. UINJILISTI: USHIRIKISHWAJI WA KILA MSHIRIKI (TMI).

Mahubiri ya TMI yamefanyika sehemu mbalimbali za Conference. Katika zoezi zima la ushirikishwaji wa kila mshiriki, tumekuwa na mahubiri ya mlipuko yaliyoendeshwa na wahubiri wa kimataifa, viongozi wetu wa Unioni Conference, Mitaa, Kanisa mahalia na idara zote walifanya kazi kama timu ndani ya Conference. Ushirikishwaji wa kila mshiriki katika mahubiri ya TMI ambapo wachungaji, wake za wachungaji, Wainjilisti wa vitabu, walei, wanawake, vijana, watoto, ATAPE, ASSA, TUCASA na Mawasiliano kwa kutumia technolojia ya leo; kwa pamoja Bwana alikuwa pamoja nasi katika huduma ya kuwaleta waumini wapya kwa yesu na kurejesha walioliacha Kanisa kurudi kundini.

**Mahubiri 2 yaliyofanyika SNC na kurushwa ndani na nje ya nchi ni Mabatini na CCM Kirumba kama ifuatavyo:**

1. Mahubiri ya Ushindi Hatimaye mwaka 2017 yaliyosimamiwa na chama cha ATAPE na kurushwa na vyombo vya habari kutokea viwanja vya Kanisa la Mabatini na kufikia sehemu mbalimbali za Tanzania na nje ya nchi na muhubiri Mch. David Mbaga ambapo watu 9,407 walibatizwa tokea SNC.



*Picha 7: Baadhi ya watu waliobatizwa SNC katika Mahubiri ya Ushindi Hatimaye Mabatini-Mwanza.*

2. Mwaka 2018 Bwana alileta mahubiri ya Ufunuo wa Matumaini, Tumaini la Leo na Mch. na Dkt. Mark Finley ambapo zaidi ya watu 19,000 walibatizwa. Yesu aliinuliwa na kujulikana ndani na nje ya Tanzania.




*Picha 8: Mahubiri ya Ufunuo wa Matumaini, Mch. & Dr. Mark Finley CCM Kirumba-Mwanza 2018.*

**Mahubiri yaliyofanyika sehemu zingine za Tanzania ambayo Conference ilishiriki:**

Tunamshukuru Mungu kwa Mahubiri yaliyorushwa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kutokea katika vituo vya mahubiri vifuatavyo: Mbeya - Tumekaribia Nyumbani, Kinyerezi – Nyumbani Hatimaye, Chato – Mungu Kwanza, Dodoma – Uzoefu wa Nguvu ya Mungu, Hedaru – Tumaini Litokalo Juu, Kizota – Shangwe katika Njia yake, Nyamongo – Amani itokayo Juu na Karatu – Ukweli Unaokuweka Huru.

Kupitia mahubiri yaliyofanyika sehemu zingine Tanzania SNC tulibatiza watu 90,701.

Kutokana na mahubiri yote yaliyofanyika 2016 – Agosti 2022 kwa njia ya Ushirikishwaji wa Kila Mshiriki TMI na kaulimbiu Nitakwenda watu 119,108 walibatizwa SNC. Jina la Bwana litukuzwe.

**Uinjilisti Kwa Njia ya Mahusiano.**

- Mahusiano katika uhalisia wake Malaika Beach Hotel ambapo Mch. Mark Finley akiwa na Viongozi mashuhuri na Wajasiriamali alishiriki nao Neno la Mungu ni pamoja na futali ya jioni na wenzetu Waislam kipindi cha mahubiri ya Ufunuo wa Matumaini.



*Picha 9: Mch. Mark Finley, Viongozi na Wajasiriamali.*

- Viongozi na Wachungaji katika Conference yetu walitembelea Viongozi wa Serikali katika mikoa minne Kufahamiana na viongozi hao na kuwajulisha Kanisa na Utume wake, wakiomba nao na kuwapatiaVitabu 70 vya Afya na uzima pamoja na Tumaini Kuu.
- Huduma ya AMR: Wenzetu Waislam walitutembelea katika Kanisa la Pasiansi, Kanisa la Kirumba, Nyegezi, Nyakato na kushiriki pamoja katika futali ya jioni. Bwana awabariki kwa huduma hii.




*Picha 10: Ndugu zetu Waislam walipotutembelea katika Kanisa la Kirumba.*

**Sherehe za Jubilee:**
Katika Conference yetu Kanisa la Kirumba tulifanya sherehe ya miaka hamsini Jubilee ya kuanzishwa kwa Kanisa la Waadventista wa Sabato katika Jiji la Mwanza iliyofanyika mwaka 2016.

**Matukio Yaliyogusa Mioyo Yetu:**
Tumekuwa na matukio mengi yaliyogusa mioyo yetu na hisia zetu. Tutaje machache:

- Mkuu wa mkoa wa Mwanza, Mhe. Eng. Robert Gabriel alishiriki katika kufanikisha ujenzi wa nyumba ya Mchungaji Mtaa wa Shamaliwa na Kanisa la Kirumba.
- Mhe. Antony Mtaka, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu alishiriki TMI kwa kugharamia zaidi ya nusu ya gharama wakati wa mahubiri ya TMI Ngulyati. Zaidi ya watu 136 walibatizwa. Pia alisaidia sana kufanikisha kambi la pekee la Bariadi-Simiyu. Gharama zote za kusafirisha wahudumu zaidi ya wanne toka ndani na nje ya Tanzania na Kwaya tatu alilipia yeye mwenyewe.
- Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Mhe. Josephine Matiro, alishiriki TMI na kuabudu nasi Sabato ya tarehe 24/06/2017

kisha kuomba kila Robo lesson ikitoka asipitwe. Baada ya ibada aliungana na Mwenyekiti wa Union kukabidhiwa Jengo la kutunza wagonjwa wa ukoma Nkolandoto lililokarabatiwa na mitaa 3 ya Shinyanga, Lubaga na Ushirika kwa kushirikiana na Vijana wa Mitaa hiyo. Siku hiyo wakoma walipewa vitu mbalimbali na kitoweo aina ya mbuzi, n.k.

- Mshiriki toka mtaa wa Buswelu SNC alitoa mabati 527.
- Mshiriki wa Buswelu alitoa mabati 477 kusaidia makanisa ya vijijini – Masumbwe na Dutwa.
- Mshiriki alitoa Tsh. 3.6 Milion kusaidia kuezeka makanisa ya Vijijini na kununua viti vya ibada katika chumba cha maombi Makao Makuu SNC.
- Baadhi ya washiriki wametoa viwanja vya kujenga makanisa.



*Picha 11: Mkuu wa mkoa wa Mwanza, Mhe. Eng. Robert Gabriel na Mwenyekiti wa SNC Pr. Beatus Mlozi katika ufanikishaji wa ujenzi wa nyumba ya Mchungaji Mtaa wa Shamaliwa.*



*Picha 12: Sherehe fupi Mwenyekiti wa Union akimkabidhi Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Jengo la wagonjwa wa ukoma lililokarabatiwa huko Nkolandodo 2017.*

## KITENGO CHA GLOBAL MISSION.

Kitengo cha Global Mission wameweza kuendesha semina kwa Walei (Pioneers), ili kuwa tayari kutumwa katika maeneo mapya na kufungua kazi. Semina ilishirikisha walei wote katika Conference, Kanda na mitaa. Makanisa yamejengwa katika maeneo mapya, Vyombo vya usafiri vimetolewa kurahisisha huduma, mitaa mipya imeanzishwa ni pamoja na kukamilisha miradi 4 iliyofadhiliwa na ECD.



*Picha 13: Baadhi ya vyombo vya usafiri vilivyotolewa na makanisa yaliyojengwa chini ya mpango wa Global Mission.*



*Picha 14: Biblia zikigawanywa kwa watu kupitia mradi wa Global Mission.*

## 9. UJENZI WA OFISI YA CONFERENCE.

Tarehe 22/05/2022 tulikuwa na sherehe kubwa ya uzinduzi wa kiwanja cha ujenzi wa ofisi mpya ya makao Makuu ya South Nyanza Conference Katika eneo la Mwananchi, Wilaya ya Nyamagana. Mgeni Rasmi katika sherehe hizi alikuwa Mwenyekiti wa Northern Tanzania Union Conference (NTUC), Mch. Dr. Godwin Lekundayo, sherehe hizi ziliandamana na utoaji wa Sadaka ya hiari kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi. Tunamshukuru Mungu kwa mwanzo huu na ujenzi umeshaanza.




## 10. MABADILIKO YA TASWIRA (IMAGE CHANGES).

Tunamshukuru Bwana Wachungaji na washiriki SNC wameelewa umuhimu wa kushughulikia mambo matatu muhimu na ya msingi (Basic needs) kwa maendeleo ya Kanisa kiroho na kimaisha ambayo ni kujenga Kanisa zuri, eneo zuri la makambi na nyumba ya Mchungaji kwa kila mtaa.

## MAENDELEO YA MAJENGO.

**Ujenzi wa Makanisa: Uinjilisti Na Kupanda Makanisa Maeneo Mapya.**

Tunamshukuru Bwana wazo la kupanda makanisa kila mahali limepokelewa kwa moyo mmoja na kufanyiwa kazi na mitaa, makanisa vijijini na mijini. Mitaa, Idara mbalimbali kabla ya kuhubiri walinunua viwanja na wengine mahubiri yalienda sambamba na ujenzi wa Kanisa. Njia hii imethibitisha kuwa na malezi mazuri kwa washiriki wapya (Nurturing and Retention).

- Baadhi ya Makanisa na mitaa walinunua viwanja na kujenga makanisa kwa muda mfupi. Hii ni mifano michache: Mtaa wa Nyegezi, Mtaa wa Nyakato, mtaa wa Mkula, Mtaa wa Ntuzu, Ngulyati, Ndagalu, n.k.

**Kubadili Taswira ya Makanisa.**

- Mitaa iliyo na uwezo kusaidia mitaa isiyo na uwezo kuezeka makanisa, mfano Nyegezi kusaidia kuezeka kanisa la Ngambo ya Mto Mtaa wa Makao.
- Majengo ya kanisa yaliyokaa muda mrefu kwa kusaidiana na Conference kubadili taswira ya Kanisa mfano: Mlima Nuru Mtaa wa Kiseke, Ilemela Mtaa wa Pasiansi, n.k.

**Ujenzi wa Nyumba za Wachungaji.**

Tunashukuru wazo la kujenga nyumba za wachungaji limepokelewa vizuri na Wachungaji na washiriki SNC, 40% ya mitaa wamejenga nyumba za wachungaji, 15% wako katika hatua ya kumalizia, 39% wameanza kujenga na 6% bado wanashughulikia viwanja. Wazo hili limetusaidia kuokoa pesa nyingi zilizokuwa zikitumika katika kupanga nyumba za watumishi.

- Ofisi imetoa fedha za kupaua nyumba za wachungaji pamoja na marekebisho kwa ajili ya nyumba za wachungaji katika mitaa 30.

## 11. IDARA ZINGINE NA TAASISI ZA KANISA.

### A. HUDUMA ZA KICHUNGAJI.

**Chama cha Wachungaji.**

- Tunamshukuru; Bwana ameendelea kuongeza jeshi lake. Mwaka 2016 tulianza safari na wachungaji 73 kufikia Dec. 2019 walikuwa 123 ongezeko la wachungaji 50. Baada ya kugawa conference tulibaki na wachungaji 70 kufikia June 2022 wako 94, ongezeko la wachungaji 24.
- Wachungaji waliowekewa mikono muhula huu ni 30.
- Uwiano wa Mchungaji katika kuhudumia makanisa 1:9 na uwiano wa Mchugaji katika kuhudumia washiriki ni 1:2186.
- Wachungaji waliowekewa mikono ambao wako kazini ni 39.
- Wachungaji waliolala mauti 2016 - 2022 wakiwa kazini ni 2 na wastaafu ni 10.



*Picha 15: Tukio la kuwekewa mikono wachungaji katika kanisa la Nyegezi Mei 21,2022.*

**Chama cha Wake za Wachungaji.**

Wamepata mafunzo na semina mbalimbali kuelimisha wake za wachungaji juu ya wajibu wao kwa Mungu, kwa familia na kwa kazi ya Bwana kama wasaidizi wa wachungaji.

Wake za wachungaji siyo wasaidizi wa waume zao tu bali nao wako mstari wa mbele katika kwenda kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu. Wamefanya mahubiri na kujenga Kanisa lililowekwa jiwe la Msingi na Mch., Dkt. Godwin Lekundayo.





*Picha 16: Mch. G. Lekundayo, Mwenyekiti wa Union akiwa katika kanisa la Butundwe ambalo pia aliliwekea Jiwe la Msingi.*

## B. IDARA YA UCHAPISHAJI.

- Idara ya Uchapishaji SNC tangu mwaka 2020 hadi 2022 tuna kanda saba ambazo zinasimamiwa na APDs. Wainjilisti wa vitabu walifanya mahubiri na kugawa vitabu, nguo, sabuni, n.k, watu 3,608 walibatizwa.

- Idara ya Uchapaji Kanda ya Bariadi wamefanikiwa kujenga ofisi kubwa ya kisasa.



*Picha 17: Picha ofisi ya uchapishaji Kanda ya Bariadi.*

## C. IDARA SHULE YA SABATO.

Idara ya Shule ya Sabato 2020 – 2022 wamefanya semina mbalimbali katika Conference yetu. Semina zilitolewa kwa viongozi na walimu wa Shule ya Sabato. Tunamshukuru Mungu kwa ofisi ya Ufunuo Publishing House kwa Miongozo ya Shule ya Sabato ambayo imekuwa ikitufikia kwa wakati.



*Picha 18: Semina za Shule ya Sabato.*

## D. HUDUMA ZA VIJANA, MUZIKI NA CHAPLENSIA.

### Huduma za Vijana.

**Sherehe za Pathfinder Day.**

General Conference Pathfinder Day iliyofanyika CCM Kirumba, Mwanza, SNC, NTUC Tanzania 21 Septemba 2019 ilimalizika kwa ushindi mkubwa. Kupitia tukio hilo SNC vijana wa pathfinder 132 walibatizwa.




*Picha 19: Sherehe za Pathfinder Day ya 69 iliyoadhimishwa Kiulimwengu Mwanza-SNC, Mgeni rasmi akiwa Andres Peralta.*

**Huduma za Vijana kwa jamii.**

Vijana wa Kiadiventista wamehusika katika kutoa huduma mbalimbali kwa jamii, kwa kutoa damu, kugawa vitabu, kujenga nyumba na vyoo kwa wahitaji, ukarabati wa nyumba, kutoa huduma katika magereza, kutembelea wagonjwa hospitali na majumbani, kufanya usafi katika maeneo ya shule, hospitali, miji, pia wametoa vyakula, nguo, na mahitaji mbalimbali kwa jamii.

**Huduma za Muziki:**

Semina za muziki zimetolewa na makongamano ya Muziki yamefanyika ili kuwaelekeza waimbaji kurejea katika muziki wa Kiadventista katika Mitaa, Kanda na Conference yetu kwa ujumla. Tumekuwa na makongomano ya uimbaji yaliyofanyika katika makanisa (Kwaya Day), mitaa, kanda na makongamano yaliyoandaliwa na Conference. Kutokana na semina zilizotolea tunashukuru makanisa na kwaya zilizokubali wito wa kufanya matengenezo ya uimbaji na kurejea kuimba muziki wa Kiadventista, Bwana awabariki.



*Picha 20: Wakufunzi katika Kongamano la Muziki la Conference lililofanyika katika viwanja vya Kanisa la Shamaliwa Feb. 2022.*



*Picha 21:Waumini waliohudhuria semina za muziki Shamaliwa.*

**Huduma za Chaplensia Public Campus Ministry (PCM).**

TUCASA na ASSA wamekuwa na mikutano mbalimbali na semina kwa nia ya kutiana moyo katika maisha ya kiroho wa wapo shuleni na katika vyuo. Wamefanya uinjilist kupitia mahubiri, kutoa huduma kwa jamii ambapo wamejenga makanisa, wamewajengea nyumba wahitaji, wamefanya mahubiri, wamegawa vitabu, wametembelea magereza na kutoa vyakula na mahitaji mengine kwa jamii.

## E. HUDUMA YA MAWASILIANO.

Tumehudhuria mikutano ya Idara ya Mawasiliano GAIN na kuendesha Semina za mawasiliano zilizotolewa kwenye kanda zote za Conference kwa kushirikiana na Ofisi ya Union - NTUC kuhusu utambulisho wa Kanisa letu (Church Identity), utendaji wa kazi katika Idara na mafunzo ya ACMS (Adventist Church Management System) namna ya kuingiza washiriki katika mfumo wa ACMS ambapo tumefanikiwa kwa 96%.

Kwa ushirikiano wetu na TAMC, tumefanikiwa kufungua kituo cha kituo cha Habari (Media Centre) kwa ajili ya kutayarishia vipindi SNC Hope Media ambacho kilizinduliwa Julai 18, 2020.



*Picha 22: Baadhi ya washiriki wa mkutano wa GAIN 2022 uliofanyika jijini Mwanza.*



*Picha 23: Mch. Switta Elias Stevns akizindua Rasmi Hope Media SNC tarehe Julai 18, 2020.*

## F. HUDUMA ZA WANAWAKE (AWM).

Idara ya Wanawake ina kanda 10. Wanawake wamefanya mahubiri maeneo mapya kama vile Mbika Wilaya ya Ushetu mkoani Shinyanga na Mbugani mtaa wa Nkololo na kununua viwanja na kujenga makanisa katika maeneo hayo.

### Chuo Cha AWM VTC.

Tunafurahi kuwajulisha kuwa Chuo Chetu cha Adventist Women Vocational Training C**ollage**(AWMVTC) kilichodumu kwa muda mrefu bila usajili sasa kimesajiliwa rasmi na Serikali (kinatambulika Kiserikali). Tunamtukuza sana Bwana.



*Picha 24: Wanafunzi wa fani ya upishi katika chuo cha AWM VTC.*

## G. IDARA YA WATOTO.

Idara ya watoto imetilia maanani mafundisho na malezi ya watoto. Idara ya watoto wamefanikiwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa idara na walimu wa watoto makanisani ikiwa ni pamoja na kutengeneza zana za kufundishia watoto makanisani. Watoto wameendesha mahubiri ya hadhara na sehemu mbalimbali za Conference, pamoja na program za watoto wakati wa sikukuu za vibanda.



*Picha 25: Huduma za watoto katika kanisa la Nyegezi.*

## H. HUDUMA YA AFYA NA KIASI.

**Ujenzi wa Hospitali**

Kazi kubwa SNC 2016 – 2020 ilikuwa ni ujenzi wa Hospitali, gorofa ya chini na ya kwanza zimekamilika na zinatumika, gorofa ya pili imekamilika kwa sehemu na gorofa ya tatu hadi ya tano finishing bado.

Hata hivyo tunafurahi kuwajulisha kwamba March 30, .2020 saa 5:30 asubuhi Kituo chetu cha Afya (Pasiansi Health Center) kilipandishwa hadhi kutoka kituo cha Afya Pasiansi na kuwa SDA Pasiansi Hospital. Haikuwa rahisi, tunamshukuru Mungu kufikia hatua hii.

Huduma mbalimbali za afya zinaendelea kutolewa katika Hospitali yetu ya SDA Pasiansi Hospital, inatoa huduma za upasuaji maalum, macho, meno, mionzi na uangalizi maalumu kwa watoto wanaozaliwa na changamoto na kupewa uangalizi wa karibu.




*Picha 26: Jengo la Hospitali ilivyokuwa 2016 na ilivyo 2022.*

## I. HUDUMA YA ELIMU

Shule zetu zimeendelea kufanya vizuri kitaaluma. Kulingana na matamanio yetu, wanafunzi waliopata Daraja la Kwanza na la pili, wameongezeka na kuvunja rekodi katika muhula huu katika shule zote Bupandagila Sekondari, Nyanza Adventist Sekondari, Ngulyati Sekondari na Bupandagila Adventist Primary School.

**Taswira ya shule zetu:**
Tunamshukuru Mungu kwa shule zetu zote tatu zimefanya vizuri katika swala la miundombinu na majengo.

- **Shule ya Bupandagila Sekondari**: Baadhi maboresho ya huduma shuleni kama vile matumizi ya gas.
- **Shule ya Nyanza Adventist Sekondari:** Baadhi ya maboresho yaliyofanyika shuleni kama vile ujenzi wa Kanisa, Geti, uzio wa shule, matumizi ya gas, n.k.
- **Shule ya Ngulyati Sekondari:** Haya ni baadhi ya maboresho yaliyofanyika shuleni kama vile kujenga Bweni la wavulana lenye uwezo wa kulaza watoto 250, ujenzi wa bwalo, jiko, visima vya maji, n.k.
- **Shule ya Bupandagila Adventist Primary School:** Tumefanikiwa kujenga shule ya Msingi Bupandagila. Ni shule pekee ya Msingi ya Kanisa SNC ambayo inafanya vizuri na idadi ya wanafunzi inaongezeka kila mwaka.

## MIPANGO MBELE YETU.

1. Kutekeleza Agizo la utume: "I Will Go - Make Disciples" Nitakwenda - Kuwafanya Kuwa Wanafunzi kwa nguvu zote.
2. Malezi na utunzaji wa washiriki.
3. Kuhakikisha kila mshiriki anatumia mfumo mpya wa matoleo - Church Financial Management System (CFMS).
4. Kujenga Ofisi ya Conference.
5. Kufundisha uongozi wa Kikristo.
6. Kuhakikisha kila mtaa unajishughulisha na mabadiliko ya taswira (Image changes).



*Picha 27: Muonekano wa juu wa jengo jipya la ofisi za jimbo ambalo ujenzi wake tayari umeanza.*

# TAARIFA YA OFISI YA KATIBU



**PR. NICODEMO NTABINDI.**

**KATIBU MKUU**

SNC

## UTANGULIZI

Awali ya yote, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa mwenyezi Mungu aliyetusaidia kuifikia siku hii ya leo ya mkutano mkuu wa Kanisa la South Nyanza Conference, Natoa shukrani zangu kwa uongozi wa Union ya Kaskazini mwa Tanzania, Mwenyekiti, Katibu na Mhazini, natoa shukrani zangu za kina kwa wajumbe wa Kamati Kuu Tendaji ya South Nyanza Konferensi kwa ushirika wao mkubwa katika kazi zote walizopewa na Konferensi hii kupitia katiba yake, naam nawashukuru wachungaji wenzagu katika Konferensi yote katika mitaa na katika taasisi zote, na tena nawashukuru watendakazi wote wa ofisi kuu ya South Nyanza Conference na watumishi katika taasisi zote za konferensi, naam ninatoa shukrani zangu za dhati kwa washiriki wote kwa kazi njema zilizotendwa kupitia mshiriki mmoja mmoja na kwa Kanisa lote kwa ujumla. Katika ujumla wake nawashukuru viongozi waliotutangulia.

South Nyanza Conference ndani ya kipindi hiki tangu Sept 2016 hadi Marchi 2022 imeweza kufanya kazi nyingi kupitia makanisa yake na katika kueneza injili, washiriki waliongezeka, konferensi nyingine imezaliwa, mitaa imeongezeka, makanisa na makundi yakaongezeka, watumishi wakaongezeka, taasisi zikaongezeka na hivi leo ni matokeo ya hiyo kazi iliyofanyika kupitia watendaji wa makanisa ya SNC na wachungaji wake.



*Picha 1: Wajumbe wa kamati kuu ya SNC.*

## KIPINDI CHA SNC KATI YA 2016 – 2019

Kwa kipindi chote hiki South Nyanza Conference imekuwa ikifanya kazi zake za kulea waumini wake katika eneo la mikoa minne ambayo ni Geita, Shinyanga, Simiyu na Mwanza bila wilaya ya Ukerewe. Makao makuu ya konferensi yakiwa Pasiansi, barabara ya Airport, Kata ya KaweKamo, Wilaya ya Ilemela, mkoa wa Mwanza. Katika kipindi hiki konferensi ilijulikana kwa kuwa na kanda sita za kijimbo ambazo zilikuwa ni Bariadi, Magu, Maswa, Mwanza, Shinyanga na Uzinza – pineapple zone. Kwa kipindi hiki mitaa, makanisa na washiriki viliongezeka. Hapa chini ni ulinganifu wa mitaa, makanisa na washiriki katika kipindi hiki.

**Takwimu za vituo vya utume na idadi ya washiriki 2016 hadi 2019.**

| Mwaka | Mitaa | Makanisa | Makundi | Washiriki |
|---|---|---|---|---|
| 2019 | 91 | 862 | 690 | 248,876 |
| SEP 2015 | 64 | 712 | 506 | 118,755 |
| Ongezeko | 27 | 150 | 184 | 130,121 |
| Asilimia Ong | 42% | 21% | 36% | 109% |

NB. Utaona kuwa washiriki waliongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka washiriki 118,755 Septemba 2015 hadi kufikia washiriki 248, 876 hapo desemba 2019 kwa mikoa yote minne.




*Kielelezo 1: Ulinganifu wa washiriki na makanisa kati ya Septemba 2015 na Desema 2019.*

Hapa chini ni jedwali linaloonyesha uhusiano wa shughuli nzima iliyokuwa ikifanyika katika maeneo haya ya mikoa minne yaani Mwanza bila Ukerewe, Geita bila Chato, Shinyanga na Simiyu.

| MKOA | IDADI MITAA | IDADI MAKANISA | IDADI MAKUNDI | IDADI WASHIRIKI | WAKAZI | UWIANO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MWANZA | 29 | 268 | 186 | 53,436 | 2,427,362 | 1:44 |
| SIMIYU | 17 | 225 | 150 | 43,570 | 1,584,157 | 1:35 |
| GEITA | 11 | 153 | 127 | 28,188 | 1,374,403 | 1:47 |
| SHINYANGA | 08 | 82 | 144 | 18,917 | 1,534,808 | 1:80 |
| JUMLA | 64 | 728 | 607 | 144,111 | 6,920,730 | 1:47 |




*Kielelezo 2: Mgawanyiko wa washiriki kimkoa, Desemba 2015.*

Kwa jedwali hili hapo juu utaona kuwa mkoa wa Mwanza ikiwemo Wilaya ya Sengerema na Buchosa ulikuwa na mitaa 29 Makanisa 268, makundi 186 na washiriki 53,436 wakati wakazi wake walikuwa ni 2,427,362. Kwa upande wa Simiyu jumla ya mitaa ilikuwa ni 17, Makanisa 225, Makundi 150, idadi ya washiriki 43, 570, huku wakazi wa mkoa huu wakiwa 1,584,157.

**Ramani ya South Nyanza Conference 2016 hadi Feb 2019.**




*Picha 2: Ramani ya Jimbo la Nyanza Kusini (SNC) kabla ya kugawanywa.*

## MITAA NA WASHIRIKI KABLA KUIGAWA KONFERENSI.

Katika kipindi hiki cha kuigawa South Nyanza Conference (SNC) ilizaliwa field inayoitwa tangu wakati huo: Nyanza Gold Belt Field. {NGBF). Kipindi hiki kinabeba umuhimu wa taarifa inayotolewa kwetu kwa kuwa sehemu ya kijiografia ya inayoitwa South Nyanza Conference imebadilika, idadi ya mitaa, idadi ya makanisa, idadi ya makundi, eneo la kijiographia na sehemu ya washirika ilikatiwa katika sehemu inayoitwa NGBF – Nyanza Gold Belt Field. Mgawanyo ulioleta kuwa na taarifa mpya ya mitaa, makanisa, makundi na washiriki na hata eneo na sehemu ya mkoa wa Mwanza mwishoni mwa mwaka 2019. Hata hivyo kazi ilisonga mbele na mwishoni mwa mwaka idadi iliongezeka katika kila Nyanja.

## Takwimu za iliyokuwa SNC Mwaka 2015 - mwaka 2019.

| Mwaka | Mitaa | Makanisa | Makundi | Washiriki |
|---|---|---|---|---|
| Des 2015 | 64 | 728 | 607 | 144,111 |
| Des 2016 | 64 | 737 | 591 | 147,785 |
| Des 2017 | 78 | 771 | 642 | 189,244 |
| Des 2018 | 85 | 800 | 686 | 219,282 |
| Des 2019 | 91 | 862 | 690 | 248,876 |




*Kielelezo 3: Ukuaji wa Kanisa (Makanisa na Makundi ) kuanzia 2015 mpaka 2019.*

## Ulinganifu wa Watumishi wote wa South Nyanza Conference 2016 hadi 2019.

| Na | Taasisi | Mwaka 2016 | Mwaka 2019 |
|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu | 107 | 153 |
| 2 | Bupandagila H/S | 63 | 53 |
| 3 | Nyanza Sec | 43 | 48 |
| 4 | Pasiansi SDA Hosp | 43 | 71 |
| 5 | Ngulyati Sec | 20 | 21 |
| 6 | Wainjilisti cheti 2/3 | 128 | 128 |
| 7 | Bupandagila Pri | - | - |
| 8 | VTC | Watumishi - mkataba | Watumishi - mkataba |
| Jml kuu | | 404 | 474 |




*Picha 3: Makao makuu ya Jimbo la Nyanza Kusini (SNC).*

### Watumishi Ofisi kuu ya SNC bila watumishi wa Taasisi 2016 na 2019.

| Na | Watumishi | 2016 | 2019 |
|---|---|---|---|
| 1 | Wachungaji | 73 | 133 |
| 2 | Wahasibu | 10 | 11 |
| 3 | Madaktari | 01 | 01 |
| 4 | Walimu | 02 | 01 |
| 5 | Teknohama - IT | 01 | 01 |
| 6 | APDD | 04 | 08 |
| 7 | Katibu Wahitasi | 05 | 08 |
| 8 | Madereva | 01 | 01 |
| 9 | Wahudumu Usafi | 02 | 03 |
| 10 | Walinzi | 05 | 05 |
| 11 | Meneja Milki | 01 | 01 |
| 12 | Meneja Miradi | 00 | 00 |
| 13 | Walei Maeneo Mapya | 00 | 03 |
| | **Jumla Kuu** | **106** | **153** |

**Ulinganifu wa watumishi kituo cha Afya Pasiansi/ Kasamwa na Hospitali ya Pasiansi. 2016 na 2019.**

| Makundi | Watumishi Pas/Kasamwa 2016 | Watumishi Pasiansi Hosp. 2019 |
|---|---|---|
| Waganga | 4 | 11 |
| Wauguzi | 10 | 31 |
| Maabara | 2 | 07 |
| Madawa | 1 | 04 |
| Wahasibu | 4 | 05 |
| Ulinzi | 2 | Makampuni |
| Usafi | 4 | 04 |
| Katibu wa Afya | - | 01 |
| Mapokezi | - | 04 |
| IT | - | 01 |
| Wahandisi | - | 01 |
| Jumla | 27 | 71 |

*NB. Watumishi mwaka 2016 kwa kituo cha Afya ilijumuisha na kituo cha Kasamwa ambacho kwa sasa kiko NGBF.*




*Picha 4: Jengo la kilichokua Kituo cha Afya cha Pasiansi (Kwasasa Hospitali ya SDA Pasiansi).*

**Watumishi katika shule ya Sekondari Bupandagila 2016 na 2019.**

| Makundi | Watumishi 2016 | Watumishi 2019 |
|---|---|---|
| Waalimu | 21 | 27 |
| Wahasibu | 3 | 03 |
| Wengineo | 35 | 23 |
| Jumla | 59 | 53 |

**Watumishi katika shule ya Sekondari Nyanza 2016 na 2019.**

| Makundi | Watumishi 2016 | Watumishi 2019 |
|---|---|---|
| Waalimu | 27 | 27 |
| Wahasibu | 4 | 04 |
| Wengineo | 16 | 17 |
| Jumla | 47 | 48 |

**Watumishi katika shule ya Sekondari Ngulyati 2016 na 2019.**

| Makundi | Watumishi 2016 | Watumishi 2019 |
|---|---|---|
| Waalimu | 12 | 10 |
| Wahasibu | 2 | 02 |
| Wengineo | 5 | 09 |
| Jumla | 19 | 21 |



*Picha 5: Watumishi wa Shule ya Sekondari ya Bupandagila.*

## KIPINDI CHA SNC TANGU MWAKA 2020 HADI 2022.

South Nyanza Conference tangu Februari 2020. Iligawanywa rasmi na kuzaa Field iliyokuwa imependekezwa kufanywa kama eneo la majaribio tangu desemba 2018. Baada ya kupangwa huku kwa Field hii Mpya South Nyanza Conference ilibaki katika eneo la kijografia lenye mikoa miwili kama ilivyobainishwa hapo kwanza. Kubaki kwa eneo hili kulipelekea pia kuangalia upya Katiba ya SNC na upangaji upya wa vituo vya kazi kiutume. Eneo la SNC huchukua mikoa miwili ya Mwanza bila Wilaya ya Ukerewe, Sengerema, Buchosa na Mkoa wa Simiyu.

Tangu wakati huo kazi ya Mungu ilichukua sura nyingine katika kuongeza kazi yake kwa kuwa watumishi wa konferensi waliweza kuyafikia maeneo mengi yaliyo katika konferensi, tofauti na hapo kwanza. Pamoja na hayo mitaa na makanisa vilipangwa ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa watumishi na utumishi

Kwa kuwa ukaribu wa huduma ulichochea makuzi ya washiriki katika ushirika na huduma kwa Kanisa, majengo ya ibada na nyumba za wachungaji viliongezeka katika idadi na ubora toka mwaka hadi mwaka. Hii ilipelekea kuongezeka kwa shughuli nyingi za kiinjilisti zilizowahimiza washiriki kwenda katika kazi ya Mungu na matokeo, imekuwa ni kuongezeka kwa washiriki katika Kanisa katika eneo hili la South Nyanza Conference.

Kanisa South Nyanza Conference linafanya shughuli zake kama agizo la Yesu Kristo linavyoagiza katika Wilaya za Nyamagana, Ilemela, Magu, Misungwi na Kwimba ambayo ni sehemu ya Mkoa wa Mwanza na kwa Mkoa wa Simiyu Kanisa linafanya kazi zake katika Wilaya zake zote ambazo ni Wilaya za Bariadi, Maswa, Meatu, Busega na Itilima. Washiriki walio katika eneo hili ambao ni sehemu ya wakazi wa eneo ilipo South Nyanza Conference, wanashughulika zaidi na shughuli za kilimo kwa aina zake, ufugaji kwa aina zake, biashara kwa aina zake, uchimbaji madini kwa aina zake na shughuli nyingine nyingi

zinazojitokeza na kuwa fursa kwa ujumla. Shughuli hizi zinachangia kwa kiasi kikubwa upatikaji wa zaka na sadaka ambazo ni nyenzo za kuipeleka Injili South Nyanza Conference na sehemu zote liliko Kanisa la waadventista wa Sabato ulimwenguni.

**Eneo la kazi la SNC kuanzia Februari 20, 2020.**




*Picha 6: Ramani ya eneo la kazi la SNC kuanzia Februari 2020.*

**Ulinganifu wa Mitaa Makanisa na Washiriki tangu 2020.**

Washiriki wa South Nyanza Conference tumeendeleza utume kupitia misukumo mbalimbali ya Kanisa ikiwemo "Mungu kwanza" na "Nitakwenda"; misukumo iliyobadilisha ari ya utendaji kwa washiriki na wachungaji wote kwa Pamoja. Katika ari hii wanaume na wanawake kwa marika tofauti, wameunganisha Talanta na Karama zao kupanua ufalme wa Yesu Kristo. Matokeo yake Kanisa la South Nyanza limeongeza mitaa, makanisa, makundi, washiriki, taasisi na wafanyakazi katika ujumla wake.

**Takwimu za Mitaa, Makanisa na Washiriki 2020 hadi Machi 2022.**

| Mwaka | Mitaa | Makanisa | Makundi | Washiriki |
|---|---|---|---|---|
| Jan 2020 | 54 | 501 | 354 | 138,489 |
| Des 2021 | 69 | 585 | 348 | 152,579 |
| Juni 2022 | 78 | 639 | 327 | 163,979 |




*Kielelezo 4: Idadi ya makanisa katika kipindi cha 2020 - 2022.*

## NJIA AMBAZO WASHIRIKI HUONGEZEKA NA KUPUNGUA.

**Njia za kupungua au kupotea kwa washiriki**

i) Kutokujulikana alipo
ii) Kifo
iii) Uasi
iv) Kuhama kwa barua

**Njia za kuongezeka kwa washiriki**

i) Ubatizo
ii) Kuikiri Imani
iii) Kupokelewa kwa barua

Kwa sababu hiyo South Nyanza Conference imepitia uzoefu wa kuongezeka kwa washiriki na kupungua kwa washiriki kupitia njia hizo hapo juu. Hivyo South Nyanza Conference imeongeza washiriki 25,490 kwa kipindi cha miaka hii miwili.

## WATUMISHI KATIKA KONFERENSI YA SNC.

Pamoja na kuigawanya konferensi kulikofanya sehemu ya mitaa, makanisa, makundi na washiriki kuwa sehemu nyingine ya kazi, kwa upande wa Taasisi hitaji la watumishi halikuguswa sana kwa upande mmoja ama mwingine, ingawa sehemu ya ofisi kuu watendakazi waligawanywa na wengine kuitwa kwa sehemu nyingine za kazi.Tangu wakati huo orodha ya wakurugenzi ilipungua sana, kwani wengi waliitwa kwa sehemu nyingine ya utumishi.



*Picha 7: Wachungaji wa SNC pamoja na wake zao.*

South Nyanza Conference zaidi ya kuwa na makanisa mahalia pia inazo Taasisi zinazoendesha shughuli za kielimu, kiafya, malezi na uinjilisti, hivyo kufanya Yesu Kristo kufahamika kupitia utoaji huduma wa taasisi hizi ndani na nje ya konferensi. Taasisi tulizo nazo zina hadhi ya Chuo, Sekondari, Msingi na Hospitali ambazo kila moja inayo timu nzuri ya watumishi wanaotoa huduma stahiki kwa wahudumiwa. Taasisi hizi ni:-

i. Bupandagila High School - BUHICO
ii. Nyanza Adventist Secondary School - NYASECO
iii. Ngulyati Secondary School - NGUSECO
iv. Bupandagila Adventist Primary School - BAPS
v. Vocational Training Center. – VTC
vi. Pasiansi SDA Hospital - PSH
vii. South Nyanza Conference Ofisi Kuu -SNC

## KITUO CHA PASIANSI/ HOSPITALI YA PASIANSI SDA.

Hiki kimepanuka kutoka kuwa Kituo cha Afya hadi kuwa Hospitali ya SDA Pasiansi Hospital iliyoko katika Jiji la Mwanza karibu na yalipo makao makuu ya Konferensi.



*Picha 8: Hospitali ya Pasiansi SDA.*

**Hapa ni Jedwali linaloonyesha watumishi katika Hospitali ya Pasiansi 2020 na 2022.**

| Makundi | Watumishi 2020 | Watumishi 2022 | ongezeko |
|---|---|---|---|
| Waganga | 12 | 15 | 3 |
| Katibu wa Afya | 1 | 1 | - |
| Wauguzi | 26 | 32 | 6 |
| Maabara | 7 | 9 | 2 |
| Madawa | 4 | 9 | 5 |
| Wahasibu | 4 | 7 | 3 |
| Usafi | 5 | 5 | - |
| Mapokezi | 5 | 5 | - |
| IT | 1 | 2 | 1 |
| Wahandisi | - | - | - |
| Jumla | 65 | 85 | 20 |

**Watumishi Katika Hospital ya SDA Pasiansi na Viwango Vyao vya Elimu.**

| Makundi | Uzamili | Shahada | Stashahada | Cheti | Vingine | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Waganga | 2 | 7 | 6 | - | - | 15 |
| Katibu wa Afya | - | 1 | - | - | - | 1 |
| Wauguzi | - | 1 | 22 | 9 | - | 32 |
| aabara | - | 3 | 6 | - | - | 9 |
| Madawa | - | 1 | 7 | 1 | - | 9 |
| Wahasibu | - | 3 | 3 | 1 | - | 7 |
| Usafi | - | - | - | 1 | 4 | 5 |
| Mapokezi | - | - | 2 | 2 | - | 4 |
| IT | - | 1 | 1 | - | - | 2 |
| | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Jumla | 2 | 17 | 48 | 14 | 4 | 85 |

**SHULE YA MSINGI BUPANDAGILA ADVENTIST.**

Shule hii iliyokuwa inafanya kazi chini ya shule ya sekondari Bupandagila, ilipanda hadhi na kuwa shule inayojitegemea tangu Januari 2022.

**Viwango vya elimu kwa watumishi wa shule ya Msingi ya Bupandagila Adventist.**

| Makundi | Uzamili | Shahada | Stashahada | Diploma | Cheti | Vingine | Jml |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | - | 12 | 4 | - | - | - | 16 |
| Wahasibu | - | 2 | - | - | - | - | 2 |
| Waganga | - | - | 1 | - | - | - | 1 |
| Lab. Tech | - | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Wauguzi | - | - | 2 | - | - | - | 2 |
| Wengineo | - | - | 2 | 2 | 7 | - | 11 |
| Jumla | - | 14 | 9 | 3 | 7 | - | 33 |

## SHULE YA SEKONDARI NYANZA.

Hii iliamua kubadili taswira na kuanzisha masomo ya A- Level tangu Aprili 2022 na kuwa shule ya tamanio kwa jiji la Mwanza na majimbo Jirani.

**Watumishi katika shule ya Sekondari ya Nyanza.**

| Makundi | Uza mili | Shaha da | Stashaha da ya Juu | Diplo ma | Che ti | Vingi ne | J ml |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | 5 | 18 | - | 3 | - | - | 26 |
| Wahasibu | - | 4 | 1 | - | - | - | 5 |
| Wengineo | - | - | - | 4 | 6 | 6 | 16 |
| Jumla | 5 | 22 | 1 | 7 | 6 | 6 | 47 |

## SHULE YA SEKONDARI BUPANDAGILA.

Hii shule imekuwa mbaraka kwa kanda ya Bariadi na nje ya South Nyanza.

**Watumishi katika Shule ya sekondari Bupandagila.**

| Makundi | Uza mili | Shah ada | Stasha hada | Diplo ma | Chet i | Vingin e | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | - | 12 | 4 | - | - | - | 16 |
| Wahasibu | - | 2 | - | - | - | - | 2 |
| Waganga | - | - | 1 | - | - | - | 1 |
| Lab Tech | - | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Wauguzi | - | - | 2 | - | - | - | 2 |
| Wengineo | - | - | 2 | 2 | 7 | - | 11 |
| Jumla | **-** | **14** | **9** | **3** | **7** | **-** | **33** |

## SHULE YA SEKONDARI NGULYATI.

Shule hii inaendelea kuwa kivutio kwa mkoa wa Simiyu na Mwanza.

**Watumishi katika Shule ya Sekondari Ngulyati.**

| Makun di | Uzamil i | Shahad a | Stashahad a | Chet i | Vinginevy o | Juml a |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | - | 7 | 3 | - | - | 10 |
| Wahasibu | 1 | - | 1 | - | - | 2 |
| Wengine | - | 1 | - | 1 | 5 | 7 |
| Jumla | 1 | 8 | 4 | 1 | 5 | 19 |

## CHUO CHA UFUNDI STADI (AWM VTC) – SOUTH NYANZA CONFERENCE.

Watumishi katika Chuo cha VTC – South Nyanza Conference

| Makundi | Shahada | Stashahada | Cheti | Level III/II | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | - | 1 | 2 | 3 | 6 |
| Wahasibu | 1 | - | - | - | 1 |
| Matron | - | - | 1 | - | 1 |
| Jumla | 1 | 1 | 3 | 3 | 8 |

## WAINJILISTI WA VITABU

| Cheti cha Tatu (Credential) | Cheti cha Pili (Licence) | Cheti cha Kwanza (Identification) | Wa muda (Part time) |
|---|---|---|---|
| 32 | 28 | 291 | 49 |

## WACHUNGAJI MSTARI WA MBELE WA INJILI.

Wachungaji walio katika Huduma South Nyanza Conference

| Makundi | Ofisini | Mitaani | Taasisi | Wastaafu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Waliowekewa Mikono | 7 | 21 | 4 | 8 | 40 |
| Hawajawekewa Mikono | - | 57 | 4 | - | 61 |
| Jumla | 7 | 78 | 8 | 8 | 101 |

Timu hii ya wachungaji kazini, inaungana na wachungaji wastaafu wenye mikono ambao ni mbaraka mkubwa kwa kazi. Hawa wanashiriki katika kulisha siku za ibada, mikutano ya makambi, ubatizo, ndoa, mahubiri ya hadhara na huduma nyingine nyingi za kanisa na jamii.

## WACHUNGAJI NA WAKE ZA WACHUNGAJI WALIOLALA MAUTI 2016 – 2022.

Wachungaji waliolala mauti katika Bwana wakiwa kazini ni 2

i. Mch. Yusuph Mharagi na
ii. Mch. Bezarel Nzobano.

Wachungaji waliolala mauti wakiwa wamestaafu ni 10

i. Mch. Apollo Jeremiah. Konzi
ii. Mch. Ephraim Kilyunguma
iii. Mch. Charles Nkwabi
iv. Mch. Erasto Nzumbi
v. Mch. Phaustine Karuma
vi. Mch. Jeremiah Matulanya
vii. Mch.Arstariko Mkama
viii. Mch. Daudi Balula
ix. Mch. Mgaywa Lugembe
x. Mch. Mika Kamambi

Wake wa Wachungaji waliolala mauti

i. Mrs. Mugaywa Lugembe
ii. Mrs. Daudi Balula
iii. Mrs. Lameck Bulugu
iv. Mrs. Charles Nkwambi

**WACHUNGAJI WASTAAFU NA WAJANE WA FAMILIA ZA KICHUNGAJI.**

Wachungaji Wastaafu waliopo na wako kusaidia huduma za kichungaji.

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Mch. Isaack Maiga | - | Mwanza |
| ii. | Mch. Joseph Bulengela | - | Mwanza |
| iii. | Mch. Methusela Masuke | - | Bariadi |
| iv. | Mch. Erasto Mitanda | - | Maswa |
| v. | Mch. Fredy Kuleng'wa | - | Bariadi |
| vi. | Mch. Lameck Bulugu (Mgane) | - | Bariadi |
| vii. | Mch. Lucas Makondo | - | Kanadi |
| viii. | Mch. Yusuph Masunga | - | Maswa |
| ix. | Mch. Ibrahim Alex Juma | - | Mwanza |
| x. | Mch. Enock Maduhu | - | Mwagala |

Wake za wachungaji wajane waliopoteza wenzi wao.

i. Mrs. Eliada Chikubure – Igombe Mwanza.
ii. Mrs. Kilyunguma Happines Daudi Kisesa Mwanza.
iii. Mrs. Zakayo Mbuti Kusekwa – Nyakato Mwanza.
iv. Mrs. Haruni Shija Mashigani – Bupandagila Bariadi.
v. Mrs. Rebecca Lameck Ng'wala – Mwanhuzi Meatu.
vi. Mrs. Naomi Mkama Aristariko – Mahina Mwanza.
vii. Mrs. Phaustine Karuma – Nyegezi Mwanza.
viii. Mrs. Ellen Jeremiah Matulanya- Mkula Simiyu.
ix. Mrs. Erasto Nzumbi- Hungumalwa Misungwi.
x. Mrs. Dinah Yusuph Mharagi.
xi. Mrs. Jesca Bezareli Nzobano.
xii. Mrs. Juliana Mika Kamambi.
xiii. Mrs. Esther Nyamtara.
xiv. Mrs. Charity Tumaini Magembe.
xv. Mrs. Mary Kabinza.
xvi. Mrs. Suzana Bagumhe.
xvii. Mrs. Gumali.

**WACHUNGAJI WALIOWEKEWA MIKONO KWA MIAKA TOFAUTI TANGU 2016 HADI 2022.**

| Mahali | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2022 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kirumba | 2 | - | - | - | - | - | 2 |
| Nyahanga | - | 6 | - | - | - | - | 6 |
| Pasiansi | - | - | 4 | - | - | - | 4 |
| Geita | - | - | - | 4 | - | - | 4 |
| Singida | - | - | - | 3 | - | - | 4 |
| Bariadi | - | - | - | - | 5 | - | 5 |
| Nyegezi | - | - | - | - | - | 6 | 6 |
| Jumla | 2 | 6 | 4 | 7 | 5 | 6 | 30 |



*Picha 9: Huduma ya kuwawekea mikono wachungaji katika kanisa la Pasiansi.*

**WACHUNGAJI WALIOAJIRIWA KATIKA HUDUMA YA KICHUNGAJI 2020 HADI 2022.**

| Mwaka | 2020 | 2021 | 2022 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Jumla Wachungaji | 5 | 7 | 11 | 23 |

**WACHUNGAJI WALIOPO MASOMONI NA WALIO NJE YA UTUMISHI.**

- Wachungaji masomoni ni 19, wanaosoma wakiwa kazini ni 18, mmoja anasoma akiwa katika likizo ya bila malipo.
- Mchungaji mmoja, Silver Damas yuko nje ya utumishi wa kichungaji (leave of absence).

**Jedwali la Watumishi SNC na kiwango cha Elimu zao.**

| Makundi | Std 7 | Sec | Cheti | Stashahada | Shahada ya Juu | Shahada ya I | Shahada ya II | Shahada ya III | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wachungaji | 2 | 12 | 9 | 4 | 1 | 57 | 8 | - | 93 |
| Wahasibu | - | - | - | - | 2 | 4 | 2 | - | 9 |
| Madakitari | - | - | - | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Walimu | - | - | - | - | - | | 1 | - | 1 |
| K. Wahitasi | - | - | - | 4 | - | 3 | - | - | 7 |
| Teknohama | - | - | - | - | - | 1 | - | - | 1 |
| APD | 2 | 1 | - | - | - | | - | - | 3 |
| Dereva | - | - | 1 | - | - | | - | - | 1 |
| M. Miliki | - | - | - | - | 1 | | - | - | 1 |
| M. Miradi | - | - | - | - | - | | 1 | - | 1 |
| Mazingira | 3 | - | - | - | - | | - | - | 3 |
| Walinzi | 5 | - | - | - | - | | - | - | 5 |
| Jumla | 12 | 13 | 10 | 8 | 4 | 66 | 12 | - | 126 |

## KUANDAA WATUMISHI NA MITAA TAZAMIWA.

Ofisi ya South Nyanza Conference imeendelea kutoa nafasi ya pekee kwa wachungaji, wahasibu, walimu na Teknohama, Makatibu wahitasi na watu wa mazingira kutoka vyuo mbalimbali ili kufanya mazoezi ya kile walichojifunza Vyuoni. Tendo hili limekuwa mbaraka mkubwa kwa watumishi waliokubali kufanya kazi na timu hizi. Tunayo mitaa tazamiwa yenye Wachungaji wanaojitolea katika mitaa hiyo 29.

South Nyanza Conference imekuwa miongoni mwa maeneo ambayo yamepokea wachungaji kwa ajili ya mazoezi kutoka chuo kikuu cha Arusha na Bugema. Lakini pia tumepata wanachuo wa fani ya mazingira kutoka VETA na pia vyuo vya Dodoma, SAUT, Chuo cha Mipango, Bugando na Vyuo mbalimbali vya Elimu, Teknohama, Uhasibu nk.




*Picha 10: Mwanafunzi wa fani ya Tehama kutoka Chuo Kikuu cha UDOM akiwa katika mazoezi (Field Training) katika ofisi za SNC.*

## MALEZI NA MATUNZO YA WASHIRIKI

Moja ya sifa nzuri tulizonazo kama South Nyanza Conference ni bidii yetu katika kufanya uinjilisti na kubatiza watu wengi.

### YALIYOFANYWA KUTEKELEZA MKAKATI WA KULEA NA KUTUNZA WASHIRIKI.

1. Kupunguza ukubwa wa mitaa kwa kuikata ili kusogeza huduma kwa washiriki, tumeongeza mitaa mipya 24
2. Kufanya uchambuzi yakinifu wa washiriki kwa kila Kanisa ili kujua idadi halisi ya washiriki wa Kanisa.
3. Tumetoa Semina za kutosha za namna ya kuratibu washiriki kwa makarani wa makanisa yote.
4. Tumetoa Semina za malezi na matunzo ya washiriki kwa mitaa yote ndani ya Conference.



*Picha 11: Katibu wa Union ya NTUC Pr David Makoye Pamoja na Katubu wa SNC Pr Nicodemo Ntabindi katika moja ya semina.*

.

## KUINGIZA MAJINA YA WASHIRIKI KATIKA MFUMO WA ACMS (ADVENTIST CHURCH MANAGEMENT SYSTEM).

Tumefanikiwa kuendesha Semina mbalimbali za kuingiza washiriki katika mfumo wa ACMS.

| Mwaka | Washiriki | ACMS | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Dec 2020 | 138,489 | 148,706 | 107% |
| Nov 2021 | 149,576 | 150,256 | 100.4% |
| April 2022 | 154,460 | 156,837 | 101.5% |
| June 2022 | 163,979 | 157,001 | 95.7% |




*Kielelezo 5: Ulinganifu wa idadi ya washiriki na wale walioingizwa katika mfumo wa ACMS katika kipindi cha miaka 3.*

Robo hii ya pili kupitia mahubiri ya mlipuko katika Conference tulipokuwa na vituo 400 kabla ya Karatu NET Event, na mikutano ya Makambi inayoendelea, pamoja na Karatu Net Event watu wengi wamebatizwa, hivyo tunahimiza jitihada za ziada kuingiza majina makanisani ziongezeke na kwamba vifaa kama Computer vipewe kipaumbele katika Makanisa, ili uingizaji wa majina uwe rahisi kwa kila Kanisa.




*Picha 12: Viongozi wakiwa katika semina ya ACMS iliyofanyika Singida.*

## KUSIMAMIA SUALA LA KUBADILI TASWIRA (IMAGE CHANGE)

Kubadili taswira (Image change) imekuwa ni mojawapo ya mambo yaliyokuwa katika misukumo ya kipindi hiki cha miaka mitano kutoka ngazi ya General Conference. Lengo hasa likiwa ni kubadili mitazamo ya mshiriki mmoja mmoja na Kanisa kwa ujumla katika masuala yahusuyo miundombinu. Majengo yetu na miundombinu yote ya Kanisa kwa ujumla iliyoboreshwa vizuri yanaweza kutumika kama vyombo vya uinjilisti pale yanapoonekana kukidhi matarajio ya watu wa kizazi hiki kinachobadilika kwa kasi kubwa. Hii inakuwa tofauti na dhana ya kipindi kilichopita wakati majengo mengi ya makanisa yalipoonekana kuwa duni sana, washiriki wakidai kuwa duniani si mahali petu pa kudumu, tunasafiri, kitambo kidogo tutakuwa Mbinguni.

Katika kutekeleza jukumu hili tumetoa Semina kwa wachungaji na wazee wa Kanisa tukisisitiza umuhimu wa kujenga majengo mazuri ya Kanisa yanayomwakilisha vizuri Mungu pamoja na Kanisa lake katika jamii hii. Tumetiwa moyo sana na mwitikio mkubwa uliopo katika kulitekeleza suala hili.

Kuna mwamko mkubwa sana katika makanisa. Mengi yamehamasika na yameamua kuacha majengo ya zamani yaliyochoka na kuanzisha majengo mapya yenye hadhi, na makanisa mengine mengi yana mpango huo pia.

Sambamba na ujenzi wa makanisa kuna mwitikio mwingine mkubwa wa kujenga nyumba za wachungaji ili kukuza heshima ya watumishi hawa na kupunguza gharama kubwa ya kupanga nyumba. Mitaa mingi imehamasika.

| Wanazoishi Wachungaji | Nyingine inafaa | Boma limekamilika | Boma Linajengwa | Msingi Umekamilika | Wananunua nyumba | Uwanja | Hawana uwanja |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 31 | 7 | 10 | 5 | 3 | 2 | 11 | 4 |



*Picha 13: Baadhi ya maeneo ambayo yamefanyiwa mabadiliko ya taswira ikijumuisha makanisa, nyumba za wachungaji, vibweta, vivuli vya makambi n.k*

## KUANDAA NA KUPELEKA TAARIFA.

Tumepokea taarifa kutoka makanisani kupitia mitaa, kuziandaa na kuzipeleka Union taarifa zote zinazohitajika kwa wakati ikiwa ni pamoja na taarifa ya washiriki ya kila robo (Quarterly Statistical reports) na za kila mwaka (Annually Statistical reports).

## UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA KAZI KWA KIPINDI CHA 2016-2020.

- Tumetimiza njozi ya kugawa Conference hii ili kusogeza huduma kwa washiriki.
- Tunaendelea na ujenzi wa Ofisi mpya ya Conference ya kisasa na yenye hadhi inayokidhi viwango vya kubadili taswira (image change).
- Tunaendelea kuboresha utumishi kwa kufanya yafuatayo: -
  - Wachungaji wengi walioajiriwa bila elimu ya Theolojia wameenda chuoni wengine wanaendelea na masomo yao, waliomaliza masomo yao ni: -
    Edson Lugwisha, Philipo George, Emmanuel Mpina, Elton Mvanga, Kalangi Mtobesya, Joel Chacha, Gamali Budo, Theonest Mwanangwa, Baraka Nchama, Lungama Jigulu, Marko Phabian.
  - Baadhi ya wachungaji wamepatiwa vyombo vya usafiri (gari/pikipiki).
- Mitaa Mingi imeongezeka Pamoja na makanisa.
- Washiriki wameongezeka kama takwimu zinavoonekana.
- Tumependekeza njia rahisi ya kutunza washiriki na kumtafuta mshiriki aliyepotea.
- Tumeshiriki matukio makubwa ya kiutume ya kanisa kitaifa kwa mahubiri yaliyorushwa CCM Kirumba, Effort ATAPE Mabatini, na mengine yaliyofanyika nje ya SNC.
- Tumeendesha Semina uongozi na Malezi katika jiji la Mwanza na katika mji wa Bariadi.

.




*Picha 14: Mchungaji akikabidhiwa chombo cha usafiri aina ya pikipiki.*

## CHANGAMOTO.

1. Bado kuna mitaa mingi inayohitaji kukatwa ili kusogeza huduma za kichungaji kwa washiriki.
2. Mabadiliko ya mara kwa mara ya makarani wa Kanisa inapekelea shughuli ya uratibu wa majina ya washiriki kutofanikiwa kwa uzuri.
3. Uhamaji wa washiriki unaosababishwa na utafutaji wa maisha (kilimo, ufugaji, biashara n.k) unatufanya tupoteze washiriki.
4. Batizo zinazolenga kupata idadi kubwa ya wabatizwa na si washiriki wanaodumu kanisani (quantitative vs qualitative church growth) ni changamoto pia.
5. Kutopitia orodha ya majina ya washiriki katika kitabu cha ushirika mara kwa mara husababisha upotevu wa washiriki usioweza kutambulika.
6. Jengo dogo la ofisi lishilotosheleza huduma zote za kiofisi, wahudumu na wahudumiwa.
7. Kuwa na vijiji na vitongoji visivyo kuwa na makundi au makanisa.

## MIPANGO YA KAZI KWA KIPINDI CHA 2022-2025.

1. Kugawa mitaa mipya na kupunguza ukubwa wa mitaa.
2. Kuhimiza kila Kanisa ndani ya Conference linatumia mfumo mpya wa kiteknolojia wa kutunza kumbukumbu za Kanisa (Adventist Church Management System).
    a. Kuhamasisha kila Kanisa kununua ngamizi mpakato (laptop) ili kuwezesha makanisa yote kuingia katika mfumo mpya wa utunzaji wa kumbukumbu za Kanisa (Adventist Church Management System).
    b. Kuunda timu ya wataalamu watakaotoa elimu ya ujuzi wa kutumia ngamizi (computer) kwa makarani.
    c. Kuendelea kutoa semina juu ya malezi na matunzo ya washiriki kwa makanisa yote.
3. Kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya konferensi.
4. Kuongeza idadi ya watumishi ili kupanua huduma kwa washiriki.
5. Kuhimiza Ubora wa huduma katika taasisi zote na kuongeza ubora wa matokeo.
6. Kudumisha zoezi la kubadili taswira katika taasisi zote za kanisa.
7. Kufungua kundi au kanisa katika kila Kijiji au kitongoji kwa kadri Mungu atakavyosaidia.

## SHUKRANI.

Napenda kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kufikia hapa tulipofika, niushukuru uongozi wa union kwa ushiriki wao kwa kipindi hiki kinachomalizika, Jina lake na litukuzwe.

Binafsi nina kila sababu ya kuwashukuru viongozi tuliopokea kutoka kwao huduma hii ya kiutumishi katika ofisi hii. Kama nilivyokabidhiwa kijiti hiki, ndivyo mikono yangu ilivyofunguliwa kumkabidhi kijiti hiki yule ambaye Bwana amekwisha kumtenga na kumchagua kwa ajili ya huduma hii na ofisi hii.

Ninawashukuru wajumbe wote wa Kamati Kuu ya Conference, wakurugenzi wa Idara zote katika Conference, watumishi wote wa ofisi ya Conference, Wakuu wa Taasisi zetu zote na Wachungaji wa mitaa kwa kila walichofanya kuhakikisha shughuli za Conference hii kwa kipindi hiki zinatekelezwa. Ninawashukuru viongozi wa makanisa mahalia, Makatibu wenzangu wa makanisa mahalia, wakuu wa Idara makanisani pamoja na waumini wote wa Conference hii kwa ushirikiano mkubwa mlioudhihirisha katika kutumika kwa pamoja katika kazi ya Mungu.

Aidha niseme asanteni kwa mikono yenu iliyobeba Injii hii na utumishi huu wa Yesu Kristo kwa muhula wote huu unaomalizika hadi tunapoingia tena katika muhula mwingine wa kazi ya Bwana.

Asanteni kwa kuisikiliza kazi mliyoifanya, nasi tukaipokea na kuijumlisha na kuisoma kwenu.

Asanteni kwa kunisikiliza, Nami nawasilisha.
ASANTENI NA BWANA AINULIWE, AMINA.

# TAARIFA YA OFISI YA HAZINA



**ELDER. MWITA MACHAGE.**

**MHAZINI MKUU**

SNC

## SHUKURANI.

Tunamshukuru Mungu wetu kwa kutufikisha katika mkutano mkuu wa nane (8) wa South Nyanza Conference Jina Lake lihimidiwe sana. Katika kipindi cha miaka Saba (7) tumeuona mkono wake katika ukuaji wa kazi katika Nyanja mbalimbali.

Shukrani ziwaendee Washiriki wote wa Konferensi hii kwa kuitegemeza kazi ya Bwana kwa nguvu zenu na mali zenu. Uaminifu wenu unathibitika siku hata siku na siku si nyingi mwenye kazi ATAWAKARIBISHA KATIKA MAKAO YA MILELE KUTOKANA NA UAMINIFU WENU KWA MACHACHE MLIYOPEWA ULIMWENGUNI.

Ningependa kutambua kazi kubwa inayofanywa na wachungaji wetu wa mitaa. Pamoja na wengi wao kuwa na maeneo makubwa ya kazi lakini wamefanikiwa sana katika kutekeleza majukumu yao katika mitaa waliyopewa. MUNGU AWABARIKI SANA.

Tunapenda kuwashukuru kwa namna ya pekee waweka hazina wote wa makanisa mahalia , waweka hazina wasaidizi, na mashemasi ambao wanajitolea muda wao kila wiki kukusanya zaka na sadaka na kusimamia fedha na rasilimali za makanisa. Ripoti hii inatokana na juhudi ya kazi ya watu hawa wote.

Mwisho ningependa kuwashukuru watumishi wenzangu katika ofisi ya jimbo wakiongozwa na maofisa wenzangu tunaoshirikiana kuliongoza jimbo Mungu awabariki sana. Wahasibu wetu wamekuwa msaada mkubwa kufanikisha utolewaji wa taarifa hii Mungu awabariki sana.

## UKUAJI WA KONFERENSI

Katika kipindi cha miaka Saba (7) baada ya mkutano mkuu wa mwaka 2015, Konferensi imefanikiwa kukua kwa ongezeko la waumini na washiriki toka 144,111 Hadi 248,876 Ukuaji huu ulipelekea kugawanywa kwa eneo la Konferensi na kuundwa NYANZA GOLD BELT FIELD ambapo hadi sasa konferensi yetu ina washiriki 163,979. Kwa kadri kanisa linavyoongezeka ndivyo mapato huongezeka. Ukuaji huu hulipatia jimbo uwezo wa kifedha na uwezo wa kuiwezesha kazi ya Mungu (Angalia kielelezo cha mapato ya jimbo hapo chini)

## TUNU YA KONFERENSI

Kila wiki maelfu ya Waadventista Wasabato katika Conference yetu huungana katika kumwabudu Muumba wao. Wanaishi maeneo tofauti, tamaduni tofauti, na ibada kwa mitindo tofauti. Lakini jambo moja linabaki vile vile: wamejitolea kueneza Injili ya Kristo duniani kote. Wanatoa wakati wao, nguvu zao, na fedha zao ili Kuwaambia watu wengine kuhusu neema ya kuokoa ya Yesu. Waadventista hufanya kazi pamoja kwa kuunganisha rasilimali zake kueneza Injili ulimwenguni kote.

## WITO NA UTUME WETU

Tunaposoma Mathayo 24:14 mara nyingi tunaweka mkazo kwenye sehemu ya mwisho: “*...na ndipo ule mwisho utakapokuja.*” Hii ni ahadi kubwa, na ndilo tumaini letu. Lakini kuna ahadi nyingine ya muhimu: “*habari njema ya Ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote*.” Ni ahadi iliyoje! Agizo la Injili katika Mathayo 28 linasema: “*Basi, enendeni, mkawafundishe mataifa yote; ...*” Ni changamoto kubwa kwetu Ni kazi kubwa! Lakini ni ahadi ya hakika kwamba “*Injili hii ya Ufalme itahubriwa katika ulimwengu wote*”

Ni ahadi inayofanana na ile aliyopewa Yoshua wakati Bwana aliposema: "*Kila mahali mtakapokanyaga kwa nyayo za miguu yenu, nitawapawapa, kama nilivyomuahidi Musa*" (Yos. 1:3).

Kwa Zaidi ya miaka 100 tumekuwa tukipeleka Ujumbe wa Malaika wa Tatu Katika sehemu nyingi za konferensi yetu. Kumekuwa na ushindi mkubwa; lakini "imesalia ardhi nyingi sana kumilikiwa." Sehemu kubwa bado haijafikiwa. Ni wakati wa sisi kusema, kama Kalebu alivyofanya baada ya kuvuka Yordani, "Nipe mlima huu." Ni "*si kwa nguvu, wala si kwa uwezo, bali kwa roho yangu, asema BWANA wa majeshi*" (Zak. 4:6).

## UHAKIKA WA UWEPO WA MUNGU KATIKA UTUME

Ulimwengu umepitia changamoto mbalimbali katika miaka saba ikiwemo majanga mbalimbali, Magonjwa kama UVIKO 19, mdororo wa kiuchumi na mengine mengi lakini tunapotazama katika ongezeko la zaka na sadaka wakati wa kipindi hiki kigumu, tunamsifu Bwana kwa uaminifu wake kwa watu wake na baraka zake nyingi. Mungu ametupatia uhakika wa kuwa pamoja nasi hata ukamilifu wa dahari (Math 28:20).

## MALI ZA KONFERENSI

Konferensi ina mali za kuhamishika na zisizohamishika na mchanganuo wake ni kama zinavyoonekana hapa chini

| ARDHI, MAJENGO NA VIFAA KWA MWAKA 2016 - 2020 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MUHTASARI WA MABADILIKO | HESABU YA MWANZO | ONGEZEKO | PUNGUZO | HESABU YA MWISHO |
| ARDHI | 176,507,422.00 | 192,893,498.00 | 202,004,298.00 | 167,396,622.00 |
| KUENDELEZA ARDHI | 10,018,500.00 | 30,885,300.00 | 12,253,000.00 | 28,650,800.00 |
| MAJENGO | 156,798,364.08 | 23,395,294.10 | 6,865,000.00 | 173,328,658.18 |
| MAKAZI | 449,729,680.70 | 213,033,200.00 | 134,634,452.13 | 528,128,428.57 |
| VIFAA | 97,292,080.22 | 134,883,100.00 | 42,515,300.00 | 189,659,880.22 |
| MAGARI | 29,000,000.00 | 52,000,000.00 | 52,000,000.00 | 29,000,000.00 |
| MILKI ZA KANISA NA SHULE | 3,526,170,101.48 | - | 908.889,427.20 | 2,617,280,674.28 |
| KAZI KATIKA UTEKELEZAJI | 54,452,605.00 | 171,692,885.00 | 156,189,352.81 | 69,956,137.19 |
| **JUMLA** | **4,499,968,753.48** | **818,783,277.10** | **1,515,350,830.14** | **3,803,401,200.44** |

Mali hizi hupatikana kwa sadaka zinazotolewa na washirki ikiwa ni moja ya chanzo cha mapato ya kanisa kama inavyoainishwa katika kipengele kinachofuata.

## VYANZO VIKUU VYA MAPATO YA KONFERENSI

ECD working policy (V14, V25) inataja vyanzo vya mapato kuwa zaka na sadaka ambapo zaka hutumika kuwahudumia wachungaji na watumishi wa kanisa ili kuwawezesha kuendelea na kazi waliyopewa na Bwana, na sadaka hutumika kueneza utume ulimwenguni kwa miradi mbalimbali ya utume pamoja na maendeleo ya konferensi. Ili Konferensi ijiendeshe kwa mujibu wa Biblia na sera za kanisa, uaminifu katika matoleo unahitajika.

“Leteni zaka kamili ghalani ili kiwemo chakula katika nyumba yangu mkanijaribu kwa njia hiyo asema BWANA wa majeshi, mjue kama sitawafungulia madirisha ya Mbinguni na kuwamwagieni Baraka hata isiwepo nafasi ya kutosha au la.” Malaki 3:10.

Hili ni fungu maarufu sana katika Biblia, tunapokuwa tunazungumzia juu ya zaka na sadaka. ujumbe wake bado ni wa muhimu sana leo kama ilivyokuwa zamani. Mungu anatuhitaji kila mmoja wetu kurudisha zaka na sadaka kwa uaminifu na tunapofanya hivyo amesema atatubariki sana. Hivyo kama viongozi na washiriki wote kwa pamoja tunapaswa kuwa kielelezo katika utoaji wa zaka na sadaka kwa uaminifu.

## MWENENDO WA MATOLEO YA ZAKA NA SADAKA KWA KIPINDI CHA MIAKA SITA KUANZIA MWAKA 2016 HADI 2021.

| MWAKA | ZAKA (TZS) | SADAKA(TZS) |
|---|---|---|
| 2016 | 2,034,190,514.35 | 545,330,603.99 |
| 2017 | 2,239,045,912.13 | 570,521,973.47 |
| 2018 | 2,961,013,313.68 | 604,886,510.26 |
| 2019 | 3,323,741,464.31 | 739,121,646.43 |
| 2020 | 2,494,103,441.57 | 511,246,632.06 |
| 2021 | 2,610,653,915.00 | 531,249,438.00 |

Tunamshukuru Mungu kwa kupanda kwa matoleo mwaka hadi mwaka jina lake lisifiwe. Katika mwaka 2020 kumeonekana kushuka kidogo kwa matoleo hii ni kwasababu zifuatazo;

- **Utengwaji wa NGBF.**

Baada ya NGBF kutengwa mwaka 2019 tuliendelea kutunza vitabu vya fedha pamoja hadi pale walipopewa hadhi ya Field kamili mwezi wa pili 2020

- **COVID 19.**

Washiriki wetu walikua wahanga wa gonjwa la Corona lakini bado katika hayo yote waliendelea kuwa waaminifu kwa Bwana kwa kile walichopata.

## ULINGANIFU WA MATOLEO YA ZAKA NA SADAKA.

Pamoja na matoleo ya zaka na sadaka kupanda kadri miaka iendavyo bado matoleo ya sadaka yako chini ukilinginisha na zaka. Nipende kuwatia moyo kumtolea Mungu kwa mpango (Systematic Benevolence) naye ataendelea kutubariki kama ilivyo ahadi yake "HATA ISIWEPO NAFASI YA KUTOSHA" Ahadi iliyoje!




*Kielelezo 1: Ulinganifu wa matoleo ya zaka na sadaka katika kipindi cha 2016 - 2022.*

## UAMINIFU WETU KATIKA VIPIMO.

Konferensi yetu ina washiriki 163,979 lakini idadi ya waaminifu ni 65,591 ambayo ni 40%.




*Kielelezo 2: Mchanganuo wa matumizi ya zaka.*




*Kielelezo 3: Mchanganuo matumizi ya sadaka.*

## GHARAMA ZA UENDESHAJI WA KONFERENSI.

Kama taasisi kuna gharama nyingi kwa ajili ya uendeshaji wa kazi ya Mungu. Kwa kadri kazi ya Bwana wetu inavyozidi kukua pia gharama zinakua na kuongezeka. Mitaa mipya inafunguliwa, Watumishi wanaongezeka na fursa mpya kwa ajili ya utume hujitokeza. Jedwali hapa chini huonyesha matumizi ya jimbo katika kipindi cha miaka yote ya taarifa hii.

| MWAKA | MATUMIZI |
|---|---|
| 2016 | 2,477,603,206.11 |
| 2017 | 2,963,500,906.00 |
| 2018 | 4,409,994,607.58 |
| 2019 | 4,340,662,361.54 |
| 2020 | 3,331,192,175.49 |
| 2021 | 3,024,956,933.46 |




*Kielelezo 4: Gharama za uendeshaji wa konferensi kwa kipindi cha miaka 6.*

## SADAKA YA KAMBI.

| SADAKA YA KAMBI 2016 - 2021 | |
|---|---|
| MWAKA | MATOLEO |
| 2016 | 183,210,371,04 |
| 2017 | 196,493,191,40 |
| 2018 | 284,787,527.33 |
| 2019 | 198,968,672.00 |
| 2020 | 270,629,567.65 |
| 2021 | 321,308,598.01 |

Jedwali hapo juu linaonesha makusanyo ya sadaka ya kambi kwa miaka tajwa na yafuatayo ni matumizi yake kutokana na sera

1. Uinjilisti 25%
2. Ujenzi wa nyumba za Wachungaji 25%
3. Ujenzi wa makanisa 25%
4. Union 25%

## UJENZI WA HOSPITALI YA PASIANSI.

Tunamshukuru Mungu mradi huu mkubwa umefikia hatua ya matumizi. Asilimia kubwa ya michango ya ujenzi imekuwa michango ya washiriki na wadau wa kazi ya Mungu ndani na nje ya jimbo letu. Michango inachanganuliwa kama ifuatavyo:-

| MWAKA | MICHANGO |
|---|---|
| 2016 | 134,679,725.39 |
| 2017 | 361,846,731.24 |
| 2018 | 79,587,717.00 |
| 2019 | 233,272,783.81 |
| 2020 | 70,366,224.96 |
| 2021 | 13,846,850.36 |
| **JUMLA** | **893,600,032.76** |

Taasisi zetu zina lengo la kueneza injili kupitia huduma zinazotoa. Tunawashukuru washiriki kwa kuwa wadau wakubwa wa maendeleo ya kanisa katika kujenga taasisi na kuziendeleza. Huu ni wajibu wetu washiriki.



*Picha 1: Jengo la Hospitali ya Pasiansi SDA.*

## UTUME ULIMWENGUNI (GLOBAL MISSION).

General Conference Kushirikiana na Jimbo letu imekuwa na miradi yautume katika mazingira yasiyofikiwa bado na kwa miradi hii jimbo limefanikiwa kuwa na mitaa mipya baada ya miradi hiyo kukamilika. Mitaa hiyo ni PAJI na MWANJOLOO. Fedha iliyotumika ikiwa ni pamoja na maeneo ya NGBF kabla ya kutengwa ni 17,842,826.92 Tzs. Mradi unaoendelea sasa ni wa KAYENZE. Kwa Neema ya Mungu tunategemea kufikia maeneo mengi Zaidi kwa msaada wa mradi huu.

Vilevile mradi umewezesha upatikanaji wa Pikipiki (15) Kumi na tano kwa wachungaji wa Mitaa.



*Picha 2: Moja kati ya pikipiki 15 zilizotolewa kama sehemu ya mradi wa Global Mission.*

## UJENZI WA NYUMBA ZA WACHUNGAJI MITAANI.

Kwa neema ya Bwana jimbo kwa kushirikiana na washiriki katika mitaa yao tumefanikiwa kuwezesha ujenzi na matengenezo ya makubwa kwa nyumba za wachungaji katika mitaa ifuatayo: -

| | | |
|---|---|---|
| BUHUNGUKILA | IGELEGELE | IPILILO |
| NGASAMO | NKOLOLO | NGULYATI |
| KIDINDA | NTUZU | KWIMBA |
| NYALIKUNGU | LAINI | NYAKATO |
| MAGU | NYAMBITI | MAHEMBE |
| NYASAKA | MASANZAKONA | NYEGEZI |
| MEATU | PAJI | OLD MASWA |
| SALAWE | MSHIKAMANO | MKULA |
| MWAGALA | NANGALE | NDAGALU |
| WILAYANI | SHAMALIWA | SIMA |

*Kielelezo 5: Mitaa 30 ambayo jimbo limehusika katika ujenzi au matengenezo ya nyumba za wachungaji.*

Tunawashukuru washiriki kwa kuweka nguvu nyingi katika ujenzi wa nyumba hizi kwa kujitolea kwa hali na mali. Mungu awabariki sana.

Kwa ujumla nyumba zipo 30 na tamanio letu ni kila mtaa uwe na nyumba ya mchungaji ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuwezesha Zaidi shughuli za utume wa kanisa katika jimbo letu.

## RUZUKU KWA TAASISI ZA KANISA.

Katika kipindi cha miaka mitano Jimbo limetoa ruzuku kwa taasisi zake na pia kutoa fedha ya uanzushwaji jimbo la NGBF kama inavyoonekana hapo chini.

| MWAKA | RUZUKU YA ZAKA | RUZUKU ISIYO ZAKA | RUZUKU YA KUSIMIKA NGBF |
|---|---|---|---|
| 2016 | 20,000,000.00 | 41,019,450.00 | - |
| 2017 | - | 76,265,700.00 | - |
| 2018 | 44,878,000.00 | 36,631,500.00 | - |
| 2019 | 73,295,000.00 | 14,965,000.00 | - |
| 2020 | - | - | 67,727,509.59 |
| **JUMLA** | **138,173,000.00** | **168,881,650.00** | **67,727,509.59** |

## MRADI WA UJENZI WA OFISI.

Tunamshukuru Mungu hatimaye ujenzi wa ofisi ya konferensi umeanza kule Mwananchi, Buzuruga. Tarehe 22/05/2022 tulikua na uzinduzi wa ujenzi ulioambatana na kukusanya fedha za kusaidia ujenzi. Kwa neema ya Mungu tulipata fedha taslimu 50,741,450 Vifaa vyenye thamani ya 6,064,500 na ahadi ya 60,201,000 jumla ni 117,006,950.

Konferensi imefanikiwa kununua mashine ya kuchakata kokoto ili kupunguza gharama za ujenzi ambayo hadi sasa inafanya kazi.

Hadi sasa vibali vyote vimepatikana na kazi imeanza. Tunawashukuru washiriki na taasisi zote kwa kuunga mkono mradi huu na tunaendelea kuwaomba kuunga mkono kwa hali na mali kwa kadri ya mibaraka mliyopewa.

## IDARA YA FEDHA NA UTUME.

Kama idara tumekuwa tukiungana na wahasibu wenzetu wa Union nzima kufanya mahubiri kila mwaka na kujenga kanisa baada ya mahubiri hayo. Hadi sasa tumefanya mahubiri manne na kujenga makanisa manne.

## MALENGO YETU KAMA IDARA YA FEDHA.

Malengo yetu ni kama ifuatavyo

- Kushiriki mikutano mbalimbali ya injili sehemu mbalimbali katika Conference yetu.
- Kuwaendeleza watendakazi kimasomo katika fani mbalimbali kadri bajeti itakavyo ruhusu.
- Kuendeleza Ujenzi wa ofisi za Jimbo.
- Kushirikiana pamoja na makanisa mahalia kujenga nyumba za wachungaji katika kila Mtaa ili kupunguza changamoto kubwa inayotukabili ya kulipa kodi za nyumba ambazo hupanda mara kwa mara.
- Kununua vifaa vya usafiri ili kurahisisha wachungaji kuyafikia makanisa kwa urahisi hasa tukizingatia kuwa mitaa inayo makanisa mengi.
- Kununua vitendea kazi kama vile ngamizi (computer) ambazo zitawasaidia wachungaji katika kutoa taarifa hasa tukizingatia mabadiliko yanayotokea mara kwa mara katika teknolojia.
- Kuendelea kutoa semina mbalimbali katika Conference yetu. Ikiwa ni pamoja na matumizi ya mfumo wa matoleo ya zaka na sadaka Church Financial Management Sysytem (CFMS).
- Kununua ardhi kwa ajili ya matumizi ya baadaye.
- Kuendeleza miradi ya jimbo

## MAFANIKIO YALIYOFIKIWA KWA NEEMA YA MUNGU.

- Tumefanikiwa kuwasomesha watumishi 35 ikiwa ni wachungaji na wafanyakazi wa kada zingine.
- Tumefanikiwa kupata umiliki wa Viwanja vya Misungwi Ekari 3.5, Magu Ekari 2.5 na Bugarika (High Density).
- Tumefanikiwa kulipa mishahara kwa wakati kulingana na bajeti.
- Tumefanikiwa kuanza mradi wa Alizeti kwenye eneo letu la Mwalogwabagole.
- Tumefanikiwa kuanza ujenzi wa ofisi za Jimbo letu.
- Tumefanikiwa kuwakopesha wafanyakazi vyombo vya usafiri yaani magari pamoja na pikipiki.
- Tumefanikiwa kufanya ukaguzi wa makanisa.

## CHURCH FINANCIAL MANAGEMENT SYSTEM (CFMS)

Kanisa katika Divisheni yetu limeanzisha mfumo wa kukusanya na kuchakata matoleo yaani zaka na sadaka. Sisi kama konferensi tumeanza kuutumia kama maagizo yalivyo. Japo bado tunaendelea na elimu kwa washiriki tunawashukuru kwa kuutumia mfumo na ifuatayo ni taarifa ya matumizi yake.

- Washiriki waliojiandikisha kwenye mfumo ni 7,674 ambayo ni 4.68% ya washiriki wa konferensi yote.
- Mitaa inayotumia mfumo ni 75 kati ya 78.
- Kiasi kilichotolewa kupitia mfumo ni 414,169,997

## KUJIANDAA NA MATUKIO YAJAYO

Janga la COVID-19 ni ishara tu ya yale ambayo bado yanakuja. Fursa kuchunguza njia mpya za kufikiri na kutumia njia mpya za kufanya utume zinapatikana tukichukua muda na kutafuta kwa maombi. Kanisa na tasisi zake zinahitaji kujenga uvumilivu unaohitajika kukabiliana na hali mbaya ya kiuchumi ambayo inaweza kutishia rasilimali zinazohitajika kwa utume hivyo tunatakiwa kufikiri mbele pamoja na Mungu.

Bei za Chakula na nishati kwa aina zake zinazidi kupanda. Hali ya maisha kwa ujumla inabadilika na mfumuko wa bei uko juu. Inatubidi kutumia rasilimalizetu kwa akili aliyotupatia Mungu ili kazi yake isikwame, Lakini katika yote tunajua tunaukaribia ule mwisho kama mtumishi wa Mungu Ellen G White anavyoandika.

“Maafa ya nchi kavu na baharini, hali isiyotulia ya jamii, kengele za vita, ni za kushangaza. Vinanatabiri matukio yanayokaribia ya ukubwa wa kushangaza. Mashirika ya uovu yanaunganisha nguvu zao pamoja. Wanajiimarisha kwa janga kubwa wa mwisho. Mabadiliko makubwa yatatokea hivi karibuni katika ulimwengu wetu, na harakati za mwisho zitakuwa za haraka.” (White 1909) Mashauri juu ya kanisa, Gombo la 9 (Tafsiri isiyo rasmi)

Sote tungeifanya kazi ya Mungu kuwa uwekezaji wetu mkuu. Tutumie rasilimali zetu kufanikisha kazi yake kabla mali zetu hazijakosa thamani na kutupwa mitaani kama takataka.

## MWISHO.

Bado kuna mambo mengi ya kufanya, baada ya Mungu kumuahidi Joshua kuwa kila mahali zitakapokanyaga nyayo za miguu yenu nimewapa ninyi kama nilivyo mwapia Musa, bado mahubiri mbalimbali yanatakiwa kufanyika ili watu wake waweze kujitoa kwake. Katika nyakati hizi zenye kazi nyingi ziliyo mbele yetu, ni lazima tujifunze kumtegemea Mungu kikamilifu. Wakati fulani tunasahau kuwa hii ni kazi yake Mungu. Lazima tukubali kufuata maelekezo yake, ili kuweza kukamilisha kazi hii tuliyoachiwa kuifanya. Malengo yetu ya kuifanya kazi yake tuyakabidhi mikononi mwake naye atayafanikisha.

SOUTH NYANZA CONFERENCE OF SDA

# STATEMENT OF FINANCIAL POSITION

## AS OF DECEMBER 31, 2021 FROM 2016

| | 2021 | 2020 | 2019 | 2018 | 2017 | 2016 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | | | | |
| Cash and Cash Equivelents | 139,474,727.33 | 556,117.71 | 49,105,516.35 | 207,022,821.04 | 447,020,268.42 | 764,464,096.87 |
| Accounts Receivable- Net | 865,538,718.92 | 762,670,222.02 | 830,664,756.88 | 689,423,011.84 | 598,205,841.99 | 483,090,927.18 |
| Cash Held for Agency | 57,618,803.96 | 205,814,535.00 | 245,049,009.13 | 124,854,586.86 | 173,823,042.50 | - |
| Notes/Loans Receivable | 25,481,103.22 | 25,481,103.22 | 50,992,840.12 | 46,005,500.00 | 30,910,166.73 | 19,278,193.92 |
| Inventory and Prepaid Expenses | 114,662,835.78 | 63,465,131.33 | 115,307,727.71 | 125,549,959.44 | 114,565,597.57 | 76,398,694.89 |
| **Total Current Assets** | **1,202,776,189.21** | **1,057,987,109.28** | **1,291,119,850.19** | **1,192,855,879.18** | **1,364,524,917.21** | **1,343,231,912.86** |
| For Use by SNC, Net | 834,569,032.00 | 763,909,031.99 | 1,097,065,935.45 | 626,520,410.02 | 620,178,950.52 | 566,254,445.35 |
| **Total Fixed Assets** | **834,569,032.00** | **763,909,031.99** | **1,097,065,935.45** | **626,520,410.02** | **620,178,950.52** | **566,254,445.35** |
| Notes/Loans Receivable-Noncurrent | 32,164,646.72 | 16,536,900.04 | 35,645,163.18 | 54,257,060.00 | 28,367,000.00 | 9,956,330.57 |
| **Total Other Assets** | **32,164,646.72** | **16,536,900.04** | **35,645,163.18** | **54,257,060.00** | **28,367,000.00** | **9,956,330.57** |
| **TOTAL ASSETS** | **2,069,509,867.93** | **1,838,433,041.31** | **2,423,830,948.82** | **1,873,633,349.20** | **2,013,070,867.73** | **1,919,442,688.78** |
| **LIABILITIES** | | | | | | |
| Accounts Payable | 313,817,733.20 | 314,008,927.21 | 357,807,456.97 | 266,400,568.98 | 163,695,335.28 | 173,855,930.58 |
| Offerings and Agency | 57,618,803.96 | 205,814,535.00 | 245,049,009.13 | 124,854,586.86 | 173,823,042.50 | 30,468,165.09 |
| Loans Payable - Current | - | - | 2,830,244.15 | 8,602,216.04 | 7,416,987.59 | 4,755,936.80 |
| **Total Current Liabilities** | **371,436,537.16** | **519,823,462.21** | **605,686,710.25** | **399,857,371.88** | **344,935,365.37** | **209,080,032.47** |
| Loans Payable - Noncurrent | - | - | - | 2,830,244.15 | 11,432,460.19 | 20,488,573.01 |
| **Total Other Liabilites** | | | | **2,830,244.15** | **11,432,460.19** | **20,488,573.01** |
| **TOTAL LIABILITIES** | **371,436,537.16** | **519,823,462.21** | **605,686,710.25** | **402,687,616.03** | **356,367,825.56** | **229,568,605.48** |
| **NET ASSETS** | | | | | | |
| Unallocated Net Assets - Tithe | (3,942,984,682.87) | (3,741,163,336.93) | (3,215,052,050.65) | - | - | (1,839,298,650.51) |
| Unallocated Net Assets - Non-tithe | 4,543,635,388.11 | 3,982,844,532.62 | 3,613,987,037.25 | 3,336,095,328.13 | 3,088,993,045.27 | 2,767,563,955.24 |
| Allocated Net Assets | 301,433,593.53 | 313,019,351.42 | 322,143,316.52 | 223,115,086.25 | 199,628,522.51 | 195,354,333.22 |
| Net Invested in Plant | 795,989,032.00 | 763,909,031.99 | 1,097,065,935.45 | 626,520,410.02 | 620,178,950.52 | 566,254,445.35 |
| **Total Net Assets** | **1,698,073,330.77** | **1,318,609,579.10** | **1,818,144,238.57** | **1,470,945,733.17** | **1,656,703,042.17** | **1,689,874,083.30** |
| **TOTAL LIABILITIES & NET ASSETS** | **2,069,509,867.93** | **1,838,433,041.31** | **2,423,830,948.82** | **1,873,633,349.20** | **2,013,070,867.73** | **1,919,442,688.78** |

# COMBINED STATEMENT OF FINANCIAL ACTIVITY

AS OF DECEMBER 31, 2021 FROM 2016

| OPERATING ACTIVITY | 2021 | 2020 | 2019 | 2018 | 2017 | 2016 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Operating Income** | | | | | | |
| Tithe Income, Net | 2,610,653,915 | 2,494,103,442 | 3,323,741,464 | 2,961,768,116 | 2,667,947,556 | 2,034,190,514.35 |
| Offering Income & Specific Donations | 531,249,438 | 511,246,632 | 741,169,646 | 1,062,710,982 | 717,891,867 | 685,633,841.02 |
| Investment Income | | 0 | 1,459,765 | | | 50,360.58 |
| Gain(Loss) From Investments | | 0 | 120,895 | | | 27,491,194.41 |
| Other Operating Income | 268,849,300 | 395,475,636 | 469,783,309 | 329,219,567 | 78,540,912 | |
| **Total Earned Operating Income** | **3,410,752,653** | **3,400,825,709** | **4,536,275,079** | **4,353,698,665** | **3,464,380,335** | **2,747,365,910.36** |
| **Operating Expenses** | | | | | | |
| Employee Related Expenses | 2,298,529,918 | 2,448,614,621 | 3,183,286,536 | 2,859,586,489 | 2,375,607,450 | 1,679,242,766.99 |
| Travel Expenses | 192,305,942 | 171,432,454 | 324,235,390 | 263,304,786 | 215,218,564 | 163,760,194.50 |
| Program Specific | 76,508,894 | 60,207,955 | 136,444,949 | 561,841,777 | 118,956,880 | 112,577,275.11 |
| Administrative Expenses | 173,120,476 | 211,686,552 | 165,661,251 | 195,819,982 | 169,170,250 | 137,024,663.47 |
| Office Expenses | 194,620,358 | 173,110,921 | 267,687,365 | 142,084,721 | 156,367,537 | 157,660,045.35 |
| General Expenses | 17,503,135 | 156,474,402 | 54,491,977 | 204,471,872 | 225,136,690 | 107,060,313.70 |
| Plant Operation | 55,147,516 | 109,665,271 | 199,250,254 | 165,082,861 | 131,293,606 | 119,791,946.99 |
| Other Property Expense | 17,220,693 | 0 | 9,604,640 | 17,802,119 | 6,000,000.00 | 486,000.00 |
| **Total Operating Expense** | **3,024,956,933** | **3,331,192,175** | **4,340,662,362** | **4,409,994,608** | **3,397,750,977** | **2,477,603,206.11** |
| **Increase (Decrease) Before Approp** | **385,795,720** | **69,633,534** | **195,612,717** | **-56,295,943** | **66,629,358** | **269,762,704.25** |
| **Operating Appropriations** | | | | | | |
| Tithe Appropriation Received | | 0 | 5,828,972 | | | |
| Tithe Appropriation Disbursed | -3,300,000 | -6,105,000 | -75,795,000 | -44,878,000 | | |
| Non-tithe Appropriation Disbursed | -24,953,110 | -28,191,283 | -62,292,925 | -84,583,366 | -114,031,641 | (108,431,126.00) |
| Net Appropriation Retained | -6,331,968 | -34,296,283 | -132,258,953 | -129,461,366 | -114,031,641 | (108,431,126.00) |
| **Increase (Decrease) from Operations** | **379,463,752** | **35,337,250** | **63,353,765** | **-185,757,309** | **-47,402,283** | **288,580,977.14** |
| **CAPITAL ACTIVITY** | | | | | | |
| Other Capital Income | | 199,850,866 | 283,844,734 | | | |
| Capital Appropriations Disbursed | NGBF?? | -67,727,510 | 0 | | | |
| Other Capital Expenses | ASSETS | -540,984,000 | 0 | | -380,588 | |
| Net Capital Increase (Decrease) | | -408,860,643 | 283,844,734 | 0 | -380,588 | - |
| **Increase (Decrease) Before Transfers** | **379,463,752** | **-373,523,393** | **347,198,498** | **-185,757,309** | **-47,782,871** | **288,580,977.14** |
| **Net Assets Increase (Decrease) for the** | **379,463,752** | **-373,523,393** | **347,198,498** | **-185,757,309** | **2,435,230,327** | **288,580,977.14** |
| **Net Assets, January 1, Of every year** | **1,318,609,579** | **1,818,144,239** | **1,470,945,733** | **1,656,703,042** | **0** | **1,401,293,106.16** |
| **Net Assets, December 31, Of every year** | **1,698,073,331** | **1,444,620,846** | **1,818,144,232** | **1,470,945,733** | **2,435,230,327** | **1,689,874,083.30** |

# WORKING CAPITAL & LIQUIDITY STATEMENT

AS OF DECEMBER 31, 2021 FROM 2016

| | 2021 | 2020 | 2019 | 2018 | 2017 | 2016 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **WORKING CAPITAL** | | | | | | |
| Current Assets | 1,202,776,189 | 1,057,987,109 | 1,291,119,850 | 1,192,855,879 | 1,363,813,013 | 1,343,231,913 |
| Current Liabilities | 371,436,537 | 519,823,462 | 605,686,710 | 399,857,372 | 358,835,290 | 209,080,032 |
| Actual Working Capital | 831,339,652 | 538,163,647 | 685,433,140 | 792,998,507 | 1,004,977,724 | 1,134,151,881 |
| Percentage of Operating Expenses | 609,642,009 | 779,635,492 | 877,058,056 | 891,589,295 | 583,368,200 | 488,814,284 |
| Allocated Net Assets | 301,433,594 | 313,019,351 | 322,143,317 | 223,115,086 | 199,628,523 | 195,354,333 |
| Recommended Working Capital | 911,570,602 | 1,104,058,220 | 1,213,220,372 | 1,126,930,806 | 800,101,468 | 700,433,286 |
| Excess (Deficiency) of Actual over Recommended | -80,230,950 | -565,894,573 | -527,787,232 | -333,932,299 | 204,876,255 | 433,718,595 |
| **Percentage of Actual to Recommended Working Capital** | **91.20%** | **48.47%** | **56.50%** | **70.37%** | **125.47%** | **161.92%** |
| **Current Ratio** | **3.24** | **2.04** | **2.13** | **2.98** | **3.80** | **6.42** |
| **LIQUIDITY STATEMENT** | | | | | | |
| Cash and Cash Equivalents | 197,093,531 | 206,370,653 | 294,154,525 | 331,877,408 | 620,843,311 | 764,464,097 |
| Investments | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Receivable From NTUC | 0 | 0 | 0 | 0 | 28,007,971.86 | 32,918,287.46 |
| Total Liquid Assets | 197,093,531 | 206,370,653 | 294,154,525 | 331,877,408 | 648,851,283 | 797,382,384 |
| Less Commitments: | | | | | | |
| Current Liabilities | 371,436,537 | 519,823,462 | 605,686,710 | 399,857,372 | 358,835,290 | 209,080,032 |
| Allocated Net Assets | 301,433,594 | 313,019,351 | 322,143,317 | 223,115,086 | 199,628,523 | 195,354,333 |
| Total Commitments | 672,870,131 | 832,842,814 | 927,830,027 | 622,972,458 | 558,463,812 | 404,434,366 |
| **Net Liquid Assets** | **-475,776,599** | **-626,472,161** | **-633,675,501** | **-291,095,050** | **90,387,471** | **392,948,019** |
| **Percentage Liquid Assets to Commitments** | **29.29%** | **24.78%** | **31.70%** | **53.27%** | **116.19%** | **197.16%** |

# STATEMENT OF CASH FLOWS

FOR TWELVE MONTHS ENDING DECEMBER 31, 2020.

| | TOTAL 2020 | TOTAL 2019 | TOTAL 2018 | TOTAL 2017 |
|---|---|---|---|---|
| **Cash Flows from Operating Activities:** | | | | |
| Increase (Decrease) in Net Assets | (499,534,659.47) | 347,198,505.40 | (185,757,309.00) | 1,656,703,042.17 |
| Adjustments to eliminate non-cash items and reclassify non-operating items: | | | | |
| Depreciation Expense | (90,991,964.64) | 40,541,757.57 | 31,314,540.50 | 4,062,422,259.56 |
| Allowance for Doubtful Accounts | 103,341,675.00 | 31,852,338.37 | 165,046,729.80 | 269,570,376.59 |
| Asset Disposal or Retirement | 540,984,000.29 | 0.00 | 0.00 | 380,587.50 |
| Gain or Loss in Fair Value of Investments | 0.00 | (120,894.96) | 0.00 | 0.00 |
| Decrease (Increase) in Accounts Receivable | (35,614,140.14) | (173,094,083.41) | (256,263,899.65) | (867,776,218.58) |
| Decrease (Increase) in Notes Receivable | 25,511,736.90 | (4,987,340.12) | (15,095,333.27) | (30,910,166.73) |
| Decrease (Increase) in Inventories | 2,198,680.00 | 20,287,400.60 | (5,775,192.90) | (25,029,687.70) |
| Decrease (Increase) in Prepayments and Other Current Assets | 49,643,916.38 | (10,045,168.87) | (5,209,168.97) | (89,535,909.87) |
| Increase (Decrease) in Accounts Payable | (43,798,529.76) | 91,406,887.99 | 102,705,233.70 | 163,695,335.28 |
| Increase (Decrease) in Notes Payable | (2,830,244.15) | (5,771,971.89) | 1,185,228.45 | 7,416,987.59 |
| Increase (Decrease) in Other Current Liabilities | (39,234,474.13) | 120,194,422.27 | (48,968,455.64) | 173,823,042.50 |
| **Net Cash Provided (Used) by Operating Activities** | **9,675,996.28** | **457,461,852.95** | **(216,817,626.98)** | **5,320,759,648.31** |
| **Cash Flows from Investing Activities:** | | | | |
| Proceeds from Maturity of Investments | 0.00 | 120,894.96 | 0.00 | 0.00 |
| Purchase of Plant Assets | (101,331,600.00) | (339,394,398.00) | (37,656,000.00) | (4,628,529,192.58) |
| Purchase of Plant WIP | 156,189,352.81 | (171,692,885.00) | 0.00 | (54,452,605.00) |
| Notes Receivable Issued | 19,375,263.14 | 18,611,896.82 | (25,890,060.00) | (28,367,000.00) |
| **Net Cash Provided (Used) by Investing Activities** | **74,233,015.95** | **(492,354,491.22)** | **(63,546,060.00)** | **(4,711,348,797.58)** |
| **Cash Flows from Financing Activities** | | | | |
| Principal Payments made on Long-term Debt | 0.00 | (2,830,244.15) | (8,602,216.04) | 0.00 |
| **Net Cash provided (used) by Financing Activities** | 0.00 | (2,830,244.15) | (8,602,216.04) | 11,432,460.19 |
| **Net Increase (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | 83,909,012.23 | (37,722,882.42) | (288,965,903.02) | 620,843,310.92 |
| Beginning Cash and Cash Equivalents - Includes Agency Cash (Overdraft) | 294,154,525.48 | 331,877,407.90 | 620,843,310.92 | 0.00 |
| Ending Cash and Cash Equivalents - Includes Agency Cash (Overdraft) | 378,063,537.71 | 294,154,525.48 | 331,877,407.90 | 620,843,310.92 |
| Less Cash Held for Agency | 205,814,535.00 | 264,403,846.08 | 143,989,008.24 | 184,875,437.09 |
| **Cash and Cash Equivalents** | 172,249,002.71 | 29,750,679.40 | 187,888,399.66 | 435,967,873.83 |

# AUDITORS OPINION ON THE FINANCIAL STATEMENT



# TAARIFA YA IDARA YA HUDUMA ZA KICHUNGAJI NA FAMILIA.



**MCH. SIMEO MAKUNJA**

MKURUGENZI WA IDARA YA HUDUMA ZA KICHUNGAJI NA FAMILIA.



MKUTANO MKUU WA NANE WA SNC (SNC SESSION)
SEPTEMBA 22, 2022.

## UTANGULIZI.

Namshukuru Mungu aliyenipatia uhai, nguvu na fursa ya kumtumikia katika muhula wa miaka mitano. Nishukuru Uongozi wa Union NTUC, Uongozi wa Conference SNC, Wakurugenzi, Wajumbe wa Kamati Kuu ya SNC pamoja na waumini wa Kanisa kwa ushirikiano ambao tumekuwa tukitumika kwa pamoja katika kutekeleza kaulimbiu 2016-2020 ya "Utume kwanza, ni wakati wa mavuno" na kauli mbiu ya "Nitakwenda" 2021 na kutimiza malengo ya Idara ya Huduma za Wachungaji na Familia. Bwana awabariki.

## MALENGO YA IDARA 2016 -2022.

- Kutoa Huduma za Kichungaji na kuleta watu kwa Yesu.
- Kutembelea familia za Wachungaji.
- Kuwa na siku ya kutambua Wachungaji.
- Mkutano wa Wachungaji na wake zao.
- Mkutano wa wake za Wachungaji.
- Kufanya mahubiri ya hadhara yatakayoendeshwa na Wake za Wachungaji.
- Kuwa na mkutano wa watoto wa Wachungaji.
- Kufanya mahubiri ya hadhara yatakayoendeshwa na Watoto wa wachungaji.
- Kuwa na maombi na kufunga siku kumi kila mwanzo wa mwaka maombi ya kanisa la ulimwenguni.
- Usomaji wa Biblia kwa mpango kila Mwaka.
- Kuunda kamati ya maombi makanisani na kufanya kazi.
- Semina ya Huduma za Kichungaji kwa wachungaji.
- Kuwa na semina ya Huduma za Familia Kanda zote SNC.
- Mkutano wa Huduma za Familia.

## A. HUDUMA ZA WACHUNGAJI

**Idadi ya Wachungaji Jan. 2016 – 2022 katika Huduma za Kichungaji.**

| S/N | HABARI ZA WACHUNGAJI | Idadi ya Wachungaji | SNC & NGBF KABLA YA KUGAWANYWA | | | | SNC BAADA YA KUGAWANYWA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Dec 2015 | Dec. 2016 | Dec. 2017 | Dec. 2018 | Dec. 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
| 1 | Jumla ya Wachungaji SNC | 73 | 84 | 101 | 103 | 123 | 70 | 85 | 94 |
| 2 | Walio katika mitaa | 64 | 69 | 83 | 84 | 102 | 58 | 69 | 78 |
| 3 | Walio ofisini | 9 | 10 | 11 | 11 | 12 | 8 | 8 | 9 |
| 4 | Wanao hudumia Taasisi | 3 | 5 | 7 | 8 | 9 | 7 | 8 | 7 |
| 5 | Waliowekewa mikono | 30 | 28 | 35 | 41 | 45 | 30 | 35 | 39 |
| 6 | Hawajawekewa mikono | 43 | 54 | 66 | 62 | 61 | 43 | 50 | 55 |

Idadi ya Wachungaji waliojiunga katika huduma za kichungaji 2020 - 2022 ni 24.

**Idadi ya Wachungaji Waliowekewa Mikono Mwaka 2016 hadi 2022.**

| Mwaka | Idadi | Mahali huduma Ilipofanyika |
|---|---|---|
| 2016 | 2 | KirumbaSDA Church |
| 2017 | 6 | Kahama SDA Church |
| 2018 | 4 | Pasiansi SDA Church |
| 2019 - Jul. | 4 | Geita Central SDA Church |
| - Dec. | 3 | Singida |
| 2020 | 5 | Bariadi SDA Church |
| 2022 | 6 | Nyegezi SDA Church |
| **Total** | **30** | |



*Picha 1: Huduma ya kuwawekea wachungaji mikono.*

**Majina ya Wachungaji Waliowekewa Mikono Mwaka 2016 hadi 2022:**

1. Mch. Lazaro Mbogo
2. Mch. Bezarel Nzobano
3. Mch. Elias Y. Shija
4. Mch. Stephen H. Manema
5. Mch. Zablon N. Meadu
6. Mch. Joseph J. Apollo
7. Mch. Renatus M. Izumangiji
8. Mch. Suleman M. Malima.
9. Mch. Ray Wankyo
10. Mch. Reuben B. Shija
11. Mch. Daniel V. Magesa
12. Mch. Seth B. Kamba
13. Mch. Titus M. Mayugu
14. Mch. Mabula T. Kilalo
15. Mch. Baraka K. Mulungu
16. Mch. Godwin L. Bitwayiki
17. Mch. Kulindwa H. Kuyenga
18. Mch. Kuba J. Mayalu
19. Mch. Joshua M. Mbwambo
20. Mch. Edson L. Maige
21. Mch. Elias M. Makambi
22. Mch Elton M. Daniel
23. Mch. Emmanuel J. Mpina
24. Mch. Ayubu M. Lenga
25. Mch. Emmanuel M.Salyungu
26. Mch. Kalangi M. Mtobesya
27. Mch. Joel Robinson Chacha
28. Mch. Gamali B. Salumu
29. Mch. Marco F. Mlingwa
30. Mch. Baraka B. Nchama

**Wachungaji Wastaafu.**

- Wachungaji waliostaafu katika muhula huu ni 1.
- Wachungaji waliostaafu zamani wako 9.

**Wachungaji Waliolala Mauti.**

- Wachungaji waliolala mauti wakiwa kazini Mch. Yusufu Mharagi na Pr. Bezareli Nzobano.
- Wachungaji waliolala mauti wakiwa wamestaafu ni Mch. Apollo J. Konzi, Mch. Ephraim F. Kilyunguma, Mch. Charles Mkwabi, Mch. Erasto Nzumbi, Mch. Phaustine Karuma, Mch. Jeremiah Matulanya, Mch. Aristarko Mkama, Mch. Daudi Balula, Mch. Mugayiwa Lugembe na Mch. Mika Kamambi.

## Wachungaji na Elimu

| Wachungaji walio na Elimu Ungu SNC Kufikia 2022 | Idadi |
|---|---|
| Wachungaji walio na Cheti | 9 |
| Wachungaji walio na Stashahada | 4 |
| Wachungaji walio na Shahada ya Kwanza | 49 |
| Wachungaji walio na Shahada ya Uzamili | 8 |
| Wachungaji walio na Shahada ya Uzamivu | 0 |
| Wachungaji wasio na Elimu ya Kichungaji | 24 |
| Wachungaji walioenda masomoni na kuhitimu | 14 |
| Wachungaji walio masomoni | 19 |

## Huduma za Kichungaji na Uinjilisti Kanisani

- Idadi ya makanisa yaliyopata huduma za kichungaji kwa ujumla ni 639
- Idadi ya makundi yaliyohudumiwa katika conference ni makundi 327
- Baada ya kugawanywa Conference hadi kufikia Jun. 2022 tumekuwa tukihudumia washiriki wa Kanisa wapatao 163,979.
- Uwiano wa Washiriki wa Kanisa kwa Mchungaji mmoja ni 1:2186.
- Uwiano wa Makanisa kwa Mchungaji mmoja ni 1:9.
- Semina za huduma za Kichungaji kwa wachungaji zilifanyika kila mwaka. Wachungaji waliowekewa mikono walipewa semina.
- Wachungaji 13 walipewa pikipiki kupitia kitengo cha Global Mission.
- Wachungaji wameshiriki kuhubiri katika mahubiri ya TMI kwa asilimia 100.

- Familia za wachungaji walioko kazini, wastaafu, wagane na wajane waliotembelewa wastani kwa kila mwaka ni familia 98.
- Tunawashukuru washiriki wetu katika mitaa na makanisa kwa siku ya kumtambua Mchungaji na kumtia moyo katika huduma yake ya kichungaji, Bwana awabariki.





## B. CHAMA CHA WENZI WA WACHUNGAJI SNC

**Idadi ya Wenzi wa Wachungaji kufikia 2022.**

| S/N | WENZI WA WACHUNGAJI SNC | IDADI |
|---|---|---|
| 1 | Wenzi wa Wachungaji kazini | 81 |
| 2 | Wenzi wa Wachungaji Wastaafu | 10 |
| 3 | Wenzi wa Wachungaji Wajane | 17 |

Wenzi za wachungaji wastaafu waliolala mauti katika muhula huu ni Mrs. Juliana D. Balula, Mrs. Mugaywa Lugembe, Mrs. Perish Gamaya na Mrs. Ellen C. Nkwabi.

**Mahubiri ya Hadhara yaliyoendeshwa na Wenzi wa Wachungaji.**

- Wenzi wa Wachungaji wameshiriki kikamilifu katika TMI, wamefanya mahubiri ya hadhara Oktoba 2018 Kayenze - Mtaa wa Butundwe mkoani Geita, watu 148 walibatizwa. Katika mahubiri haya tulikuwa na Mratibu wa Chama cha Wenzi wa Wachungaji Union, Mrs. Rachel Mahende. Tulipata upendeleo wa kuwa na Mwenyekiti wa Union Mch. Godwin Lekundayo, alikuja kuwatia moyo na kutoa Tsh. 2,000,000, pia aliweka jiwe la msingi kwenye kanisa lililojengwa katika kiwanja cha eka mbili kilichonunuliwa na Wenzi wa Wachungaji Tshs. 3,720,000/=. Kanisa hilo lilipewa jina la Shepherdess.
- Wenzi wa Wachungaji walisambaza vitabu 120 wakati wa kuandaa mahubiri yao katika Hospitali ya Geita.
- Mwaka 2019 wamefanya mahubiri ya TMI mtaa wa Tinde, watu waliobatizwa 105 na mahubiri yaligharimu kiasi cha Tsh. 1,550,000/=.
- Mahubiri ya Nyanguge Mtaa wa Ngulyati mwezi May 2022 watu 23 walibatizwa na kila mmoja wao alipewa Biblia zenye thamani ya Tsh. 460,000. Katika mahubiri haya uinjilisti wa nyumba kwa nyumba ulifanyika na kugawa vitabu 164 Tumaini la Mwisho, Sabato ya kweli na Daniel na siku zetu, ni pamoja na nguo na viatu. Thamani ya vitu walivyogawa ni Tsh. 1,128,200.

**Semina na mikutano ya Wenzi wa Wachungaji.**

- Wenzi wa wachungaji walihudhuria masomo (continuing Education Course) 2018 Kanisa la Geita Central na kule Singida 2019 na kuwatunuku cheti Wenzi wa Wachungaji 60.
- Mkutano wa uamsho na semina zilizofanyika Rorya - Mwanza mwezi Desemba 2021 wa Wenzi za Wachungaji walio kazini, wastaafu na wajane, mahudhulio kwa ujumla walikuwa 82. Masomo mbalimbali yalitolewa kama vile huduma kwa Kanisa na jamii, mapishi, ujasiriamali, malezi ya watoto, n.k.
- Wamefanikiwa kutembeleana katika shida na raha na kuwafanya kuwa pamoja nyakati zote.





## C. WATOTO WA WACHUNGAJI (PASTORS' KIDS).

Watoto wa Wachungaji wametoa huduma mbalimbali SNC na nje ya Conference yetu kama vile mahubiri ya hadhara, kutoa huduma kwa jamii, kutembelea na kuhudhulia semina zilizotolewa. Tuna watoto wa wachungaji wapatao 412.

- Mwezi Juni 2017 watoto wa wachungaji walihudhulia mkutano wa Divishen wa Watoto wa Wachungaji uliofanyika Arusha, ambapo watoto wa wachungaji 28 walihudhuria.
- Kongamano la watoto wa wachungaji Tanzania lililofanyika mwezi Dec. 2021 Kanisa la Nyegezi – Mwanza likiendeshwa na Unioni ya NTUC na STUM, waseminishaji walikuwa Mrs. Winifrida Mitekaro toka ECD, Mch. Mark Malekana toka STUM na Mch. Simeo Makunja toka SNC.
- Mkutano mwingine ulifanyika Kahama 2018 ambapo watoto wa wachungaji 84 walikutanika kwa ajili ya ibada na mashauriano.
- Mikutano mingine ya Watoto wa Wachungaji iliyofanyika ndani ya Conference: mwezi Juni 2019 ulifanyikia Mukidoma, Kisesa – Mwanza, waseminishaji walikuwa Pr. Ngussa Steven, Pr. Switta Elias na Mr. Sadick. Waliohudhuria walikuwa 102. Mwaka 2020 mikutano mitatu ilifanyika Mabatini, Butimba na Pasiansi.
- Watoto wa wachungaji wamekuwa wakitembeleana na kutiana moyo katika shida na raha na kusaidiana katika mahitaji mbalimbali ya kiroho na kimwili pia.
- Wameshiriki pia katika huduma kwa jamii, wakitoa huduma za afya, kugawa nguo kwa wahitaji na vitabu. Gharama ya vitabu vilivyotolewa ni Tsh. 10,000,000.

## D. UKUAJI KIROHO WA WASHIRIKI

- Tunamshukuru Mungu ndani ya Conference yetu waumini wameitikia wito wa uamsho kwa kufunga na kuomba siku kumi za maombi wakishiriki kwa pamoja masomo maalumu yaliyoandaliwa na kanisa GC.
- Pamekuwa na mwitikio mkubwa wa makanisa kuendesha program ya maombi ya Sabato ya kwanza ya kila robo.
- Kwa mujibu wa taarifa za robo tulizopokea, wastani wa washiriki waliosoma Biblia kwa mpango kila mwaka ni 16, 322.
- Ukuaji kiroho na uamsho katika kufanya matengenezo kunahitaji kusoma vitabu. Vitabu vya Roho ya Unabii ambavyo vimetumika muhula huu ni kitabu cha Wazee na Manabii, Manabii na Wafalme. Pia tumekuwa na kitabu cha kusoma kila mwaka ambavyo ni Pendo Lisilo Kifani, Nguvu ya Tumaini, Tumaini kwa Familia za leo, Tumaini Katika Tufani, Wakati Taabu Itakapokoma na Tumaini la Mwisho ni pamoja na familia kuwa na vitabu vya Kesha la Asubuhi.
- Kamati za maombi makanisani ziliundwa na kupewa Semina kuhusu Uamsho na matengenezo na kufanyia kazi makanisani, matokeo yake ni mahudhulio ya waumini kuongezeka kila mwaka katika siku kumi za maombi kila mwanzo wa mwaka.

## E. HUDUMA ZA FAMILIA

- Majuma ya maombi ya Huduma za Familia kwa ratiba ya GC yaliendeshwa Makanisani mara mbili kwa mwaka katika kudumisha familia ya Kikristo ni pamoja na majuma ya familia yaliyoandaliwa na Kanisa mahalia, Conference na Union.
- Tulihudhuria Kongamano la Union la Huduma za Familia lililofanyika Kanisa la Lubaga – Shinyanga mwezi Feb. 2022 likiongozwa na viongozi wetu wa Huduma za Familia toka ECD Pr. M. Mitekaro na Mrs. W. Mitekaro, NTUC – Pr. D. Fue, wakishirikiana na Mrs. B. Kahitira - NGBF na Mr. Suleiman D. Mathias toka kanisa la Nyamhongolo, Mwanza.
- Tumekuwa na semina za Huduma za Familia za Union zilizofanyika mwaka 2021, kanisa la Nyegezi – Mwanza na kanisa la Bariadi – Simiyu zikisimamiwa na Kiongozi wa Huduma za Familia toka NTUC - Pr. D. Fue, akishirikiana na Pr. S. Makunja na Mrs. Urio.
- Semina na mafunzo ya uongozi zimetolewa kwa wazee wa Kanisa na mashemasi.



## MALENGO YA IDARA YA HUDUMA ZA KICHUNGAJI 2023

(a) Kuhakikisha kwamba kila familia ya Mchungaji na mshiriki wanasoma Biblia kwa mpango.
(b) Kuhakikisha kila familia inakuwa na Kitabu cha Roho ya Unabii, Kesha la Asubuhi na kitabu cha mwaka ili kukuza hali ya kiroho ya kila mshiriki.
(c) Kuandaa masomo kwa wachungaji na washiriki yanayohusu ukuaji kiroho katika Nyanja zote.
(d) Kamati za maombi makanisani kutekeleza wajibu wake kikamilifu.
(e) Kuandaa mafunzo kwa wachungaji juu ya uongozi wa kichungaji ili kuwawezesha wafikie viwango vya juu vya kiroho.
(f) Kuwa na siku ya kuwatambua wachungaji katika South Nyanza Conference.
(g) Kuwawezesha Wachungaji kupata vyombo vya usafiri kurahisisha utendaji wa kazi katika zama hizi.
(h) Kugawa mitaa mikubwa ili kurahisisha kazi ya Mchungaji wa mtaa.
(i) Kuwa na mahubiri ya Wenzi za Wachungaji.
(j) Kuwa na mahubiri ya watoto wa wachungaji.
(k) Kutayarisha mkutano wa kiroho kwa ajili ya watoto wa wachungaji.
(l) Kuwa na mkutano wa Wenzi wa Wachungaji.
(m) Kuwa na mkutano wa wachungaji waliowekewa mikono.
(n) Kuhimiza vijana ambao hawajaoa wapate wenzi wa maisha kanisani.
(o) Kuhimiza uaminifu katika ndoa na kutoa semina katika mkakati mzima wa kupunguza taraka kwa wanandoa kanisani.
(p) Kuhimiza upatikanaji wa taarifa za idara kwa wakati.

# TAARIFA YA IDARA YA UWAKILI, MAENDELEO, AMANA, MAJENGO NA  ATAPE.



**MCH. BARAKA B. NCHAMA**

MKURUGENZI WA IDARA YA UWAKILI,
MAENDELEO, AMANA, MAJENGO
NA CHAMA CHA ATAPE.

MKUTANO MKUU WA NANE WA SNC (SNC SESSION)
SEPTEMBA 22, 2022.

## UTANGULIZI

Tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu maana amekuwa mwema katika huduma za idara ya uwakili, maendeleo, amana, majengo na chama cha ATAPE chini ya usimamizi wa maofisa wa Union na Conference, Kamati kuu ya Jimbo, ushirikiano wa wakurugenzi, watumishi wa jimbo, wachungaji na washiriki wote, Jina la Bwana litukuzwe. Hakika Bwana amekuwa ni ngome na nguvu yetu katika huduma hizi. Tulianza shughuli za idara ndani ya mikoa minne (Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Geita) mwaka 2016 na sasa tunapoileta taarifa hii mwaka 2022, shughuli zetu ziko katika mikoa miwili (Mwanza na Simiyu). Hii ni baada ya mikoa ya Geita na Shinyanga kuunda field mpya mwaka 2020.

# IDARA YA UWAKILI

## MIPANGO YA IDARA (2016 - 2022)

Kukuza uhusiano wa waumini na Mungu wao kwa kiwango cha juu.

Kuongeza idadi ya Waaminifu kila mwaka.

Kufikia Malengo yaliyokusudiwa ya ukusanyaji wa zaka na sadaka kwa kila mwaka.

Kuendeleza kauli mbiu ya utume wa kanisa ya ***Mungu Kwanza*** (2015 -2020) na ***Nitakwenda*** (2021 – 2025).

Kushirikiana na idara zingine katika mikutano yao kupenyeza elimu kuhusu uwakili na ujasiriamali. Ikiwemo mikutano ya vijana, wanawake, walei/Wainjilisti wa Vitabu. nk

Kutoa semina kwa Wachungaji, Wajumbe wa Baraza la kanisa na washiriki namna bora na mbinu za kuongeza na kudumisha idadi ya waaminifu kwa kila kanisa.

## YALIYOFANYIKA KATIKA IDARA YA UWAKILI 2016 - 2022.

i. Idara imefanikiwa kuwasaidia washiriki kukuza mahusiano bora na Mungu wao kwa kuhimiza utumiaji talanta, nguvu, muda, mvuto na mali ili kuendeleza kazi ya Bwana katika conference na kwa kanisa la ulimwengu. Hili limefanywa kupitia semina mbalimbali za Uwakili zilizoendeshwa kwa nyakati tofauti kwa jimbo zima na mitaa yote kufikiwa.

ii. Tumeshiriki kikamilifu katika msukumo wa kauli mbiu ya utume ya ***Mungu Kwanza (God First)*** na ***Nitakwenda (I Will Go)*** kwa kuwakumbusha waumini utoaji kwa mpango ambapo zaka na sadaka za vitu vilihimizwa na magunia yenye nembo ya Mungu kwanza yalisambazwa kwa conference nzima, mashati yalitengenezwa kuamsha ari ya moto huu, nyimbo ziliimbwa za Mungu kwanza nyakati za semina na mpangilio wa kutoa siku za Sabato uliwekwa vizuri.

iii. Wakati wa makambi utoaji umeendelezwa kila siku na siku ya Alhamisi imekuwa kivutio kwa utoaji wa sadaka za vitu

kulingana na shughuli aifanyayo mtu (Kutikisa mganda), hili limeongeza sana sadaka ya kambi kwa mitaa mingi mwaka kwa mwaka. Nyimbo za kristo zimekuwa ndiyo uimbaji unaopendekezwa wakati wa matoleo na umeongeza hamasa ya ibada kwa njia ya matoleo.

iv. Idara imefanikiwa kuratibu, kusimamia na kuendesha majuma mbalimbali ya uwakili kutoka ngazi ya divisheni na union mara mbili kwa kila mwaka, ambapo wachungaji walibadilishana vituo pamoja na Wainjilisti Walei katika confrensi nzima jambo lililoongeza ufahamu mkubwa kwa washiriki na kukuza mahusiano yao na Mungu. Katika majuma hayo yafuatayo pia yalifanyika:
   - Semina za uwakili ziliendeshwa kwa kila kanisa.
   - Washiriki walitembelewa majumbani na katika maeneo yao ya kazi.
   - Maombi yalifanyika.
   - Zaka na sadaka za mifugo na mazao zilitengwa.
   - Miradi na biashara mbalimbali viliombewa.
   - Washiriki na waumini waliongozwa kufanya maagano ya uaminifu na Bwana wao.

v. Idara kwa kushirikiana na idara zingine imefanikiwa kufikisha elimu ya mambo ya uwakili kwa washiriki wengi zaidi wakiwemo vijana kupitia mikutano ya Vijana, wanawake kupitia makongamano yao na mikutano mbalimbali ya wainjilisti walei na wa vitabu.

vi. Kwa miaka 3 mfululizo kwa kushirikiana na maofisa wa jimbo na wakurugenzi wote (team work) tumefanikiwa kutembelea mitaa yote ya jimbo kwa muda mfupi kama timu, na kufanikisha yafuatayo:
   - Kuendesha semina za uwakili, ujasiriamali, utoaji wa mpango na udhibiti wa ndani ya kanisa kwa kila mtaa.
   - Kutembelea washiriki katika miradi, biashara na ofisi zao za uzalishaji.
   - Kufanya maombi maalum ya Baraka katika miradi, biashara na kazi zao.

- Kutenga zaka na sadaka za mifugo na mazao katika mazizi na mashamba.
- Washiriki na waumini waliongozwa kufanya maagano ya uaminifu na Bwana wao kwa kupewa vyeti maalum vya **Mungu Kwanza** na **Nitakwenda**.

vii. Idara imefanikiwa kutengeneza jicho la kanisa kwa njia ya vitabu maalum na makanisa mengi yameanza kutumia vitabu hivyo, program hii imerahisisha utendaji kwa makanisa na imeongeza matoleo sambamba na watoaji.

viii. Tumefanikiwa kutoa taarifa za matoleo kila mwezi kidigitali kwa kuonesha mitaa iliyofanya vizuri zaidi na hili limeongeza hamasa kwa Washiriki na wachungaji kwa ujumla.

ix. Idara imefanikiwa kuanzisha na kudumisha program ya kutuma nukuu za uwakili (Jumbe za Uwakili) kwa kila juma (ijumaa) kupitia mitandao ya kijamii ili kuendeleza mkazo wa elimu ya uwakili kwa washiriki.

x. Idara kwa kushirikiana na maofisa wa jimbo imefanikiwa kutoa semina kwa wachungaji na wajumbe wa baraza la kanisa kwa mitaa mbalimbali na kwa nyakati tofauti jambo lililoleta ufanisi mkubwa katika ukusanyaji na udhibiti wa matoleo katika makanisa.

xi. Idara imefanikiwa kutoa elimu ya mfumo wa matoleo (CFMS) na makanisa yameanza kutumia mfumo huo tangu Januari 2022.

xii. Tumefanikiwa kuanzisha mradi wa kilimo cha alizeti katika eneo la Mwalogwabagole.

xiii. Kwa miaka na mahali tofauti idara imepokea viongozi mbalimbali kutoka ngazi za juu ambao walikuwa chachu kubwa ya msukumo wa uwakili hasa katika kutimiliza kauli mbiu ya Mungu kwanza na Nitakwenda. Viongozi kutoka NTUC – Pr. Dr. G. Lekundayo na P. kikiwa, na kutoka ECD, Pr. Dr. Baptiste na Pr. W. Bagambe walitufikia kwa huduma za Uwakili katika vituo vya Mabatini, Bariadi na Maswa.

xiv. Tangu mwaka 2016 hadi 2020 kiasi cha zaka kimekuwa Tshs. **20,432,137,116.52** sawa na ongezeko la **asilimia 73%**

ikilinganishwa na mwaka 2011 hadi 2015 ilipokuwa **Tshs. 11,806,208,072.29.**

xv. Tangu mwaka 2016 hadi 2020 sadaka ya pamoja iliyokusanywa ni **Tshs 7,724,881,936.12** sawa na ongezeko la **asilimia 78%** ikilinganishwa na mwaka 2011 hadi 2015 sadaka ilipokuwa **Tshs. 4,351,219,047.49.**

Hivyo basi, kwa mwaka 2016 – 2020 idara imefanikiwa kuongeza **mapato ya zaka kwa 73%** na **sadaka kwa 78%** kulingalisha na mwaka 2010 - 2015.

## ULINGANIFU WA MATOLEO YA ZAKA 2011 – 2015 NA 2016 -2020

| MWAKA | ZAKA | MWAKA | ZAKA |
|---|---|---|---|
| 2011 | 1,638,626,063.37 | 2016 | 3,557,880,265.98 |
| 2012 | 2,019,174,102.77 | 2017 | 3,896,501,401.42 |
| 2013 | 2,457,269,200.02 | 2018 | 4,434,941,450.72 |
| 2014 | 2,623,462,620.24 | 2019 | 4,948,271,621.95 |
| 2015 | 3,067,676,085.89 | 2020 | 3,594,542,376.45 |
| **JUMLA KUU** | **11,806,208,072.29** | **JUMLA KUU** | **20,432,137,116.52** |






## ULINGANIFU WA MATOLEO YA SADAKA 2011 – 2015 NA 2016 - 2020.

| MWAKA | SADAKA | MWAKA | SADAKA |
|---|---|---|---|
| 2011 | 560,223,737.94 | 2016 | 1,243,094,078.22 |
| 2012 | 721,667,041.70 | 2017 | 1,324,502,195.76 |
| 2013 | 873,085,177.88 | 2018 | 1,774,233,732.64 |
| 2014 | 994,093,262.75 | 2019 | 1,947,011,676.23 |
| 2015 | 1,111,664,261.82 | 2020 | 1,436,010,253.27 |
| **JUMLA KUU** | **4,351,219,047.49** | **JUMLA KUU** | **7,724,851,936.12** |






## MATOLEO KWA KIPINDI CHA 2016 – 2022.

| MWAKA | IDADI YA MIKOA | ZAKA | SADAKA | MAKAMBI |
|---|---|---|---|---|
| 2016 | 4 | 3,557,880,265.98 | 1,243,094,078.22 | 183,210,371.00 |
| 2017 | 4 | 3,896,501,401.42 | 1,324,502,195.76 | 196,493,191.40 |
| 2018 | 4 | 4,434,941,450.72 | 1,774,233,732.64 | 284,787,527.33 |
| 2019 | 4 | 4,948,271,621.95 | 1,947,041,676.23 | 198,968,672.00 |
| 2020 | 2 | 3,594,542,376.45 | 1,436,010,253.27 | 270,629,567.65 |
| 2021 | 2 | 3,779,091,077.33 | 1,534,894,040.74 | 321,308,598.01 |
| 2022 (JAN-JUNE) | 2 | 2,052,414,759.35 | 817,135,057.61 | |
| **JUMLA KUU** | | **24,211,228,193.85** | **9,259,775,976.86** | **1,455,397,927.43** |

## IDARA YA MAJENGO.

### MAJENGO YA IBADA.

- Idara imefanikiwa kuhimiza makanisa kuendelea kujenga majengo bora na ya kisasa ili huduma za ibada zifanyike kwa ubora. Jumla ya Makanisa Mapya 257 yamejengwa kuanzia 2016 hadi 2022 na yako katika hatua tofautitofauti za ujenzi.
- Majengo ya kanisa yaliyokaa muda mrefu pasipo kupauliwa kwa mwaka 2016 - 2022 yamefanikiwa kupauliwa likiwemo kanisa la Mhangu mtaa wa Salawe, Mlimani mtaa wa Salawe na Paji mtaa wa Paji.
- Majengo ya kanisa yamejengwa katika maeneo Mapya likiwemo kanisa la Mwanjolo, Bulyashi na Mbogo mtaa wa Nkololo.
- Makanisa yapatayo 82 yamekarabatiwa na kupakwa rangi baada ya kuonekana dalili za uchakavu.
- Jimbo limesaidia makanisa 27 kwa mabati na fedha katika kuhimiza ujenzi wa makanisa katika kila kituo cha ibada.
- Kanisa la Ikungulipu katika mtaa wa Itilima liliwekwa wakfu desemba 2021 na kuongeza idadi ya makanisa yaliyowekwa wakfu na kufikia makanisa 11 katika jimbo letu.
- Baadhi ya makanisa yamekamilika na yako mbioni kuwekwa wakfu likiwemo kanisa la Ilemela mtaa wa Pasiansi na Bariadi mtaa wa Ntuzu.



## VIBWETA, OFISI, VYOO NA VISIMA VYA UBATIZO.

- Kumekuwa na hamasa, mwamko na msukumo mkubwa sana kwa kipindi cha mwaka 2016 -2021 katika kubadili taswira ya vibweta, ofisi, vyoo na visima vya ubatizo makanisani. Kwa hakika baadhi ya mitaa na makanisa wameboresha mazingira ya mikutano na ibada mbalimbali hali inayoleta utukufu na utulivu mzuri katika kumwabudu Mungu. Mfano mzuri ni kwa mtaa wa Nyegezi, Shamaliwa, Buswelu, Ntuzu, Meatu n.k
- Vibweta (Platform) 53 vya nje kwa mikutano ya nje ya kanisa vimejengwa na wakati huo vibweta vya ndani ya kanisa 78 vikijengwa kwa huduma za ibada vikiwa kwenye hatua tofauti tofauti za ujenzi.
- Mimbari (Pulpit) 119 zimewekwa na kuongeza mvuto wakati wa kuhubiri nje ya kanisa ama ndani ya kanisa.
- Jumla ya Vyoo vya kisasa 21 vimejengwa ndani ya ofisi za wachungaji na vyoo 49 vya kisasa vimejengwa nje kwa huduma za kanisa.
- Ofisi za kichungaji 28 zimejengwa ili kuifanya huduma ya kichungaji kuwa ya heshima na yenye kumtukuza Mungu.
- Jumla ya Visima vya Ubatizo 30 vinaendelea kujengwa vikiwa katika hatua tofautitofauti za ujenzi na baadhi ya mitaa imekamilisha.



## UJENZI WA NYUMBA ZA WACHUNGAJI.

Idara kwa kushirikiana na kamati ya Ujenzi wa nyumba za wachungaji ya jimbo iliyoundwa mwezi Julai 2021, imefanikiwa kuifikia mitaa yote na kufanya vikao na wajumbe wa baraza la mtaa sambamba na kukagua nyumba ya mchungaji kwa kila mtaa jambo lililoleta hamasa na ufanisi mkubwa katika mwendelezo wa ujenzi wa nyumba za wachungaji kwa kiasi kikubwa.

- Nyumba za wachungaji zilizojengwa na zinazotumika hadi sasa ni 28 na ambazo zinaendelea na ujenzi mpaka sasa ni nyumba 35 na ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi.
- Konference ilisaidia ukarabati kwa nyumba 12 za watumishi, zilizoko mitaani na zilizoko katika ofisi kuu ya conference.
- Ofisi ya jimbo imesaidia kutoa mabati ya kupaua nyumba za wachungaji katika mitaa 30 jambo ambalo limeongeza kasi ya ukamilishaji wa nyumba hizo.
- Ujenzi wa nyumba za wachungaji umeleta heshima kubwa kwa wachungaji na hata kwa kanisa kwa kuondoa adha ya kuishi katika nyumba za kupanga na kuleta ufanisi mkubwa kazini.



HALI YA UJENZI WA NYUMBA ZA WACHUNGAJI

| SN | HALI YA NYUMBA | MITAA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 1 | Hawana viwanja | Kirumba | 5 |
| | | Buzuruga | |
| | | Nazareth | |
| | | Kiseke | |
| | | Usagara | |
| 2 | Mipango ya Ununuzi wa Nyumba | Nyamanoro | 2 |
| | | Majengo Mapya | |
| 3 | Wana Kiwanja | Nyamhongolo | 10 |
| | | Isandula | |
| | | Pasiansi | |
| | | Butimba | |
| | | Malampaka | |
| | | Buswelu | |
| | | Sweya | |
| | | Misungwi | |
| | | Paji | |
| | | Matongo -Dutwa | |
| 4 | Msingi Umekamilika | Bulyashi | 2 |
| | | Makao | |
| 5 | Boma linajengwa | Mwanjoro | 9 |
| | | Mkolani | |
| | | Igombe | |
| | | Jiwekuu | |
| | | Buhongwa | |
| | | Sapiwi –Dutwa | |
| | | Kadashi –Nyambiti | |
| | | Mwankuba –Nyambiti | |
| | | Tindabiligi -Mwandoya | |
| 6 | Boma limekamilika | Somanda | 13 |
| | | Mwaukoli | |
| | | Kisesa | |
| | | Mahina | |
| | | Nyanguge | |
| | | Isamilo | |
| | | Malya | |
| | | Sola | |
| | | Kishili | |
| | | Nkoma | |
| | | Lamadi | |
| | | Dutwa | |
| | | Meatu - Majengo | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7 | Wapo hatua ya umaliziaji | Igelegele | |
| | | Shamaliwa | |
| | | Nyalikungu | |
| | | Mkula | |
| | | Nangale | |
| | | Salawe | |
| | | Wilayani | |
| | | Mahembe | |
| | | Mwagala | |
| | | Meatu | |
| | | Mwamapalala | |
| | | Sumve | |

Zifuatazo ni Nyumba ambazo tayari wachungaji wanaishi - 31

Nyegezi, Nyasaka, Nyakato, Igoma, Magu, Masanzakona, Nassa, Ngasamo, Old Maswa, Nkololo, Gasuma, Ntuzu, Kidinda, Lagangabilili, Sima, Laini, Migato, Mwandoya, Mshikamano, Ipililo, Buhungukila, Kwimba, Ndagalu, Ngulyati, Itilima, Nera, Paji, Maswa, Kanadi, Nyambiti, Dutwa.

## VIWANJA VYA MAKANISA NA VYA OFISI KUU YA CONFERENCE

Idara imefanikiwa kutoa mashauri mbalimbali juu ya utunzaji bora wa viwanja vya kanisa kupitia mtaalam (Estate Manager) kwa makanisa 357 na mashauri hayo yamepokelewa na kuanza utekelezaji ikiwa ni pamoja na namna bora ya kujenga na kuviendeleza viwanja hivyo.

Idara imefanikiwa kuratibu ulipaji wa kodi kwa viwanja vya jimbo.

Konferensi iliendelea kufidia viwanja vitatu yaani Ndala, Nhelegani na Mwananchi kilichoko jijini Mwanza.

Makanisa yamefidia jumla ya viwanja 72 kwa ajili ya ujenzi wa makanisa na nyumba za wachungaji mitaani.

Fensi na Wigo 27 zimewekwa katika viwanja vya makanisa.

Kodi ya ardhi kwenye kiwanja cha jimbo kilichopo Misungwi kilichotolewa na mshiriki imelipwa na hatua za kukiendeleza zinaendelea.

## UJENZI WA OFISI KUU YA CONFERENCE

Michoro ya ramani ya ofisi kuu ya confrensi imekamilishwa chini ya usimamizi wa kamati ya ujenzi wa ofisi ikiwemo na BOQ.

Hatua za kuweka kibao cha ujenzi (sticker) zinaendelea chini ya kamati ya ujenzi na ziko kwenye hatua nzuri.

Tayari kibali cha kuanza ujenzi kilishatolewa, hivyo hatua za ujenzi zimeanza.

## HUDUMA YA AMANA

### VITU VILIVYOTOLEWA NA WASHIRIKI NA WATU BINAFSI KWA UKARIMU.

- Washiriki na watu binafsi wameyanunulia na kuyapatia makanisa viwanja 44 ili kujenga nyumba za ibada.
- Waumini wametoa majengo 6 kwa ajili ya kuendeshea shughuli za ibada kwa makundi na makanisa.
- Washiriki na viongozi mbalimbali wametoa jumla ya mifuko ya cement 480 kusaidia ujenzi wa makanisa na nyumba za wachungaji.
- Jumla ya mabati 843 yalitolewa na waumini kusaidia kuezeka makanisa yaliyoingia katika uhitaji mkubwa.
- Jumla ya mbao za kuezekea 703 zimetolewa na waumini na wasio waumini kama sehemu ya ukarimu wao kusaidia kenchi za makanisa.
- Jumla ya Tshs. 23, 585,000.00 zimetolewa na washiriki na wadau wa maendeleo ya ujenzi kusaidia ujenzi wa makanisa.

## CHAMA CHA ATAPE

- Chama kimefanya mahubiri mbalimbali ndani ya jimbo kwa nyakati tofauti na mahali mbalimbali na kuanzisha makanisa ikiwa ni pamoja na kujenga majengo ya ibada kwa kushirikiana na makanisa mahalia jambo ambalo limeleta ufanisi mkubwa wa injili katika jimbo letu. Maeneo waliyohubiri ni pamoja na Ibulyu- Ngulyati, Mwagimagi - Magu, Kolomije-kwimba, Mwadila na Nkungulu – Maswa na baadhi ya maeneo bado kazi inaendelea wakati pengine kazi imekamilika.
- Chama kilitoa mifuko 300 kusaidia ujenzi wa Hospitali ya Pasiansi.
- Chama kilipangisha nyumba wachungaji walei wawili Sapiwi - Simiyu na Igombe – Mwanza.
- Chama kilinunua mkono wa msichana - Pendo mremavu wa ngozi aliyekatwa mkono.
- Chama kilitoa Tsh 11,000,000/= kuwezesha mahubiri ya Ushindi Hatimaye - Mabatini Mwanza.
- Wakati wa Jubilee ya Kanisa la Kirumba Chama kilitoa ushauri bure na sehemu ya dawa kwa wagonjwa 1785.
- Chama kiliratibu Jubilee ya miaka 25 ya ATAPE - TANZANIA hiliyofanyika Bariadi- Simiyu ambapo Pr. Emanuel Pelote na Pr. Joshua Njuguna walikuwa wanenaji wakuu.
- Chama kiliratibu Mkutano wa ATAPE taifa hapa jijini Mwanza April 2021, mkutano uliokuwa mbaraka kwa jimbo letu.
- Wamefanya Makongamano ya ATAPE mbalimbali likiwemo lililofanyika Bariadi kwa siku 4 na jumla ya watu 380 walihudhuria toka mkoa wa Simiyu liligharimu 3,800,000/= ambalo lilikuwa chachu ya kuongeza vipato na uaminifu katika matoleo kwa wanakongamano na washiriki waliohudhuria.
- Wametoa msaada kwa Mchungaji mmoja aliyeko masomoni sh. 260,000/=.

- Wameshiriki kambi ya Afya kila mwaka kwa kuchangia na kutuma madaktari kuwa sehemu ya wana timu (Kiteto 5,500,000)
- Wamefanikiwa kuandaa na kushiriki sabato ya mahusiano na waislamu (AMR) katika jiji la Mwanza mtaa wa Buhongwa na kuchangia ujenzi wa matundu ya choo cha Msikiti, Jumla ya sh. 2,500,000/= zilitumika katika tukio hilo. Jambo lililofungua mlango wa mahusiano hata sasa.
- Chama kimefanikiwa kuunga mkono shughuli za uinjilisti kwa ufanisi mkubwa hususani katika mahubiri yote ya NET Events.
- Chama kimefanikisha upatikanaji wa vyombo vya usafiri kwa wachungaji katika mitaa mbalimbali kama vile Mtaa wa Ipililo, Mtaa wa Mwandoya na Mtaa wa Maswa.



## MIPANGO YA IDARA YA UWAKILI 2022 - 2025

- Kukuza uhusiano wa waumini na Mungu wao kwa kiwango cha juu.
- Kukuza mtazamo chanya wa maendeleo binafsi na kanisa kwa ujumla (Image Change).
- Kuongeza idadi ya Waaminifu kanisani.
- Kufikia Malengo yaliyokusudiwa ya ukusanyaji wa zaka na sadaka kwa 100%.
- Kubadili taswira ya mitaa na makanisa hasa katika Matoleo, Miundombinu na Majengo. (Makanisa Bora, Ofisi, Maeneo ya Mikutano (Kumbi), Vyoo vizuri, Visima vya Ubatizo vya kisasa, Uzio, Nyumba za Wachungaji nzuri na kuhimiza Miradi mbalimbali makanisani).
- Kuendeleza ujenzi wa ofisi kuu ya Conference.
- Kuanza mpango wa Kujenga walau Nyumba 2 kwa kila mwaka kwa watumishi wa Ofisi ya Confrensi.
- Kuendelea kuratibu program ya kusaidia kupaua Makanisa yenye uhitaji mkubwa.
- Kukamilisha ujenzi wa nyumba za wachungaji kwa kila mtaa.
- Kuweka wakfu makanisa yasiyopungua 10 kwa kila mwaka.
- Kukamilisha upimaji wa viwanja vya ofisi na kuviendeleza kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji katika maeneo hayo. (Mwalogwabagole n.k)
- Kukuza, kupanua na kuendeleza Utume wa chama cha ATAPE.

## MBINU NA MIKAKATI 2022 - 2025

- Semina, mikutano na mafundisho mbalimbali katika kanda za Uwakili. (Team Work).
- Ziara na kutembelea makanisa, mitaa na washiriki katika miradi, ofisi na maeneo ya biashara. (Program Maalum ya Nitakwenda kufanya Wanafunzi kwa Zaka na Sadaka-Cheti cha Mungu Kwanza na Cheti cha Agano).
- Kutawanya Mifuko Maalum kwa kila mtaa kwa ajili ya Zaka na Sadaka ya mazao na pia kuhimiza kutenga zaka na sadaka ya vitu kama mifugo, viwanja n.k na kuhimiza viongozi wa kila kanisa kuendeleza mpango huu.
- Kutumia mitandao ya kijamii kufikisha jumbe mbalimbali za kuelimisha na kuhamasisha elimu ya Uwakili kwa kila juma. (Jumbe za Uwakili & Video Fupi/ Clips).
- Utoaji wa taarifa za matoleo kwa kila kanisa na mtaa kwa kutumia fomu maalum iliyoandaliwa.
- Kutumia kila karama, ujuzi na taaluma ndani ya kila kanisa ili kuleta mafanikio na ufanisi wa kazi ya Mungu.
- Kubadilishana wahudumu hasa Wachungaji na Walei ndani ya Confrensi wakati wa majuma ya uwakili kwa kila mwaka.
- Kutembelea kila mtaa kwa ushirikiano na Kamati ya Majengo kukagua hali ya miundombinu kwa kila kanisa na kutoa ushauri stahiki ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa makanisa ili yawekwe wakfu.
- Kudumisha program maalum ya kuwatembelea na kuwasiliana na wachungaji ili kuwatia moyo na kushauriana njia bora ya kupandisha matoleo hasa kwa mitaa isiyofanya vizuri.
- Kwa kushirikiana na ofisi ya mhazini kuendelea kutambua mitaa inayofanya vizuri kwenye matoleo kama matokeo ya juhudi, bidii na mipango bora ya mchungaji wa mtaa kwa kumpatia zawadi (Motivation & Appreciation Program).

*"Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu ..."*
*Malaki 3:10*

**2022 NITAKWENDA KUFANYA WANAFUNZI, KWA ZAKA NA SADAKA. BWANA AWE NANYI.**

# TAARIFA YA IDARA YA HUDUMA BINAFSI, SHULE SABATO NA UCHAPISHAJI.



**MCH. ONESMO DANIEL**

MKURUGENZI WA IDARA
YA HUDUMA BINAFSI, SHULE
SABATO NA UCHAPISHAJI.



MKUTANO MKUU WA NANE WA SNC (SESSION)
SEPTEMBA 22, 2022.

# IDARA YA HUDUMA BINAFSI.

## UTANGULIZI.

Nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha South Nyanza Conference kusimamia Agizo lake la **ENENDENI ULIMWENGUNI POTE**;

"**Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari**" Mathayo 28:19-20.

"**Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe.**" Marko 16:15.

Ndugu wajumbe wote South Nyanza Konference miito ya kutoka juu kuhusu kazi ya uongoaji roho na mikakati ya ndani kwa ndani, Kimtaa, kikanisa ya kupeleka injili katika maeneo husika.

## UTUME KWANZA - NI WAKATI WA MAVUNO.

Mkakati huu ulihusisha washiriki wote ulikuwa ukiitwa TMI (Total Member Involvement) kama ilivyoelekezwa, kila idara na kila muumini tukaelekeza katika maeneo matatu.

- Kumfikia Mungu (Reach up to God).
- Kuwafikia washiriki kanisani (Reach in with God).
- Kuwafikia wengine katika jamii (Reach out with God)

## UTENDAJI KAZI WA IDARA HII ULIELEKEZWA.

- Kuwa na semina mbalimbali kikanda/kimkoa.
- Kuwa na mahubiri makanisani yakisimamiwa na wachungaji na walei.
- Kukazia ubatizo makanisani.

Semina ziliendeshwa kikanda na kimkoa, lengo ni kuwafikia walengwa karibu, ili utendaji uwe mzuri. Maeneo Makuu ya Semina yalikuwa;

- Nyanza Sekondari - Walei wote walikusanyika hapo na kupewa vyeti na vitambulisho.
- Pasiansi kanisani- Wakati wa mahubiri ya Pr Mark Finley Walei walipewa semina.
- Buswelu kanisani na Sima (Bariadi) walei walipewa Semina (2021).
- Nyegezi kanisani na Sima (Bariadi) semina ziliendeshwa vizuri.
- Katika semina zote hizi wachungaji wa mitaa walihusishwa.
- Waalimu wa semina walikuwa viongozi wa Union na Conference.



*Picha 1: Walei wakiwa katika semina.*

.

## MATUKIO MAKUU YA UONGOAJI ROHO.

| MWAKA | MAHUBIRI | MHUBIRI | MAHALI | UBATIZO |
|---|---|---|---|---|
| FEB, 2017 | USHINDI HATIMAYE | PR. DAVID MBAGA | MABATINI MWANZA | 9,407 |
| MEI, 2018 | UFUNUO WA MATUMAINI | PR. MARK FINLEY | CCM KIRUMBA MWANZA | 19,227 |
| MEI, 2019 | TUMEKARIBIA NYUMBANI | PR KENANI MWAMSOMOLA | MBEYA | 603 |
| SEP ,2019 | NYUMBANI HATIMAYE | PR. PAUL SEMBA | KINYEREZI DAR-ES SALAAM | 1,962 |
| FEB, 2020 | MUNGU KWANZA | PR. CARLTON BYRD. | CHATO BUKOBA | 398 |
| MEI, 2020 | UZOEFU WA NGUVU YA MUNGU | PR. MGANDA BARAKA | DODOMA | 418 |
| SEP, 2020 | TUMAINI LITOKALO JUU | PR, NZUNGU LUCAS | HEDARU MANYARA | 3,250 |
| MEI, 2021 | SHANGWE KATIKA NJIA YAKE | PR. MARK W. MALEKANA | KIZOTA DODOMA | 6,008 |
| SEP, 2021 | AMANI ITOKAYO JUU | PR. GODWIN LEKUNDAYO | NYAMONGO TARIME | 11,880 |
| JUNI, 2022 | UKWELI UNAOKUWEKA HURU | PR. DAVID MAKOYE | KARATU, MANYARA | 11,955 |
| **JUMLA** | | | | **65,108** |

## UBATIZO ULIVYOFANYIKA KUTOKA 2016 - ROBO YA 1 2022

| MWAKA | ROBO 1 | ROBO II | ROBO III | ROBO IV | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 2186 | 3757 | 9809 | 4141 | 19893 |
| 2017 | 9407 | 0 | 24110 | 3811 | 41759 |
| 2018 | 6946 | 11475 | 6800 | 5920 | 31141 |
| 2019 | 7824 | 8216 | 10859 | 2644 | 29543 |
| 2020 | 3188 | 1331 | 6411 | 2836 | 13766 |
| 2021 | 1095 | 5889 | 5101 | 3356 | 15441 |
| 2022 | 2209 | - | - | - | 2209 |
| JUMLA KUU | | | | | 153,752 |

## ULINGANIFU WA UBATIZO KWA VIPINDI VIWILI (2011-2015 & 2016-2022).




*Picha 2: Ulinganifu wa ubatizo kwa vipindi vya 2011-2015 na 2016-2022.*



*Picha 3: Muumini mpya akikaribishwa katika familia ya Kristo kwa njia ya ubatizo.*

## SADAKA YA MAKAMBI TOKA 2016 -2021.

| MWAKA | MATOLEO |
|---|---|
| 2016 | 183,210,371.04 |
| 2017 | 196,493,191.40 |
| 2018 | 284,787,527.33 |
| 2019 | 198,968,672.00 |
| 2020 | 270,629,567.65 |
| 2021 | 321,308,598.01 |
| **JUMLA KUU** | **1,455,397,927.43** |

## MATOKEO YA KAZI HII.

Mitaa kuongezeka toka **64 Mwaka 2016** mpaka **91 Mwaka 2020** conference ilipogawanywa na South Nyanza ikabaki na **mitaa 54**. Kutoka **Mitaa 54 mwaka 2020** mpaka mitaa **78 mwaka 2022**. Conference imeongezeka tena.

Ndugu wajumbe ambao ndani yenu mlisukuma kazi hii Bwana awabariki, na wapelekeeni salam walei wenzetu na makanisa yote yaliyofanya kazi hii.

## CHANGAMOTO KATIKA KUONGOA ROHO 2016 – 2022.

- Ugonjwa wa Korona (Covid 19) hata hivyo Bwana aliifanya kazi yake mwenyewe.
- Vibali; Sehemu zingine zilipata shida kulipia gharama kubwa hasa vituo vya mjini.
- Malezi: Hii ni changamoto ambayo baadhi ya makanisa walishindwa kufanya mahubiri, pia hofu ya kupoteza watu baada ya ubatizo.

## ADVENTIST MUSLIM RELATIONS (AMR).

Maana yake ni huduma ya mahusiano baina ya Waadventista Wasabato na jamii ya Waislam. Huduma hii imeweza kupokelewa vizuri sana katika jiji la Mwanza. Kirumba ndiyo mtaa uliolipokea vizuri sana.

Waadventista Wasabato wa jiji la Mwanza wanashiriki chakula cha pamoja na Waislam, tunamshukuru Mungu kwa kufanikisha jambo hili.

Semina zimefanyika sehemu mbalimbali, Kirumba, Buswelu, Kwimba, Igombe, bado tunaendelea.

Viongozi wa General Conference AMR Division, Union na Conference yetu wameongoza na kusimamia semina za AMR.

### MAFANIKIO.

- Washiriki wa AMR wana uwezo wa kuimba nyimbo kwa kiarabu. Nk.
- Miongozo ipo kwa sasa ya kuelekeza na kuifahamu AMR.
- Mitaa, makanisa ya jiji la Mwanza wameshaielewa huduma hii.




*Picha 4: Washiriki wa huduma ya AMR wakiwasilisha wimbo.*

## KITENGO CHA GLOBAL MISSION.

Tunamshukuru Mungu tumefanikiwa kuendesha mikutano na semina kwa Walei (Pioneers) ili kuwa tayari kutumwa katika maeneo mapya na kufungua kazi. Semina za walei zilifanyika katika Conference, Kanda na mitaa. Wakufunzi wa semina hizi walitokea ECD, NTUC, na hapa Conference.

- Miradi iliyofadhiliwa na ECD 4: Kanisa la Ilemela-Pasiansi, Mwakuba-Kwimba, Mwawaza- Shinyanga na Mwanjolo.
- Makanisa yaliyosaidiwa na ECD kutimiza ahadi ya Mwenyekiti wa Division Pr. Ruguri ni Kirumba, Geita na Betheli.
- Walei (Pioneers) 126 wamepata semina mbalimbali na waliingia maeneo mapya sehemu mbalimbali za Conference na kufanya kazi.
- Baadhi ya makanisa yaliyopokea Mabati toka kitengo cha Global Mission: Kanisa kubwa la kijijini Kagunga - Mtaa wa Sengerema lililodumu zaidi ya miaka 10 kuezekwa hatimaye kwa kushirikiana na Conference, Kanisa la Kijiweni Mtaa wa Sengerema TX – Mwanza na Ijinga-Magu.
- Kitengo cha Global Mission kupitia rafiki wa Mratibu wa Kitengo hicho kilipata ufadhili wa baiskeli 29, pikipiki 15 SNC walipewa wakuu wa vituo vya Global na baadhi ya Wachungaji wa mitaa.
- Biblia 300 zilitolewa, Vitabu Vya Roho ya Unabi 200 viligawiwa na miongozo kwa walezi (Wainjilisti Walei) 70 walipewa; kwa ujumla vyote viligharimu Tsh. 24,200,000.
- Mitaa kama Matokeo ya Global Mission: Mahembe, Mwanjolo, Paji, Majengo Mapya Nyegezi, Kituo cha Gobal Habiya na Ngasamo.



*Picha 5: Makanisa yaliyokamilishwa katika mradi wa Global Missioni.*



*Picha 6: Moja ya pikipiki zilizokabidhiwa kwa wakuu wa vituo vya global mission na wachungaji wa mitaa.*

# IDARA YA SHULE SABATO.

Napenda kumshukuru Mungu kwa kusaidia idara hii, maana hii ndio MOYO WA KANISA.

Lakini pia sitasahau uongozi mzima wa Union yetu kuweka mkono wa ushirikiano katika Konference yetu, na pia sitasahau kuwashukuru viongozi wa Ufunuo (UPH). UFUNUO PUBLISHING HOUSE kuleta miongozo kwa wakati tofauti na vipindi vilivyopita.

## MIPANGO YA IDARA.

Malengo ya shule sabato kanisani ni:-

1. Kujifunza neno la Mungu.
2. Ushirika.
3. Uinjilisti.
4. Utume Ulimwenguni.

Ili kufanikisha malengo haya tumekuwa na mipango ifuatayo;

- Kuhakikisha kuwa mwongozo wa kujifunza Biblia unapatikana kwa wakati.
- Kuendesha semina za shule sabato – kikanda (Kimkoa).
- Kuendesha semina za waalimu wa shule sabato.
- Kuhimiza uinjilisti kupitia madarasa ya shule sabato



*Picha 7: Semina ya Shule ya Sabato.*

## UTEKELEZAJI.

Namshukuru Mungu sana ile hali ya zamani ya kukosa lesoni (au mwongozo ya kujifunza Biblia) au kuchelewa kuzipata sasa haipo. Miongozo hiyo tumeipata kwa wakati.

Ufunuo Publishing House, wameamua kusaidia conference yetu kutumia ofisi zetu kuleta miongozo hapo Bariadi kwenye ofisi yetu ya uchapaji mkoa wa simiyu unapata miongozo kwa wakati. Hapa Mwanza duka la ufunuo na mawakala wachache wanasaidia kuzileta lesoni.

Semina za shule sabato zimeendeshwa vizuri kuanzia 2020 – 2022 na tunapata waalimu wa madarasa ya shule sabato wenye uzoefu.

Mwaka 2020 wafuatao walipelekwa na mitaa yao kupata elimu ya kufundisha lesoni au miongozo ya kujifunza Biblia huko Kahama; **Lita Katoya (Nyegezi)**, **Rebeka Maduhu (Ntuzu) na Ndugu Burilo kutoka Nyashimo -Nassa**. Pamoja nao, baadhi ya wachungaji pia walihudhuria mafunzo hayo. Wachungaji hao ni; Pr. Sengiyumva Siniga (Nyamanoro), Pr. Paschal Shingashinga (Mwagala) na Pr. John Dotto (Nyanguge).

Hawa wamekuwa waalimu wetu wazuri. Union yetu NTUC imewatumia sana katika semina mbalimbali kama vile Pasiansi na Ntuzu.

Ninapenda kuwaambia mkutano huu tuna waalimu ambao wamekuwa na uzoefu wa kufundisha waalimu wengine wa shule sabato; waiteni makanisa ni mwema mtabarikiwa,

Kupitia programu hii tunao walimu wa shule sabato wenye mafunzo 388, Mkoa wa mwanza 179 na Mkoa wa Simiyu 209. Hawa watu ni akiba ya Konference kwa miaka yote.

## USOMAJI WA LESONI.

Miaka kadhaa iliyopita lesoni zilikuwa shida kidogo kupatikana, hata hivyo tulikuwa tunatumia mawakala hapa na pale, kwa sasa Ufunuo Publishing House wamesogeza huduma ya upatikanaji wa lesoni jimboni kwetu kupitia maeneo yafuatayo;

1. Simiyu kwenye ofisi ya uchapaji.
2. Mabatini ofisi ya UPH
3. Mawakala wachache

Baada ya kugawanyika SNC imepata miongozo ifuatayo ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo chini:-

**Taarifa ya Mauzo ya Miongozo ya Shule Sabato 2020 – 2022.**

| S/N | AINA ZA MIONGOZO NA UTUME | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | WATU WAZIMA | 88,143 |
| 2. | VIJANA (15-18) | 22,980 |
| 3. | WATOTO | 60,900 |
| 4. | UTUME (WAZIMA) | 4,874 |
| 5. | UTUME (WATOTO) | 1,275 |

# IDARA YA UCHAPISHAJI

## UTANGULIZI.

Idara ya uchapishaji ina majukumu makubwa ya kuwapelekea watu vitabu ili wajifunze na kuokolewa. Jambo jingine ni kuwaletea washiriki vitabu wavisome na kuimarika kiroho, wanahimizwa kusoma Biblia, vitabu vya roho ya unabii, vitabu vya familia na vitabu vya mwaka.

Ndugu Mwenyekiti wa Union na Viongozi wote wa Union yetu ya kasikazini mwa Tanzania (NTUC), South Nyanza Conference, wajumbe wote wa mkutano mkuu wa Conference, Bwana apewe sifa.

Napenda kumshukuru Mungu kwa Mema. Idara hii ya uchapishaji, kwa kweli tumesafiri salama, japo changamoto zilijitokeza kama; Kuadimika kwa vitabu mwaka 2018-2019 na kupatwa na wimbi la Corona (COVID 19). Hata hivyo wainjilisti wa vitabu walikuwa wakienda kila ofisi japo kulikuwa na Corona.

## MALENGO YALIYOKUWEPO.

- Kuongeza wainjilisti wa vitabu.
- Kuwa na makambi ya wainjilisti wa vitabu
- Kuongeza idadi ya kanda.
- Kuongeza maduka.
- Kumbukumbu za wainjilisti wa vitabu.
- Kuwa na mafunzo ya LMS.

## MATUKIO YALIYO TENDEKA

- Wainjilisti wa vitabu walihudhuria semina iliyofanyika Baraton Desemba 2018.
- Semina za LMS zilizoendeshwa na uongozi wetu wa Union Conference (NTUC)
    - Maswa (Ndani ya conference).
    - Nzega (Nje ya conference).
    - Tarime (Nje ya conference)
- Kuwa na makambi ya wainjilisti wa vitabu
    - Maswa – Pr. David M. Makoye, Katibu Mkuu wa Northern Tanzania Union Conference akiwa mgeni rasmi.
    - Bariadi – Pr. George Ojwang', Mwenyekiti Mara Conference akiwa mgeni rasmi.
- Ujenzi wa ofisi Kanda ya Bariadi ya nguvu Idara ya Uchapishaji iliyowekwa jiwe la msingi na Mwenyekiti wetu wa Union Conference Dr. Pr Lekundayo. Nipende kusema kuwa viongozi wetu wa Union Conference waliweka mkono kwa kufanikisha ukamilishaji wa ofisi hiyo. Vitabu vimewekwa hapo vingi na hata ofisi yetu ya Union Publisher House imeleta pale machapisho mbali mbali.
- Semina zilizo endeshwa kwa kila kanda zikiendeshwa na PD, APD,na APLS.



*Picha 8: Uzinduzi wa kitabu cha Tumaini Kuu.*



*Picha 9: Ofisi ya Uchapishaji Bariadi - Simiyu.*

## KANDA ZA KAZI.

South Nyanza Conference ina kanda saba (7) ambazo ziko chini ya usimamizi wa APD na APLS nazo ni:

1. Maswa – Msimamizi ni Faustine Magashi (APD).
2. Bariadi – Msimamizi ni Jenipher Joseph Gilihe (APD).
3. Magu – Msimamizi ni Zebida Kajeli (APD).
4. Misungwi – Msimamizi ni Prisca Ndege (APL).
5. Mabatini – Msimamizi ni Yohana Kishamuri (APL).
6. Nyakato – Msimamizi ni Asante Maherere (APL).
7. Pasiansi – Msimamizi ni Lucas Daudi (APL).

## MADUKA YA VITABU.

Bwana ametusaidia kuwa na maduka sehemu mbalimbali ili kusogeza huduma kwa Wainjilisti wa vitabu na washiriki pia.

| | DUKA | MSIMAMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Pasiansi | Jeremiah Ludovick |
| 2 | Mabatini | Amos Isaya |
| 3 | Buzuruga | Rebeka Joseph Mpina |
| 4 | Kisesa | Naomi Phares |
| 5 | Shamaliwa | Mecktilida Mitundwa |
| 6 | Buhongwa | Rehema Athman |
| 7 | Buswelu | Adamu Mukami |
| 8 | Misungwi | David Magori |
| 9 | Magu | Anna Nyizigiye |
| 10 | Nyambiti | Daniel James Bukekere |
| 11 | Nassa | Edda Bwengi |
| 12 | Lamadi | Milka Wanna |
| 13 | Maswa | John Mahona Musesa |
| 14 | Malampaka | Rebeka Simon Mapesa |
| 15 | Mwandoya | Musa Samwel Ngoloba |
| 16 | Meatu | Agnes Deus Jiganga |
| 17 | Bariadi | Esther Kalimelo |
| 18 | Lagangabilili | Philemon Tindigwe Shauri |
| 19 | Dutwa | Yona Maduhu Mudodo |



*Picha 10: Muinjilisti wa Vitabu akiwa katika meza yake ya vitabu.*

# TAKWIMU ZA KAZI 2016-2022

## MWAKA 2016.

| KANDA | IDADI YA VITABU | THAMANI YA FEDHA | UBATIZO |
|---|---|---|---|
| MAGU | 7,023 | 67,140,632 | 8 |
| BARIADI | 7,624 | 78,606,587 | 49 |
| MASWA | 9,157 | 101,512,263 | 57 |
| MWANZA | 1,8150 | 242,219,153 | 60 |
| **JUMLA** | **4,1954** | **489,478,635** | **174** |

## MWAKA 2017

| KANDA | IDADI YA VITABU | THAMANI YA FEDHA | UBATIZO |
|---|---|---|---|
| MAGU | 5,799 | 61,294,179 | 160 |
| BARIADI | 3,965 | 44,221,210 | 131 |
| MASWA | 6,884 | 85,619,144 | 422 |
| MWANZA | 16,567 | 155,944,768 | 237 |
| **JUMLA** | **3,3215** | **347,079,301** | **950** |

## MWAKA 2018

| KANDA | IDADI YA VITABU | THAMANI YA FEDHA | UBATIZO |
|---|---|---|---|
| MAGU | 7,927 | 63,416,205 | 27 |
| BARIADI | 9,863 | 79,721,188 | 39 |
| MASWA | 7,652 | 51,211,896 | 67 |
| MISUNGWI | 3,664 | 13,348,702 | 11 |
| MABATINI | 10,223 | 92,385,675 | 32 |
| PASIANSI | 8,893 | 85,424,247 | 40 |
| NYAKATO | 9,992 | 90,368,065 | 36 |
| **JUMLA** | **58,241** | **475,875,978** | **252** |

## MWAKA  2019

| KANDA | IDADI YA VITABU | THAMANI YA FEDHA | UBATIZO |
|---|---|---|---|
| MAGU | 4,372 | 35,020,852 | - |
| BARIADI | 6,329 | 62,163,306 | 52 |
| MASWA | 3,669 | 37,287,673 | 18 |
| MISUNGWI | 1,649 | 11,153,857 | - |
| MABATINI | 5,385 | 71,111,969 | 41 |
| PASIANSI | 6,015 | 102,107,514 | 22 |
| NYAKATO | 5,076 | 61,487,420 | 50 |
| **JUMLA** | **32,495** | **380,332,591** | **183** |

MWAKA 2020

| KANDA | IDADI YA VITABU | THAMANI YA FEDHA | UBATIZO |
|---|---|---|---|
| MAGU | 6,362 | 42,773,397 | 107 |
| BARIADI | 14,915 | 151,331,889 | 81 |
| MASWA | 7,980 | 58,510,011 | 165 |
| MISUNGWI | 1,644 | 19,375,500 | 3 |
| MABATINI | 7,941 | 92,027,246 | 10 |
| PASIANSI | 14,846 | 144,446,575 | 159 |
| NYAKATO | 8,340 | 88,716,646 | - |
| **JUMLA** | **32,771** | **597,181,264** | **5,256** |

MWAKA 2021.

| KANDA | IDADI YA VITABU | THAMANI YA FEDHA | UBATIZO |
|---|---|---|---|
| MAGU | 7,646 | 65,539,243 | 106 |
| BARIADI | 8,598 | 90,591,158 | 123 |
| MASWA | 4,107 | 45169576 | 211 |
| MISUNGWI | 2,449 | 20,165,040 | 366 |
| MABATINI | 6,827 | 83,172,272 | 218 |
| PASIANSI | 6,869 | 83,498,073 | 58 |
| NYAKATO | 5,509 | 69,011,549 | 164 |
| **JUMLA** | **42,005** | **456,146,911** | **1,344** |

## ULINGANIFU WA KAZI VIPINDI VIWILI

| | 2011-2012 | 2016-2021 | ONGEZEKO |
|---|---|---|---|
| MASAA | 1,225,845 | 1,316,782 | 90,037 |
| IDADI YA VITABU | 309,263 | 240,654 | 58,609 |
| MAUZO | 2,493,940,246 | 2,746,094,680 | 252,154,434 |
| UBATIZO | 40765 | 3428 | (-1337) |

## VIONGOZI WA UCHAPISHAJI SNC.

| | 2011-2015 | 2016-2022 | ONGEZEKO |
|---|---|---|---|
| PDD | 1 | 1 | |
| APDD | 4 | 3 | |
| HHES MANAGER | | | |
| SUB ABC | 15 | 19 | 4 |
| APL | | 4 | 4 |

## ULINGANIFU WA WAINJILISTI WA VITABU KWA MIHULA MIWILI.

| DARAJA | 2011-2015 PAMOJA NA NGBF | 2016-2022 SNC PEKEE |
|---|---|---|
| IDENTIFICATION | 71 | 291 |
| LICENCE | 71 | 28 |
| CREDENTIAR | 57 | 23 |
| PART TIME | 17 | 49 |

## WAINJILISTI WALIOSTAAFU 2016 - 2022.

1. Neema Kwitukula Manga.
2. Penina Midala Nhabalyaga.
3. Eunice John.
4. Modesta Nsongoma.
5. Marco Nsongoma.
6. Magreth Mtingwa.
7. Ezekiel Busalu Sanagu.
8. Gaudensia Basime.
9. Peruth Kalebu Masalu.
10. Magreth Joseph Malaba.
11. Pendo Mashashi Maige.
12. Asia M. Mtobesya.
13. Joyce Mwita Wanzagi.
14. Asteria Albert Mahande.

## SHUKRANI.

Shukrani zetu ziwaendee maofisa wote wa Northern Tanzania Union Conference na Mkurugenzi wa Idara ya Uchapishaji, walifanya juhudi ya kupata vitabu, pamoja na hili tunawashukuru maofisa wa South Nyanza Conference kuwa pamoja nasi na kututia moyo wainjilisti wa vitabu. Wainjilisti wa vitabu walipitia katika wimbi la ugonjwa wa Corona (COVID – 19), kwa uweza wa Mungu walisonga mbele; ndiyo maana vitabu vinaeleza kuwa huko tunakoelekea itabaki Idara ya vitabu ikifanyakazi, huduma zingine zikikiwa hazifanyi kazi.

Mbarikiwe wana Mkutano.

# TAARIFA YA IDARA YA HUDUMA ZA AFYA NA KIASI. (2016 – JUNE 2022).



**DR. BARAKA MAGINGA**
MKURUGENZI WA HUDUMA ZA AFYA NA KIASI.





MKUTANO MKUU WA NANE WA SNC (SESSION)
SEPTEMBA 22, 2022.

## UTANGULIZI

Idara ya Huduma za Afya na Kiasi katika South Nyanza Conference, tuko mstari wa mbele kuhakikisha utume wa kanisa la waadventista wa sabato unasimamiwa kwa kutoa maelekezo, mbinu na njia bora za kuhakikisha vilele vya afya bora vinafikiwa. Kwa kuongozwa na biblia, roho ya unabii na mafundisho ya afya yaliyothibitishwa kitaalam, idara hii imefikisha ujumbe huu kwa kanisa na jamii kwa ujumla na kusaidia mwanadamu ambaye angeangamia kwa kutokujua ukweli wa maandiko na kubadili mtindo wake wa maisha.

Kabla ya jimbo la South Nyanza kugawanywa kwa kuzaa jimbo la NGBF, idara ya huduma za afya na kiasi imehusika kusimamia maeneo ya mikoa ya Geita, Shinyanga, Simiyu na Mwanza. Tumekuwa na Zahanati ya Kasamwa, Bupandagila na hospitali ya SDA Pasiansi bila kusahau hospitali ambayo bado iko katika kuendelea kujengwa katika mkoa wa Geita iitwayo Magogo Hospital. Hivyo taarifa hii itagusa maeneo zaidi ya jimbo letu la SNC. Kwa sasa katika conferensi yetu tuna zahanati ya Bupandagila SDA na hospitali moja ijulikanayo kama SDA Pasiansi Hospital iliyopandishwa hadhi mwezi Machi mwaka 2020 kutoka kituo cha afya kuwa hospitali ngazi ya mkoa.

Taarifa hii imegawanyika katika maeneo yafuatayo;

A. Maendeleo katika huduma za tiba.
B. Uinjilisti.
C. Mfanikio katika huduma ya Afya na Kiasi.
D. Mahusiano ya kijamii, kitaifa na kimataifa
E. Mipango kufikia njozi 2025+

## MAENDELEO KATIKA HUDUMA ZA TIBA.

Katika eneo hili tunaangalia zaidi katika maendeleo ya vituo vyote vinavyomilikiwa na kanisa katika SNC. Kwa muda wote tangu mwaka 2016, idara ya huduma za afya imehakikisha kuwa kunakuwa na maendeleo chanya katika vituo vyote vya afya vilivyo chini ya jimbo la South nyanza Conference. Katika upande wa tiba tumehakikisha kuwa vituo vyote vinapanda hadhi katika miundombinu na pia katika rasilimali watu na taaluma kwa ujumla. Afya kama mkono wa kuume wa injili unathibitika zaidi pale ambapo kila mwanataaluma wa afya aliposhirikishwa katika huduma hii katika kanisa mahalia au pale mgonjwa anapopatiwa huduma katika vituo vyetu vya afya.

- Hapo awali zahanati ya Kasamwa ilikuwa ikitegemea kituo cha afya cha SDA Pasiansi kwa kila jambo, hivyo kuletea zahanati hiyo kushindwa kusimamia malengo kwa sababu ya kuwa tegemezi. Mnamo mwaka 2017 mwanzoni, mpango wa makusudi wa kuifanya Zahanati ya Kasamwa kujitegemea ulifanikiwa, kwa kuwa na uongozi wa kituo husika na kufanya maamuzi yao wenyewe kwa kujitegemea.
- Sambamba na hilo ili kuhakikisha zahanati inakuwa na taswila mpya ukarabari wa majengo ulifanyika ili kuleta taswira nzuri kwa wagonjwa wanaopata huduma katika zahanati hiyo. Vilevile gari zuri la wagonjwa limenunuliwa kwa ajili kusafirisha wagonjwa pale dharula zinapojitokeza. Katika mwezi January 2019, zahanati ya Kasamwa ilianza ujenzi wa majengo mapya mengine ili kuelekea katika hatua za upandishwaji hadhi kuwa kituo cha afya. Katika kufanikiwa kutenga zahanati hii, kumekuwa na mchango mkubwa sana katika kupandisha hadhi utengwaji wa field ya Geita Ukanda wa Dhahabu.

- Mkoa wa Geita ni miongoni mwa mikoa inayokuwa kwa haraka kwa sababu ya shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika mkoa huo. Kwa kutambua hitaji hilo na ongezeko la wakazi mkoani Geita, ikagundulika kuwa bado tunapaswa kuunyoosha mkono wa kuume kwa kuanzisha ujenzi wa hospitali. Kwa kushirikiana na serikali chini ya uongozi wa mkuu wa mkoa wa Geita kipindi hicho Mhe. Mhandisi. Robert Gabriel Luhumbi, kuamua kujenga majengo ya hospitali katika eneo la Magogo ambayo bado iko katika hatua za kumalizia ujenzi huo hadi sasa.
- SDA Pasiansi Hospital inavyojulikana sasa, ilikuwa ni kituo cha afya tangu mwaka 2006. Mpaka mwaka 2016 kulikuwa kunatumika majengo madogo ya awali kwa kutoa huduma kwa wagonjwa waliofika hapo kituoni. Jengo linalotumika sasa kwa shughuli za hospitali, lilikuwa limejengwa lakini bado lilikuwa halijamalizika. Hatua za kuanza kukamilisha jengo la hospitali zilianza kwa uharaka ili kupanua huduma na kupandisha hadhi toka kituo cha afya kuwa hospitali. Maeneo yaliyofanyiwa kazi katika kukamilisha jengo ni pamoja na kuweka madirisha yote ya nje, kukamilisha chumba cha upasuaji, kuweka miundombinu ya umeme, mtandao na maji.
- Katika kukamilisha baadhi ya maeneo ya jengo la hospitali, kumewezesha upanuzi wa huduma hadi huduma za kibingwa ambazo zimekuwa ni msaada mkubwa sana kwa wakazi wengi wa kanda ya ziwa. Kwa kupanuka kwa huduma zetu kumetupatia uwezo wa kupandishwa hadhi na kuwa hospitali ngazi ya wilaya. Kwa kugundua kuwa hospitali yetu iko katika eneo la ushindani wa huduma, tumefanya maboresho zaidi katika kuhakikisha kuna gari la wagonjwa (Ambulance) pia kuwepo umeme wa uhakika kwa kununua jenereta yenye uwezo wa kuendesha shughuli zote za hospitali.

- Ujenzi wa hospitali katika gorofa ya chini na ya kwanza zimekamilika kwa 100% na ziko katika matumizi. Gorofa ya pili imekamilika kwa 90%, ya tatu kwa asilimia 60% ya nne kwa asilimia 50% na ya tano bado haijaanza kufanyiwa finishing. Na sasa tumeanza kupokea wataalamu mbalimbali kutoka nchi za Ulaya ambao wamevutiwa sana na hospitali yetu. Hii inafungua milango kuitambulisha hospitali yetu katika mataifa ya nchi zilizoendelea. Vilevile huduma za macho, meno, mionzi na upasuaji maalum zinaendelea tangu hospitali yetu kuwa na hadhi ya ngazi ya wilaya.



## UINJILISTI

Lengo kuu la kuwepo huduma za afya ni kuhakikisha utume wetu tulioitiwa unafanikiwa kwa viwango vikubwa. Kama sehemu ya mkono wa kuume wa injili tumefanikiwa kuwa sehemu ya uongoaji wa roho kupitia huduma zetu katika jamii ya wakazi wa dunia.

- Mnano mwaka 2017, timu ya wataalamu wa afya kutoka katika Conference yetu, kwa kushirikiana na timu ya wataalam wa afya toka Korea ya kusini tulifanya mahubiri ya wiki mbili katika eneo la Minjingu mkoani Manyara. Kwa habari zinazotolewa na waadventist wenyeji wa umasaini ni kwamba, inaweza kuchukua miaka mitano ya injili ili kuweza kubatiza mmasai mmoja. Lakini kwa neema ya Mungu, watu 25 walibatizwa katika siku ya mwisho ya kufunga mahubiri hayo ya Minjingu. Habari njema ni kwamba mpaka sasa kanisa linaendelea kukua kwa idadi kubwa zaidi ya waumini.



- Katika program ya TMI, tumeweza kuhudumia kambi kadha wa kadha za afya ikiwemo kambi ya Buswelu na iliyofanyika katika jengo la hospitali ambapo wagonjwa 654 walifanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu kwa magonjwa waliokutwa nayo. Katika kipindi hicho tulifanikiwa pia kukusanya damu kiwango cha unit 720.
- Katika mahubiri ya USHINDI HATIMAYE yaliyorushwa kutoka kanisa la Mabatini jijini Mwanza, wataalamu wa afya walihudumia watu wapatao 2015 na katika hao watu 1769 walipatiwa matibabu bila kulipia gharama yoyote.
- Tumeweza kushiriki kikamilifu katika mahubiri ya TMI CCM Kirumba kwa kutoa huduma za ushauri, kupima na matibabu kwa baadhi ya watu walioweza kuhuzulia katika mabanda ya kutolea huduma za afya. Jumla ya watu walifika katika mabanda yetu na kupata huduma ni watu 9610. Vilevile tumeweza kuhudumia watu wapatao 21, ambao walikuwa ni wawezeshaji wa mkutano huo, pale ambapo walipatwa na matatizo ya kiafya. Hii ikaweka jumla ya watu 9631 sawa na asilimia 96% na lengo lilikuwa ni kuhudumia watu 10,000.
- Mwishoni mwa mwaka 2021 Idara ya afya na kiasi kwa kushirikiana na wataalam wa jiji la Mwanza na ATAPE tumefanya mahuburi ya hadhara na kutoa huduma za afya katika kijiji cha Bugabu na Lagangabilili mkoani Simiyu. Katika mahubiri hayo watu zaidi ya 551 wamebatizwa huko Lagangabilili na watu 100 wamebatizwa hapo Bugabu Magu. Katika eneo la Bugabu jengo kubwa la kanisa limekamilika na tayari waumini wapya wanamwabudu Mungu katika kanisa hilo.

## MAFANIKIO KATIKA HUDUMA YA AFYA NA KIASI.

Katika kipindi chote, idara ya afya imeendelea kutoa elimu kwa waumini na wasio waumini kwa njia ya semina na mahubiri ndani na nje ya conference. Ili kuweka msisitizo tulianza kwa kuwatia moyo viongozi wa taasisi zetu ikiwemo vituo vya afya kwa kuwasisitiza kusoma biblia kwa mpango. Kwa tathmini ni kwamba asilimia 90 wa viongozi wa taasisi waliweza kufikia malengo kwa asilimia 100.

Katika mwaka wa jubilee kwa kanisa la Kirumba, na katika mahubiri yaliyofanyika Mwamagigisi, na katika mahubiri ya Masumbwe, wataalam wa afya waliweza kuhudumia watu wapatao 4094. Katika watu hao waliopata huduma na shauri wa kitabibu, watu 411 walipatiwa dawa kwa kutibu magonjwa yaliyokuwa yakiwasibu, watu 51 waliokuwa na uoni dhaifu walipatiwa miwani, watu 36 walifanyiwa upasuaji mkubwa na jumla za unit 652 za damu zilikusanywa kupitia huduma katika maeneo hayo. Katika huduma hizo zote, watu wapatao 296 walimpokea Yesu kwa njia ya ubatizo.

Kwa kushirikiana na Idaya ya Afya ngazi ya Union Conference, South Nyanza Conference tumeweza kufanikisha kongamano la afya na vijana lililofanyika katika viwanya vya kanisa la Pasiansi, ambapo wataalamu wa afya 566 waliuzulia katika kongamano hilo na kati ya hao watu 429 ni wajumbe waliotumwa kutoka katika mitaa ya Conference yetu. Mafunzo haya yalitoa hamasa kwa wakurugenzi wa afya makanisani kujifunza zaidi ili kwenda kuwafundisha waumini makanisani na pia jamii inayowazunguka. Kongamano hili kubwa la Afya na Vijana liliendeshwa na wakurugenzi wa afya toka GC, ECD na NTUC ambao ni Dr. Katia Garcia Reinert, Dr. Locero,Dr. Fesaha na Dr. Silas Kabhele.

Katika kuhamasisha mtindo wa maisha bora kiafya, tumeweza kuanzisha club za afya katika makanisa ya Nyegezi, Buzuruga, Mabatini na Kirumba pia na kwa watumishi wa South Nyanza. Katika zoezi hili wanakikundi hukutana katika baadhi ya siku ndani ya wiki na kufanya mazoezi ya viungo. Ndio maana mpaka sasa tulivyofanya zoezi la kupima shinikizo la damu katika watumishi wa jimbo ni mtumishi mmoja tu ndio alionekana kuwa na shinikizo la juu la damu.

## MAHUSIANO YA KIJAMII, KITAIFA NA KIMATAIFA.

Katika eneo hili tumeweza kuifikia jamii ya ndani ya kanisa ndani na nje ya Tanzania, pia kuifikia jamii isiyo ya waadventista ikiwemo kujenga mahusiano mazuri na serikali. Mathalani, tumeweza kutembelea baadhi ya mashule ya kanisa, serikali na binafsi na kufanya uchunguzi wa afya za wanafunzi na kutoa matibabu.

**Kushiriki katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona.**

- Kwa kushirikiana na kamati ya maafa ya wilaya ya Ilemela, hospitali yetu ya SDA Pasiansi imekuwa mstari wa mbele kushiriki mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covis-19. Kwa kushirikiana na ADRA Tanzania, Hospitali ya Pasiansi imekuwa kimbilio kwa kuhudumia wagonjwa wa Corona ambao katika hospitali nyingine wamekuwa wakikataliwa, hivyo tumaini lao limepatikana katika hospitali yetu.

**Kushiriki katika zoezi la uchangiaji damu.**

- Katika kipindi ambapo taifa zima lilikumbwa na ugonjwa hatari wa homa ya mapafu, kulionekana kuwa na hitaji kubwa sana la damu salama. Kwa kushirikiana na ofisi ya mkuu wa mkoa wa Mwanza kanisa la waadventista wa sabato katika SNC limekuwa ni

sehemu ya msaada mkubwa katika kuhamasisha zoezi la uchangiaji damu. Kiasi cha unit 225 katika maeneo ya jimbo letu. Vilevile katika siku ya mchangiaji damu duniani, kanisa letu limekuwa mstari wa mbele na kuifanya wilaya ya Ilemela kuwa namba moja kitaifakatika zoezi la ukusanyaji damu. Katika siku ya kilele cha mchangiaji damu, Mh. Ummy Mwalimu Waziri wa afya alikabidhi cheti cha mchangiaji damu kwa kanisa la waadventista wa sababo kupitia jimbo la SNC.

**Kuanzisha kampeni mbalimbali za jamii.**

- Tumefanikiwa kuanzisha kampeni ya upasuaji wa watoto watu wazima wenye midomo Sungura, na kwa mwaka jana watoto 20 na watu wazima watatu wamefanyiwa upasuaji bila kulipia ghalama yoyote katika hospitali yetu.

**Kutembelewa na viongozi mbalimbali wa serikali.**

- Kwa kipindi chote ambacho tumekuwa kukijishughulisha na mambo ya kijamii, tumetembelewa na viongozi mbalimbali wa kiserikali na kufika kuangalia miradi ambayo kanisa imeanzisha ukiwemo mradi wa hospitali. Miongoni mwa wageni waliotutembelea na Naibu Waziri wa Ardhi Dr. Angelina Mabula, Naibu waziri wa Afya Dr. Khamis Kigwangala, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mh. John Mongela na mkuu wa wilaya ya Ilemela Mh. Severine Lalika.

## MIPANGO KUFIKIA NJOZI 2025+

Baada ya kugundua kuwa kuna hitaji kubwa la kuhudumia wagonjwa nchini Tanzania, kanisa limekuja na mpango madhubuti wa kuhakikisha kuwa katika miji mikubwa kunakuwa na hospitali kubwa za kanisa ambazo zitakuwa ni moja ya kulitambulisha kanisa vyema nchini mwetu na nje ya mipaka ya nchi yetu.

Hivyo mpango huu umeitwa vision 2025+, yaani njozi 2025 na kuendelea. Njozi hii itaiwezesha hospitali yetu kuwa moja ya hospitali bora kabisa nchini kwa namna ambavyo itatoa huduma za afya kwa viwango vya hali ya juu. Kwa muda wa miaka mitatu, hospitali yetu inapaswa iwe na jumla ya madaktari bingwa wasiopungua 10, vifaa vya kisasa zaidi ikiwemo CT-Scan na MRI. Pia Kuhakikisha kunakuwa na chuo cha afya katika jimbo letu.

Mungu awabariki.

# TAARIFA YA IDARA YA VIJANA, CHAPLENSIA NA MUZIKI.



**MWL. ISAACS MANYONYI**
MKURUGENZI WA IDARA YA VIJANA, CHAPLENSIA NA MUZIKI.

MKUTANO MKUU WA NANE WA SNC (SESSION)
SEPTEMBA 22, 2022.

# IDARA YA VIJANA (2016-2022)

## UTANGULIZI

Ninawashukuru wote, maofisa, wakurugenzi wa idara, wachungaji, kamati kuu ya Conference na washiriki kwa kadri tulivyoshirikiana katika kulisukuma gurudumu la kazi ya Bwana katika idara ya vijana tangu 2016 hadi 2022 tunapofikia kwa mafanikio makubwa.

South Nyanza Conference kwa wastani tuna idadi ya vijana kuanzia umri wa miaka 4-30 wapatao 90,572. Tumekuwa na Wanachama kati ya 36,289 - 45,000, kwa hiyo tumekuwa na vijana wasio wanachama yapata 45,000-54,334

## MIPANGO YA IDARA YA VIJANA 2016-2022.

- Uinjilisti
- Uongozi-kuhitimisha Master Guide kila kanisa
- Kiongozi mwandamizi wa vijana
- Malezi na makuzi kwa makundi yote ya vijana

Semina za vijana zimefanyika katika mitaa na kanda mbalimbali katika CONFERENCE YETU;

- Kozi ya uongozi wa vijana wakubwa ilianzishwa mwaka 2018 na kuzinduliwa kule Jinja, Uganda Feb 2019. Conference yetu iliwakilishwa na viongozi wanne: Isaacs Manyonyi, David Kitundu, Yango Mafuru na Mabula Tobe na hao ndio wakufunzi walioidhinishwa kutoa mafunzo kwa ajili ya kozi ya vijana wakubwa(SYL) pamoja na Faustine Msese aliyehitimu darasa la Kiongozi Mwadventista na imeendelea katika kanda zote 13 za vijana South Nyanza Conference na wanafunzi wanaochukua na kuendelea na kozi hii wameongezeka hadi kufikia 350. Katika Conference

yetu SYL waliohitimu ni 41(Shamaliwa Feb 2021-25, Sogesca Sep 2021-6, Shamaliwa Feb 2022-10)

- Kozi ya Master Guide: Waliohitimu kozi ya Master Guide ni 44 (Shamaliwa 34 na Sogesca 10)
- Investiture programs (vyeti/uvishaji wa pini na nishani) zimefanyika kila mwaka katika makanisa na kimtaa. Tangu mwaka 2016 tumevisha nishani 8648 na pini 1296 za watafuta njia. Pini za wavumbuzi 1001 na Tuzo 4606
- Siku ya Watafuta njia imekuwa ikifanyika katika makanisa mahalia na katika mitaa na kanda. Mwaka 2019 siku ya Watafutanjia duniani ilifanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba ambapo watu wapatao 12,000 walihudhuria sherehe hizi. Tulikuwa na uwakilishi kutoka Union ya kusini mwa Tanzania,Uganda, Rwanda, na Kenya na viongozi wetu toka Divisheni ECD-Pr Mwakalonge na General Conference- Pr Andres Peralta -Mkurugenzi wa Watafutanjia GC. Siku hiyo walibatizwa Watafutanjia 132.
- Effort zilizoendeshwa na vijana makanisani na kanda ni 51 na roho 5,930 Zilibatizwa.
- Sabato maalumu za Wavumbuzi zilifanyika kule Nyegezi, Mwanza Mwezi Septemba,2020- na Sima, Bariadi mwezi Novemba 2020. Na mwaka 2022, Wavumbuzi walikuwa na Sabato maalum katika kanisa la Waadventista Wasabato Kirumba tarehe 7/5/2022. Sabato ya Wavumbuzi duniani imesherehekewa mara mbili tangu ilipoanzishwa, mwaka 2021 na mwaka 2022 kulikuwa na mwitikio mzuri katika makanisa na mitaa mahalia.
- Idara ya vijana South Nyanza Conference imekuwa ikishiriki katika matendo ya huruma kila mwaka, Huduma ya kuchangia damu imelifanya kanisa la Waadventista wa Sabato kuwa kundi la kwanza la dini

Tanzania katika uchangiaji damu. Unit 4200 zimechangwa. Katika majuma ya matendo ya huruma, nguo, chakula,fedha, vifaa vya shule, vitabu vilitolewa pamoja na kaya maskini kukatiwa bima za afya.. Nyumba kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum, wajane na wazee zilijengwa kule Bariadi, Mahina na Igombe. Ujenzi wa nyumba ya kipofu Igogwe mtaa wa Pasiansi ulifanywa na kanda ya Mwanza Magharibi na Mashariki. Wafungwa walitembelewa na kuwa na ibada na vijana na wengine walitoa maisha yao kwa Kristo. Huduma kwa magereza haikuishia hapo bali maofisa wa Magereza walitembelewa pia pamoja na familia zao na waligawiwa vitabu kama vile Pendo lisilo kifani, Sabato ya kweli nk. Gharama zilizotumika katika program ya matendo ya huruma ni kiasi cha shilingi 70,489,550/=

- Kwa ajili ya mafunzo ya uongozi na fani mbalimbali za ujuzi wa Maisha tumekuwa na rale na makambi ya vijana yaliyofanyika kimtaa na kikanda (kule Lalago, Nangale, Mukidoma, Luchelele, Kayenze, Kitongosima) na Conference kule Busulwangili, Kizumbi na Sogesca
- Tumeshiriki mikutano ya kimataifa kule Kisumu-Kenya katika kongamano la uongozi la Divisheni mwaka 2018 vijana 100 walihudhuria na Congress ya Vijana ya Divisheni tatu (ECD, AID, na WAD) iliyofanyika University of Eastern Africa Baraton na waliohudhuria ni 32.
- Tumeweza kutafsiri miongozo kadhaa ambayo imekuwa ni msaada kwa viongozi na walimu wa makundi ya vijana wadogo na wakubwa kama moduli za Mabalozi ya kwanza hadi ya saba, Mwanakondoo na Kinda la awali, Njia ya Furaha kwa ajili ya Watafutanjia, mwongozo wa Mabalozi na miongozo ya vijana wakubwa.




*Picha 1: Program ya Investiture iliyofanyika katika kanisa la Kisesa.*



*Picha 2: Vijana Watafutanjia wakiwa katika program ya huduma kwa jamii.*

## MRADI WA OYIM

Tunayo makundi ya vijana yanayoshiriki katika miradi ya utume na jumla ya vijana 356 wanashiriki. Miradi hiyo ni Pamoja na huduma kwa waganga wa kienyeji, kaya maskini, Watoto wa mtaani, watu wa madhehebu mengine, huduma mahospitalini, wanafunzi, waendesha boda boda.

Uzinduzi wa Oyim katika union yetu ulifanyika katika viwanja vya kanisa la Waadventista wa Sabato Pasiansi tarehe 3/5/2021 na mkurugenzi wa Vijana wa ECD, Pr Magulilo Mwakalonge na Mkurugenzi wa Vijana NTUC, Pr Elias Kasika. Vijana yapata 300 walihudhuria uzinduzi wa Oyim.Kiasi cha sh 16,300,450 zimetumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya OYIM

Pamoja na yote yaliyofanyika zipo baadhi ya changamoto zilizojitokeza:

- Upatikanaji wa vifaa vya vijana kama vile nishani na pini Pamoja na miongozo ya idara. Hata hivyo jitihada kubwa zilifanyika kuvipata.
- Baadhi ya viongozi wa kanisa kutoifahamu idara na kukosa kutoa kipaumbele kwa huduma za vijana na program zake.



*Picha 3: Uzinduzi wa mradi wa One Year in Mission (OYIM) Pasiansi.*

## PUBLIC CAMPUS MINISTRY

Huduma kwa wanafunzi katika Taasisi za Umma inahusisha vijana wanafunzi wanaosoma shule za sekondari wapatao 30,000 na wale wa vyuo vya kati na vyuo vikuu 1500. TUCASA inahusisha vyuo vifuatavyo: ADEM-AGENCY FOR DEVELOPMENT OF EDUCATIONAL MANAGEMENT, CUHAS-BUGANDO, BUTIMBA TTC, CBE-COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION, FETA, IFM, LITA MABUKI, MCSD, LUCHELELE, MIPANGO, MISUNGWI CDTTI, NGUDU SCHOOL OF ENVIRONMENTAL HEALTH SCIENCES, SAUT, SUMVE SCHOOL OF NURSING AND MIDWIFERY, JEMA, MCOHAS-MWANZA CITY COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES, MALYA FDC, BWIHAS-BWIMA INSTITUTE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES, BINZA VTC, MASWA COTC, MALAMPAKA VTC, IFM-SAPIWI, MWAPOI-MWANZA POLYTECHNIC INSTITUTE,

Angalia takwimu ya Mei 2022

| NO | KANDA | IDADI YA WANA ASSA |
|---|---|---|
| 1 | MASWA | 2650 |
| 2 | MAGU | 2672 |
| 3 | BARIADI KASKAZINI | 2721 |
| 4 | BARIADI KUSINI | 2478 |
| 5 | BARIADI MASHARIKI | 2217 |
| 6 | BUSEGA | 2509 |
| 7 | MWANZA MASHARIKI | 2584 |
| 8 | DUTWA | 2011 |
| 9 | ITILIMA | 2312 |
| 10 | MISUNGWI | 1380 |
| 11 | MWANZA MAGHARIBI | 2530 |
| 12 | MWANZA KATI | 1120 |
| 13 | MEATU | 2719 |
| | **JUMLA** | **29903** |

**MALENGO:**

Kuwashirikisha katika huduma za kuhubiri, kutoa masomo mbalimbali kama ya afya, kaya na familia na uongozi kanisani.

Kuhamasisha wanachama wote wa ASSA na TUCASA kununua Biblia na kuzisoma na kufanya uamuzi wa kubatizwa kwa wale ambao hawajabatizwa

Kuhamasisha uinjilisti mashuleni: Vijana wa Assa wameshiriki katika kuendesha efforts katika maeneo mbalimbali kama vile Nyakato, Nangale, Itilima, Igombe, Rodan, Bariadi Kaskazini-Kusekwa Memorial, Bujingwa-mtaa wa Wilayani, Migato,Mabatini. nk Jumla ya Efforts 29 zilifanyika na Roho 2200 zilibatizwa.



*Picha 4: Wana TUCASA wa IFM Sapiwi wakiwa na mkurugenzi.*

## CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA HUDUMA KWA WANAFUNZI MASHULENI/KAMPASI ZA UMMA.

- Idadi ndogo ya wanachama wa ASSA wanaotoa ada, ambazo pia hazitolewi kwa wakati. Uhamasishaji ni mchakato endelevu.
- Muingiliano wa ratiba za matukio na likizo za vyuo, jambo ambalo lilisababisha kuwepo na ufanisi mdogo. Tutaendelea kunyumbulika kulingana na mazingira.
- Makanisa mengi kutokuwa karibu na wanafunzi hawa kwa malezi na maelekezo ya kiutawala. Bado wapo wanafunzi wengi wanajihudumia katika vipindi vya dini na ibada. Semina na msisitizo uendelee kufanyika.
- Baadhi ya shule kutotoa ruhusa kwa wanachama kuhudhuria mikutano ya chama na ibada.
- Ukosefu wa fedha kuwawezesha viongozi wa chama kufika kwenye matukio mbalimbali waliyohitajika kuwepo. Makanisa yasisitizwe kuweka bajeti kidogo kuwawezesha viongozi kutekeleza majukumu yao.
- Upungufu wa machaplensia(wachungaji walezi) kusaidia huduma za chaplensia hasa katika miji ya Mwanza na Bariadi.

## IDARA YA CHAPLENSIA (ADVENTIST CHAPLAINCY MINISTRY)

- Idara inashughulika katika kutoa huduma za Kiroho kwa Makundi maalum ya Kijeshi, Magereza na Hospitali.
- Kuhamasisha na kuwaunga mkono/ kuwawezesha Machapleni wa Kiadventista.
- Kupanua wigo wa injili katika jamii kubwa kupitia huduma ya Machapleni.
- Kutoa malezi na mafunzo ya Kichungaji na ya kidini kwa washiriki wa Kanisa katika hali maalum.
- Kusudi la huduma ya Kiadventista ya Chaplensia ni kutangaza kwa ulimwengu Injili ya Milele, hivyo kurejesha ubinadamu ulioharibiwa kuelekea katika ukamilifu wa mahusiano na Mungu.

Hapo nyuma Idara ya Chaplensia ilishughulika na maeneo matatu:

- Magereza, Majeshi.
- Hospitali na vituo vya afya.
- Taasisi za Elimu na Umma (Wanafunzi).

Tangu mwaka 2020 kitengo cha wanafunzi kilirudishwa kwa Idara ya vijana.

### HUDUMA ZA MAGEREZA:

Huduma za Magereza zimefanyika katika gereza la:

- Butimba – Mwanza
- Malya – Maswa
- Maswa
- Bariadi – simiyu.

Huduma zilizotolewa ni Pamoja misaada ya vitu kama vile Sabuni, Mipira ya kuchezea, Chakula, kufungiwa dishi/King'amuzi kwa ajili ya Mahubiri na taarifa mbalimbali za habari.

Mwaka 2017, kulifanyika Hafla kubwa katika gereza la Kirumba ambapo wafungwa wote na askari walipata chakula cha pamoja, Program iliyogharimu Sh. 11,000,000/= (kiasi hicho kilitoka katika Makanisa mbalimbali katika Conference yetu), Nakala 2500 za Pendo lisilo kifani ziligawiwa gerezani. Hafla hii ilipelekea wafungwa watatu kubatizwa.

Mwaka 2018 Mungu alitufanikisha kuwapatia Chakula gereza la Kasungamile. Hafla ile ilipelekea wafungwa watatu kubatizwa katik Kanisa la Waadventista wa Sabato baada ya kutoka gerezani, Hafla hii iligharimu kiasi cha Sh. 3,500,000/=, tunawashukuru sana Kanisa la Igoma waliojitolea kwa kiasi kikubwa na Wadau wengine katika Conference yetukuanikisha huduma hii, pia nakala Zaidi 1500/= za Pendo lisilo Kifani zilipelekwa gerezani.

Katika gereza la Mkoa la Bariadi vitabu vipatavyo 569 vyenye Thamani ya Sh. 4,187,850/= vilitolewa (vitabu hivyo ni Mapambano na faraja, Maisha yangu leo, Leo na Mungu, Haki kwa Imani, Tumaini kuu, Jipatie Amani moyoni, Pendo lisilo kifani, Sabato ya kweli, Kukua Kiroho, Biblia, Makesha na Lesoni. Mahitaji mengine ya kimwili kama vile Nguo, Viatu, Sabuni za unga na za vipande, Dawa za Meno, Miswaki vyenye thamani ya Sh. 250,000/= wafungwa Kumi walikata shauri kubatizwa.

## HUDUMA ZA MAHOSPITALI:

Huduma za Mahospitali ni pamoja na

- Ibada na maombezi
- Misaada ya kijamii, ikiwa ni pamoja na chakula, Nguo, Sabuni n.k (katika Hospitali ya Bariadi, thamani ya vitu ni 250,000/=. Katika maeneo haya ya vituo vya afya na Hospitali, Makanisa yameshirikishwa kutoa huduma za faraja na kuwatia moyo wagonjwa.

Kwa vile Chaplensia inashughulika na hali maalum kwa watu wasio Waadventista, yupo mtoto wa mtaani aliyeletwa na wanafunzi Waadventista na hatimaye kupata Msaada wa kusomeshwa na Kanisa la Waadventista wa Sabato Mkolani.

Katika tetemeko la Ardhi kule Kagera Idara ya Chaplensia ilishiriki kwa kuchangia jumla ya
Sh. 3,000,000/=.
Mwaka 2021 Vijana wanaotoka maeneo ya Matongo, mtaa wa Dutwa walifanikiwa kutembelea gereza la Matongo na kupeleka misaada mbalimbali Pamoja na kufanya ibada ya Pamoja na wafungwa. Ilikuwa ni ibada ya pekee ambayo wafingwa walikiri kutoipata tangu waingie gerezani hapo. Baada ya huduma hiyo wafungwa waligawiwa vitabu na maofisa wote wa gereza Pamoja na familia zao walipta nakala za vitabu vya Pendo lisilo kifani na vitabu vingine.




*Picha 5: Huduma ya kuwatembelea wagonjwa.*

Nipende kutambua mchango mkubwa uliofanywa na Wachungaji wafuatao katika huduma ya Chaplensia Hospitalini na Magereza, na kundi la Wanafunzi:

1. Alex Ibrahim Juma.
2. Samweli Majenga.
3. Joseph Apollo.
4. Beatus Mlozi.
5. Nuhu Suleman.
6. Kubba Mayalu.
7. Joel Chacha.
8. Harun Kuyenga.
9. Boaz Abayo.
10. Samweli Ndekeja.
11. Magreth Mbagga.
12. Phillip Ndikumwami.
13. Joshua Mbwambo.

## MAONI/MAPENDEKEZO:

- Wachungaji wa Mitaa ambapo kuna Taasisi kama Hospitali na Magereza, na Wanajeshi wapange ratiba za kutembelea maeneo hayo.
- Kushugulikia vibali vya Wachungaji na wale wanao jitolea kuhudumu katika Magereza.
- Kuongeza Machapleni katika Miji ya Bariadi na jiji la Mwanza ili kuhudumia kwa urahisi na wepesi vituo vya afya na Hospitali pamoja na Magereza ambayo muda mwingi unapita bila huduma ya Chaplensia kwa kuwa Taasisi zimeongezeka sana na huduma zinahitajika.
- Ushirikishaji makini wa Makanisa kupitia vyama vya AMO na Dorikas kuwafikia watu waliomo Magerezani na Hospitalini.

# IDARA YA MUZIKI

Kulingana na takwimu ya February 2022 South Nyanza Conference ilikuwa na jumla ya kwaya 953.

- Kwaya za Kanisa za wana wa kike (Adventist Women Choir)– 47.
- Kwaya za Kanisa za Watafutanjia/ Wavumbuzi/ Watoto – 121.
- Kwaya za Kanisa za vyama vya vijana – 260.
- Kwaya za Kanisa – 525.

Kumefanyika Makongamano ya muziki

- Shamaliwa 2016.
- Shamaliwa 2022.
- Pasiansi 2019.

Na kanda za Bariadi (2020), Dutwa (2022). Katika makongamano yote haya Elimu kuhusu muziki na falsafa ya muziki wa Kiadventista ilitolewa.

Mambo ya msingi yaliyosisitizwa katika idara ya muziki.

- Kila kanisa linahimizwa kuwa na vyombo vya usikivu kwa ajili ya kuboresha ibada ya uimbaji kanisani.
- Kufanyika kwa makongamano ya muziki mara kwa mara katika Conference ili elimu ya muziki iweze kuwafikia wengi na kwa urahisi na kwa muda uliokusudiwa.
- Taasisi zetu za elimu, zianze kufundisha muziki wa kikristo. Kuwe na somo la muziki shuleni.
- Wachungaji, wazee wa makanisa na uongozi wengine, wapewe semina stahiki ya muziki wa Kikristo na washirikiane na waratibu wa muziki makanisa I kusimamia uimbaji unaoendeana na falsafa ya muziki wa Kiadventista, na Kusimamia miongozo na taratibu

zote kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo wa Kanisa.

- Kuhimiza na kutambua washiriki walio na karama ya uimbaji na kuwasaidia kujiunga katika chuo cha muziki (TASUBA)
- Idara imeendelea kuelimisha kuacha kuimba nyimbo zenye mahadhi ya Reggae, Jazz, Rock and Roll, Rumba.
- Idara ilisisitiza uimbaji wa waumini wote (Congregation Singing). Nyimbo 20 zilichaguliwa na kuhimizwa kufundishwa na kuziimba kanisani. Nyimbo hizo ni zile ambazo hazikuzoeleka kuimbwa na kutofahamika kwa washiriki wengi. Nipongeze kanisa la Kirumba ambao wamejitahidi kufanya vizuri katika huduma hii ya waimbaji wa waumini wote.




*Picha 6: Mgeni kutoka Kenya katika semina ya muziki.*

# TAARIFA YA IDARA YA MAWASILIANO.



## MCH. PHILIP GEORGE

MKURUGENZI WA IDARA YA MAWASILIANO, VYOMBO VYA HABARI SATELLITE



MKUTANO MKUU WA NANE WA SNC (SESSION)
SEPTEMBA 22, 2022.

## UTANGULIZI:

Wapendwa watumishi wa Mungu aliye hai, Nawasalimu katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo! Idara ya mawasiliano vyombo vya Habari na Satellite tunamshukuru sana Mungu kwa ulinzi na baraka zake tele alizotupatia kwa kipindi kizima cha miaka hii sita ya kutumika shambani mwake.

*Ndugu Wajumbe;*

Ikumbukwe kwamba idara ya mawasiliano, ndiyo idara pekee inayowezesha idara zingine kutekelezeka. Mungu alianza kazi kwa kuwasiliana na kuweka mitambo yake ya TV na kamera pale Roho wa Mungu alipoelea juu ya vilindi vya maji kisha uumbaji ukaendelea. Mwanzo 1:2 "Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji"

Idara ya mawasiliano huhamasisha utumiaji wa program thabiti ya uhusiano na mbinu zote za kisasa za mawasiliano, teknolojia endelevu ya vyombo vya Habari katika kueneza injili. Nitakwenda kidijitali kuwafanya kuwa wanafunzi.

Wajumbe napenda ninukuu maneno ya kalamu ya uvuvio ya nabii. E.G White;

*"Inatupasa kutumia kila njia iliyo halali kuleta nuru kwa watu. Vyombo vya Habari vitumike, kila shirika la matangazo litakalovuta usikivu juu ya kazi ya Mungu" 6T, 36.pg*

*"Njia zitabuniwa za kuifikia mioyo, baadhi ya njia zitumikazo katika kazi hii zitakuwa tofauti na njia zilizokuwa zikitumika zamani." 6T, pg 37.*

## MIPANGO YA IDARA 2016-2020:

- Uzalishaji wa vipindi vya Radio ya Morning Star na kuanzisha sadaka ya Morning Star TV.
- Kuhimiza mfumo wa kumbukumbu za washiriki ACMS.
- Kuanzisha kituo cha Habari (Media Centre) cha jimbo SNC.
- Kushiriki kikamilifu katika mahubiri kwa njia ya vyombo vya Habari (Media Evangelism) kila mwaka.
- Kuwa na mikutano, semina na mafunzo ya wana-mawasiliano wa kanisa Tanzania inayojumuisha, Wachungaji, Makarani wa kanisa, Viongozi wa mawasiliano na wadau wa Habari mbalimbali.
- Kuhimiza matumizi bora ya mitandaoni kwa ajili ya malezi na uinjilisti.
- Kukuza mahusiano ya kanisa na vyombo vingine vya Habari visivyomilikiwa na kanisa la Waadventista Wa Sabato.
- Kuhimiza na kusisitiza viwango vya juu kutambulisha mahali jengo la kanisa lilipo; nyumba ya Mchungaji, vibweta vya makambi, visima vya ubatizo na vyoo vya kisasa.
- Kuhimiza makanisa kufundisha na kushiriki kuitumia teknolojia na tasmia ya Habari katika juhudi za kuifikia jamii tukiwa na Yesu kwa ajili ya injili ya milele.



*Picha 1: Semina ya Mawasiliano Simiyu Bariadi.*

## UTEKELEZAJI WA MALENGO:

- Tumefanikiwa kutoa semina na mafunzo elekezi kwa kanda zote za jimbo letu – juu ya namna ya kuitumia teknolojia katika kufikisha injili. Kwa uchache tumefikia kanda ya Bariadi, Meatu, Maswa, Mwanza na Nassa. Jumla ya mitaa 70 kati ya 78 imefikiwa.
- Tunamshukuru Mungu kutuwezesha kufanikiwa kutoa habari na taarifa kwa ofisi kuu kwa ngazi ya juu kama zilivyohitajika kwa wepesi Zaidi.
- Kuhusu uzalishaji wa vipindi vya Radio ya Morning Star na Televisheni ya Hope Media SNC, tumefanikiwa kutengeneza vipindi 116 vya redio na vipindi 116 vya Television. Sadaka ya Radio na Hope TV imeongezeka kutoka 280,774,625/= (2015) hadi 768,059,970/= (2022) sawa na asilimia 267.8% ongezeko.
- Pengine, tunamshukuru sana Mungu kutuwezesha kuhimiza mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za washiriki, (ACMS) kidijitali kwa asilimia 96% ambapo jumla ya washiriki 150,800 kati ya 154,460 wamesajiliwa, Makanisa 550/562 na mitaa 78 ilikuwa imesajiliwa taarifa hii inapoandaliwa.
- Pamoja na hayo, hivi karibuni tumefanikiwa kupokea mfumo wa CFMS – Unahusiana na utunzaji na udhibiti wa fedha za kanisa ambapo tayari tumesajili Washiriki 4607, Makanisa 562, Mitaa 78 kufikia April, 2022.



*Picha 2: Waumini wakiwa katika mojawapo ya semina za mawasiliano.*

- Tunamshukuru Muumbaji wetu pia kwa kutusaidia kufikia uanzishwaji wa kituo cha Habari (Media Centre) ya jimbo letu la SNC, ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 18 Julai 2020 na Mch. Switta E. Stevens aliyekuwa katibu mkuu wa jimbo la SNC, ambacho kinaitwa Hope Media SNC. Jina la Mungu liinuliwe.



*Picha 3: Muonekano wa ndani wa kituo cha habari chaHope Media SNC.*

- Sambamba na hayo, hatuna budi kumshukuru Bwana kwa kutuwezesha kushiriki kikamilifu katika mahubiri ya hadhara kwa njia ya vyombo vya Habari (kidijitali) ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa kanisa la Waadventista Wa Sabato Tanzania SNC.
- Tunamshukuru Mungu kwa mwitikio mkubwa wa matumizi ya mitandao ya kijamii mfano Instagram tuna wafuasi takribani 3300; Facebook tunao wafuasi zaidi ya elfu saba (7000). Whatsap inatumiwa na 90% ya mitaa yote ya SNC. Pamoja na hayo tumekuwa wastani wa watazamaji na wafuasi wa 20,000 katika mtandao wa YouTube (Hope MEDIA SNC) toka kuanzishwa kwa chaneli hiyo.

- Tumefanikiwa pia kushirikiana na vyombo vingine vya habari kama Sahara Media; Start Tv; Start Tv Religeon; Star International Tv; (Mwanza) AFAMA TV na Sibuka Radio (Maswa), na Bariadi FM (Simiyu).
- Kupitia semina na mafundisho, idara ya mawasiliano tumefanikiwa kutayarisha na kusambaza mabango/sticker zisizo pungua 515 kuelekea mahali pa kanisani, mashuleni na hospitali zetu zinazopatikana katika Conference yetu nzima; Vibweta vizuri vimejengwa na vyoo vimejengwa; Mfano: Mtaa wa Mkolani (kisima makini cha ubatizo); Ntuzu (choo makini) Nyumba za Wachungaji (Buzuruga); mitaa mingine ni Ngasamo, Kidinda; na Nyegezi. Pia Vivuli vizuri vya Makambi, mtaa wa Nyegezi, Shamaliwa, Buswelu, Nyakato, Meatu. n.k




*Picha 4: Bango linaloelekeza uelekeo wa kanisa.*

- Kwa kushirikiana na TAMC tumefanikiwa kuandaa mikutano ya mawasiliano (GAIN- Tanzania) miwili 2017-2022 na pia kushiriki mikutano mingine Arusha, Dar-es salaam, Morogoro n.k. Zaidi ya 70% ya washiriki wa mikutano wamekuwa wakihudhuria kwenye mikutano ya Gain-Tanzania kutoka SNC.



*Picha 5: Picha ya pamoja washiriki wa mkutano wa GAIN 2022.*



*Picha 6: Semina za mafunzo elekezi ya mawasiliano.*

## MAHUBIRI YALIYOFANYIKA TANGU 2017 HADI 2021

| MWAKA | MAHUBIRI | MHUBIRI | MAHALI | WMM* | UBATIZO |
|---|---|---|---|---|---|
| FEB, 2017 | USHINDI HATIMAYE | PR. DAVID MBAGA | MABATINI MWANZA | 37526 | 9,407 |
| MEI, 2018 | UFUNUO WA MATUMAINI | PR. MARK FINLEY | CCM KIRUMBA MWANZA | 18940 | 19,227 |
| MEI, 2019 | TUMEKARIBIA NYUMBANI | PR KENANI MWAMSOMOLA | MBEYA | 6035 | 603 |
| SEP ,2019 | NYUMBANI HATIMAYE | PR. PAUL SEMBA | KINYEREZI DAR-ES SALAAM | 13913 | 1,962 |
| FEB, 2020 | MUNGU KWANZA | PR. CARLTON BYRD. | CHATO KAGERA | 4120 | 398 |
| MEI, 2020 | UZOEFU WA NGUVU YA MUNGU | PR. MGANDA BARAKA | DODOMA | 4188 | 418 |
| SEP, 2020 | TUMAINI LITOKALO JUU | PR, NZUNGU LUCAS | HEDARU MANYARA | 9102 | 3,250 |
| MEI, 2021 | SHANGWE KATIKA NJIA YAKE | PR. MARK W. MALEKANA | KIZOTA DODOMA | 8697 | 6,008 |
| SEP, 2021 | AMANI ITOKAYO JUU | PR. GODWIN LEKUNDAYO | NYAMONGO TARIME | 12780 | 11,880 |
| JUNI, 2022 | UKWELI UNAOKUWEKA HURU | PR. DAVID MAKOYE | KARATU, MANYARA | 52,280 | 11,955 |
| **JUMLA** | | | | | **65,108** |

*WWM* - Wastani wa Watazamaji Mtandaoni.*

## CHANGAMOTO.

- Mwamko tunduizi wa viongozi na washiriki wa kanisa kuthamini juhudi za kubandika mabango makanisani na taasisi za kanisa jimboni.
- Ufunguzi wa online TV umeghubikwa na vikwazo na masharti magumu ya TCRA.
- Wafuasi wachache kwenye mitandao ya kijamii-kufuatia mwamko mdogo wa washiriki wa kanisa kusherehesha injili kwenye mitandao ya kijamii. Mfano online TVs.
- Tovuti nyingi za makanisa ni mfu, hazina vivutio vipya, habari, matukio n.k
- Imani potovu na ujinga wa ki-elektroniki kwa baadhi ya mitaa na makanisa ya vijijini. Mfano: Ukusanyaji wa habari kuhusishwa na kafara za freemanson. pia mfumo wa CFMS & ACMS - kuhusishwa na ujio wa namba 666. (alama ya mnyama).
- Ushirikiano duni kwa baadhi ya wachungaji wachache na viongozi wa makanisa. Mfano ufunguzi wa akaunti za bank kwa makanisa.



## MALENGO YA 2023-2025

Kwa kuwa idara ya mawasiliano ipo ili kuunganisha idara zote za kanisa kwa utume ulimwenguni, tutaitumia idara kuhakikisha kuwa media na njia zote zinazotumika kuifikia mioyo, zinatumika vizuri kuendeleza utume wa kanisa katika himaya ya jimbo la SNC kwa njia zifuatazo: -

- Kushiriki kikamilifu mikutano ya GAIN Tanzania na mikutano yote ya NET EVENT na semina zote ngazi ya Union-NTUC kwa mwaka 2023-2025.
- Kuendeleza Motto wa Nitakwenda 100% kwa kufanya mahubiri na uinjilisti kwa njia ya mitandao, Whatsap, You Tube, Instagram, Twitter. n.k (kuhimiza uinjilisti wa kidijitali).
- Kuandaa semina za kunoa wana-mawasiliano 100% kwa kila mtaa na kutoa miongozo ya kujifunza kwa wahubiri wanaoamua kutumia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari katika mahubiri yao.
- Kuweka kielektronia masomo ya ugunduzi na sauti ya unabii kwa ajili ya watumiaji wa mitandao ya kijamii, kutoa mitaala/miongozo kwa ajili ya kukusanya, uandaaji wa taarifa ya uhamasishaji wa majina ya washiriki kuingia kwenye mifumo ya ACMC na CFMS.
- Kufufua, kuanzisha na kuimarisha tovuti za makao makuu ya jimbo letu SNC na makanisa yake yote.
- Kutayarisha na kusambaza matangazo ya matukio makubwa ya Jimbo la SNC pamoja na Taasisi zake (shule na hosptali).
- Kusimamia na kuimarisha kuwa kila kanisa limeweka utambulisho wa kuelekeza mahali lilipo, kwa kufuata maelekezo ya idara.
- Kuwezesha usajili wa online TV kwa angalau 50% ya makanisa yote ya Jimbo la SNC.
- Kuanzisha gazeti la SNC na makala zingine maalum za afya, kiteolojia n.k kwa ajili ya kanisa na jamii kwa ujumla.

- Kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu Mkuu na Mhazini kuhamasisha matumizi ya mifumo ACMS na CFMS ikiwemo malezi ya washiriki wapya wa kanisa.
- Kuandaa vipindi mbali mbali vya Redio na TV kwa kuwahusisha wachungaji wote na kuvirusha kwenye mitandao ya kijamii.
- Kushirikisha vyombo vingine vya habari, wadau wa habari, waandishi na makarani wa kanisa kuunda timu ya mawasiliano-kanisa na kanisa la mtandaoni ili kuratibu shughuli za ki-utume.
- Kununua vitendea kazi vyakutosha ili kuendeleza njozi ya 'Hope media ya South Nyanza Conference kuwa na studio ya Television na Redio yake kwa 100%.
- Kushiriki kikamilifu kuandaa mahubiri ya Simiyu Net Event September 2023 na mengine yatakayo fanyika kwa kipindi hicho.
- Kupanua kituo cha Hope TV kwenye Mkoa wa Simiyu.

## HITIMISHO

Tunawashukuru kwa dhati viongozi wetu (Maofisa) Mwenyekiti, Katibu na Mhazini wa NTUC & SNC kwa ushirikiano, malekezo na maongozi mema waliyoipatia idara hii ya mawasiliano.

Pamoja na hayo nawashukuru pia Wakurugenzi wenzangu, wachungaji wote wa mitaa, IT's, Makatibu wahitasi na wafanyakazi wote wa SNC, Pamoja na Kamati kuu ya jimbo letu la Nyanza Kusini.

BWANA Awabariki sana,
Ahsanteni kwa kunisikiliza.

# TAARIFA YA IDARA YA HUDUMA ZA WANAWAKE NA WATOTO.



**MRS. MARTHA ZACHARIAH**

MKURUGENZI WA
IDARA YA HUDUMA ZA
WANAWAKE NA WATOTO.



MKUTANO MKUU WA NANE WA SNC (SESSION)
SEPTEMBA 22, 2022.

## UTANGULIZI

**Kusudi la Idara**:

Ni kulea, kuwezesha, na kuwaunga mkono Wanawake katika maisha yao ya Ukristo kama wanafunzi wa Yesu Kristo na Washiriki wa Kanisa lake ulimwenguni.

**Tamko la Utume**:

Idara ya Huduma za Wanawake iko kwa ajili ya kuwainua, kuwatia moyo, na kuwapa changamoto Wanawake Waadventista Wa Sabato katika safari yao kama Wanafunzi wa Yesu Kristo.

**Utume wa Idara**:

Ni kumwinua Yesu Kristo Kanisani na Ulimwenguni.

**Malengo ya Idara**:

1. Malezi (Nuture).
2. Kuwawezesha (Empower).
3. Kuwafikia watu walioko nje ya Kanisa (Out Reach) kwa njia ya uijilisti kuwafanya kuwa Wanafunzi wa Yesu Kristo.



## MIPANGO KAZI MWAKA 2016 – 2022.

1. Mahubiri:
   - Mahubiri ya Hadhara.
   - Mahubiri TMI.
   - Mahubiri ya mlipuko ya AWM NTUC (Meatu).
   - Mahubiri ya AWM Ki-Conference, Kanda, Mitaa na Makanisa.
   - Mradi wa kuhubiri na kujenga Makanisa.
   - Kurejeza Wanawake waliokuwa wameliacha Kanisa.
2. Machangizo ya aina Tatu katika Idara ya Wanawake SNC:
   - Changizo la kituo cha Mvuto Singida Ititi.
   - Changizo la Chuo cha Adventist Women Ministry VTC SNC Pasiansi Mwanza.
   - Machangizo ya kikanda Mwanza, Bariadi, Geita, Maswa, Kahama, Magu, Nkololo, Meatu, Mwakitolyo.
3. Makongamano ya Idara.
4. Kuendeleza Miradi ya Idara iliyokuwepo na kuanzisha Miradi mingine ya Idara.
5. Matendo mbali mbali ya Huruma kwa jamii.
6. Mafunzo ya Mashamba darasa na Bustani za jikoni za mboga mboga.
7. Usajili wa Chuo cha Adventist Women Ministry VTC.
8. Semina za Idara ya Huduma za Wanawake Kikanda, Mitaa na Makanisani.
9. Kugawa Kanda.

## MAFANIKIO:

### 1. MAHUBIRI YA HADHARA.

- Idara imefanikiwa kufanya mahubiri ya Hadhara na kubatiza jumla ya watu 3,683.
- Idara imefanikiwa kurejeza Wanawake 380 na sasa wanaendelea vizuri Kanisani.
- Mahubiri ya mlipuko ya vituo Vinane Kanda ya Meatu. Mahubiri haya yalikuwa ya AWM NTUC vituo ni: Mwakipugela, Mwanyahina, Mwamishali, Majengo, Mshikamano, Mwambiti, Bulyanaga, Ikigijo na kubatiza watu 302.
- Mahubiri Wanawake ki- Conference, kikanda, Mitaa na Makanisani na kubatiza Jumla ya watu 3381.



- Mahubiri ya TMI: Idara imefanikiwa kufanya TMI Magereza yafuatayo: Butimba, Malya, Maswa, Bariadi, Matongo, Meatu, Butundwe, Nyamakwe, na kutoa vitu kama ifuatavyo: Nguo za kike na za kiume, viatu, sabuni, mafuta ya kupakaa, Mafuta ya kula, kiwi, viatu,

Nguo za Watoto, Nyembe, Screen 3, Deck 2 mipira ya kuchezea Miguu 2, jezi za timu 2 za mipira, Biblia, Lesoni, vitabu vya Roho ya Unabii vikiwemo na Vitabu vya Sabato ya kweli. Thamani yake ni kiasi cha Tsh. 38, 840,800/=.

- Matendo ya huruma, Idara imefanikiwa kutoa misaada mbalimbali kwa ajili ya wahitaji kiasi cha Tsh. 12,000,000/= zilitumika.



## 2. MACHANGIZO YA MIRADI IDARA YA WANAWAKE 2016 – 2022.

i. Machangizo ya Miradi – Singida – Ititi – AWM NTUC Mwaka 2016 – 2022.

| TAREHE | KANDA | PESA CASH | MGENI RASMI | KUTOKA |
|---|---|---|---|---|
| 03.09.2016 | MWANZA | 28,000,000.00 | Ev. ZUKI | AFRICA KUSINI |
| 26.08.2017 | KAHAMA | 10,342,000.00 | Pr. Geoffrey MBWANA | GC |
| 02.09.2017 | GEITA | 2,231,000.00 | Pr. Samwel MAKORI | EKUC |
| 09.09.2017 | MWANZA | 26,873,000.00 | Mrs. Debbie MALOBA | ECD |
| 16.09.2017 | BARIADI | 4,223,000.00 | Pr. Mark MALEKANA | STUM |
| 23.09.2017 | SHINYANGA | 1,730,000.00 | Mr. Paulo SOSOMA | MWANZA |
| 30.09.2017 | MEATU | 2,315,000.00 | Pr. Paulo KWILASA | GEITA |
| 07.10.2017 | MASWA | 1,410,000.00 | Mrs. Martha ZACHARIA | SNC |
| 13.10.2018 | BARIADI | 1,438,500.00 | Pr. Paulo KWILASA | GEITA |
| | AWM TF SNC | 5,619,200.00 | TF SNC | SNC |
| 13.10.2018 | WASHIRIKI SNC | 79,500.00 | MAKANISA YOTE SNC | SNC |
| 13.10.2018 | | KITENGE PAIR 1 PIECE 3 AINA YA TELEZA, THAMANI SH. 15,000.00 | MTU BINAFSI | BARIADI |
| **JUMLA YA MACHANGIZO YOTE NI TSH. 84,260,700.00 + 15,000 YA KITENGE = 84,275,700.00** | | | | |

ii. Changizo la Maendeleo ya Mradi wa Chuo cha Adventist Women Ministry Vocational Training College (AWM VTC).

| MWAKA | WAHUSIKA | KIASI TSH. |
|---|---|---|
| 2016 | Wanawake Makanisani | 1,731,300.00 |
| 2017 | Wanawake Makanisani | 6,517,000.00 |
| 2018 | Wanawake Makanisani | 1,366,000.00 |
| 2021 | Wanawake Makanisani | 962,000.00 |
| **JUMLA** | | **10,576,00.00** |

iii. Machangizo ya kikanda kwa ajili ya ununuzi wa Maeneo ya Miradi ya Idara ya Huduma za Wanawake Waadventista kuanzia Mwaka 2004, 2016– 2022.

| JINA | MWAKA | ENEO LILIPO | UKUBWA | KIASI TSH. |
|---|---|---|---|---|
| AWM VTC | 2004 | Pasiansi – SNC | - | - |
| Katoro – Mizeituni | 2004 | Katoro Mizeituni – NGBF | Ekari 3 | 35,000.00 |
| Ngashanda | 2016 | Ngashanda Bariadi – SNC | Ekari 8 | 3,600,000.00 |
| Katoro – Mlimani | 2016 | Katoro – Geita NGBF | Ekari ¼ | Fidia ya uwanja wa kwanza |
| Nyashigwe | 2016 | Nyanguge – Mwanza | Ekari 2 ½ | 7,100,000.00 |
| Kasamwa | 2017 | Kasamwa – Geita NGBF | Ekari 3 | 3,000,000.00 |
| Chandulu | 2017 | Ndagalu – Magu | Ekari 1 ¾ | 700,000.00 |
| Nyashigwe | 2019 | Nyashigwe Mwanza – SNC | Ekari ½ | 3,500,000.00 |
| Mbika | 2018 | Mbika ushetu – Kahama NGBF | Ekari 6 | 2,290,000.00 |
| JUMLA | | | | 20,225,000.00 |

iv. Baada ya Jimbo kugawanywa Mwaka 2019, January 20, Jimbo la SNC tulibakiwa na Maeneo ya Miradi ya Wanawake kama ifuatavyo:

| JINA | ENEO LILIPO | UKUBWA | MKOA |
|---|---|---|---|
| AWM VTC | Pasiansi – SNC | - | Mwanza |
| Ngashanda | Ngashanda – Bariadi | Ekari 8 | Simiyu |
| Nyashigwe | Nyashigwe – Nyanguge | Ekari ½ | Mwanza |
| Chandulu | Ndagalu – Magu | Ekari 1 ¾ | Mwanza |
| Nyashigwe – Kanisa | Nyaguge – Magu | Ekari 2 ½ | Mwanza |

v. Baada ya Conference kugawanywa maeneo yaliyoenda Field ya NGBF ni:

| No. | JINA LA ENEO | UKUBWA | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1 | Katoro – Mizeituni | Ekari 3 | Geita |
| 2 | Katoro – Mlimani | Ekari ¼ | Geita |
| 3 | Kasamwa | Ekari 3 | Geita |
| 4 | Mbika - Usetu | Ekari 6 | Shinyanga |

## 3. MRADI WA KUHUBIRI NA KUJENGA KANISA KUANZIA MWAKA 2016 - 2022 SNC.

**Mahubiri ya Hadhara:**

Idara imefanikiwa kufanya Mahubiri Kumi na moja (11) na kubatiza watu 1398 (Elfu Moja Miatatu Tisini na Nane. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:

- Kanda ya Kahama Mwaka 2018 Kijiji cha Mbika Mtaa wa Mseki Wilayani Ushetu, tulinunua eneo la ukubwa wa Ekari 6 (Sita) kwa thamani ya Tsh. 2,290,000.00 na kujenga Kanisa la uwezo wa kukaa watu 350. Pia tulihubiri na kubatiza watu 97, huduma kwa Jamii tulitoa nguo za thamani ya Tsh. 100,000.00 na katoni za Sabuni Mbili zenye thamani ya Tsh. 50,000.00, Jumla 150,000.00, ujenzi wa Kanisa uligharimu kiasi chaTsh. 3,916,000.00. Eneo hili kwa sasa liko Field ya NGBF. Ni eneo jipya.

| VIFAA VILIVYO NUNULIWA | KIASI (TSH) |
|---|---:|
| Matofali 8,000 ya kuchoma | 500,000.00 |
| Mawe Trip 14 | 500,000.00 |
| Fundi ujenzi Boma | 200,000.00 |
| Wasomba Matofali | 80,000.00 |
| Mbao za Kenchi | 230,000.00 |
| Ufundi wa kuezeka | 250,000.00 |
| Misumari ya Bati na mchanganyiko | 130,000.00 |
| Waya wa kufunga Kenchi | 20,000.00 |
| **JUMLA** | **3,916,000.00** |

- *Ununuzi wa Eneo* **(Tsh. 2,290,000.00)** + *Ujenzi wa jengo la Kanisa* **(Tsh. 3,916,000.00)** = *Jumla Kuu* **(TSh. 6,206,000.00).**

- Kanda ya Jiji la Mwanza Mwaka 2016 Kijiji cha Nyashigwe Mtaa wa Nyanguge, tulinunua eneo la ukubwa wa Ekari 2½ kwa Thamani ya Tsh.7,100,000/= Kulikuwa na Nyumba Mbili za tope zimeezekwa Nyasi, tukajenga Kanisa kubwa lenye uwezo wa kukaa watu 600, ujenzi wake umekamilika bado tu kuweka sakafu chini na kupaka Rangi. Pia tulifanya Mahubiri ya hadhara na kubatiza watu 97. Ujenzi wa Kanisa hilo uligharimu kiasi cha Tsh. 22,286,800 kufikia hapo lilipo (Eneo hili liko SNC).

| VIFAA VILIVYO NUNULIWA | KIASI TSH. |
|---|---|
| Ujenzi wa Boma | 7,142,000.00 |
| Mabati Bando 16 | 3,500,000.00 |
| Mbao, Misumari na Kamba za kupimia | 1,090,000.00 |
| Mafundi ujenzi, Maji na Chakula chao | 1,360,000.00 |
| Ujenzi wa Hanamu | 818,000.00 |
| Fundi wa kuezeka | 800,000.00 |
| Plasta, vifaa vya Umeme na Mifuko 6 ya Cement | 1,070,000.00 |
| Mchanga Trip 11 | 450,000.00 |
| Mafundi wa lipu | 550,000.00 |
| Mbao za kenchi | 3,186,800.00 |
| Milango 5 na Madirisha 11 (hizi ni Gril zote) | 1,570,000.00 |
| Gharama za Mlezi wa kundi (M/Mlei Miezi 6 | 750,000.00 |
| **JUMLA** | **22,286,800.00** |

- *Ununuzi wa Eneo* **(Tsh. 7,100,000.00)** *+ Ujenzi wa Jengo la Kanisa* **(Tsh. 22,286,800.00)** *= Jumla kuu* **(Tsh. 29,386,800.00)**

- Kanda ya Magu Mwaka 2017 kijiji cha Chandulu Mtaa wa Ndagalu Wilayani Magu Mkoani Mwanza tulifanya Mahubiri na kubatiza Watu 76. Tulinunua Eneo la ukubwa wa Ekari 1¾ (Moja na Robo Tatu) kwa thamani ya Tsh. 700,000.00, ujenzi wa Msingi wa Kanisa unaendelea. (Eneo hili liko SNC).

- Kanda ya Geita Mwaka 2018 Kijiji cha Kayenze Mtaa wa Butundwe Wilayani Geita, Mkoani Geita Wanawake ambao ni Wake wa Wachungaji (Chama cha Wake wa Wachungaji - Pastors' Spouses SNC) walifanya Mahubiri na kubatiza watu 147 na kununua eneo la ukubwa wa Ekari 1 ¾ (moja na Robo tatu), pia na kujenga Kanisa la ukubwa wa kukaa watu Miatatu (300)
- Kanda ya Mwanza 2019 Mtaa wa Nyakato Kanisa la Kangaye, tulihubiri na kubatiza watu 75 Wilayani Ilemela Mkoani Mwanza na kufanikiwa kununua kiwanja kiasi cha Tsh. 8,000,000.00 kwa sasa ujenzi wa Kanisa unaendelea.
- Wanawake wajasiliamali na Wanataaluma ATAPE kanda ya Jiji la Mwanza, Mwaka 2020 tulihubiri Kijiji cha Nkunguru Mtaa wa Ngudu Wilayani Kwimba Mkoa wa Mwanza na kubatiza watu 208. Pia tulinunua eneo la kujenga Kanisa, kwa sasa Kanisa linaendelea na ujenzi.
- Kanda ya Nkololo Wilayani Bariadi Mtaa wa Nkololo Mkoani Simiyu Mwaka 2021. Tulihubiri na kubatiza watu 126. Pia tulinunua eneo la kujenga Kanisa kwa thamani ya Tsh. 1,500,000.00 mbugani kwa sasa ujenzi unaendelea wa Kanisa.
- Kanda ya Geita Mwaka 2018 Kijiji cha Kakubilo Mtaa wa Bugando Wilayani Geita Mkoani Geita tulihubiri na kubatiza watu 144.
- Kanda yaSengerema Mwaka 2018 Kijiji cha Katwe Kanisa la Mwangika, Mtaa wa Kahunda Wilayani Sengerema, Mkoani Mwanza tulihubiri na kubatiza watu 23.
- Kanda ya Meatu, Wilayani Meatu, Mkoani Simiyu Mwaka 2016, tulihubiri mahubiri ya mlipuko vituo Vinane (8). Mahubiri haya yalikuwa ya AWM NTUC tukabatiza watu 302. Tukasaidia Makanisa Mawili (1) Mwanyahina (2) Bulyanaga Mifuko 20 ya Sementi kwa

kila Kanisa mifuko 10 yenye thamani ya Tsh. 400,000.00 ikiwemo gharama ya usafirishaji.

- Kanda ya Maswa, Mtaa wa Ipililo Kijiji cha Mwakabeya tulihubiri na kubatiza watu 103 kanisa la Mwakabeya.

## 4. MAHUBIRI YA TMI MAGEREZA KWA NJIA YA KUWAFIKIA WAFUNGWA 2016 – 2022.

- Gereza la Butimba Wilayani Nyamagana Mkoani Mwanza, Wanawake waliwafikia Wafungwa na kutoa vitu:- Vitabu, Lesoni, Sabuni, Nguo, Mafuta ya kupaka, Taulo za kike, Chakula na Matunda, Viatu, Nyembe, dawa za meno, Thamani ya Tsh. 11,900,000.00.
- Gereza la Malya Wilayani Malya Mkoani Mwanza, Wanawake wamewafikia Wafungwa na kutoa vitu vifuatavyo: Nguo, Sabuni, Miswaki, Dawa ya meno, Mafuta ya kupaka, Mafuta ya kula Ndoo 1, Kiwi, brash, Vitabu vya Roho ya Unabii 20, Sabato ya kweli 50, Biblia 20, Mipira Miwili ya kuchezea, Majezi ya Timu 2 za Wanaume, King'amuzi 1, Screen 1, Deck 1 na Kanda za Mahubiri ya TMI ya Pr. Mark Finley package yote. Thamani ya vitu vyote ni Tsh. 2,639,900.00
- Gereza la Maswa Wilayani Maswa Mkoani Simiyu. Wanawake wamewafikia wafungwa kwa kutoa Nguo, Sabuni, Mafuta ya kupaka, Vitabu vya Roho ya Unabii 20, Sabato ya kweli 68. Thamani ya vitu vyote ni Tsh. 2,100,000.00
- Gereza la Butundwe Geita, Mkoani Geita, Wanawake tumewafikia wafungwa kama ifuatavyo: Vitabu vya Roho ya Unabii, Biblia, Mafuta, Sabuni, Miswaki, Nguo, Chakula na Matunda, thamani ya Tsh. 891,000.00. Gereza hili kwa sasa liko Field ya NGBF.
- Gereza la Bariadi Wilayani Bariadi Mkoni Simiyu Wanawake tumewafikia Wafungwa kwa kuwapelekea Nguo, Sabuni, Dawa za Meno, Miswaki, Mafuta ya kupaka, Matunda. Thamani ya hivyo vitu ni Tsh.5,700,800.00
- Idara yamkomboa Mwanamke mwenzao Mwadventista kwa kosa la kuabudu siku ya Sabato na kuitunza kama

ilivyo amriwa na Bwana Mungu, na kuhukumiwa kifungo cha Miezi 6 au faini ya Sh. 200,000.00

Jumla ya thamani ya vitu vilivyotolewa ni kiasi cha **Tshs. 23,428,700.00**

## 5. UJENZI NA UKARABATI WA NYUMBA ZA WACHUNGAJI.

Kama Idara ya Huduma za Wanawake, umechangia kusaidia ujenzi wa Nyumba za Wachungaji na kukarabati kama ifuatavyo;

| KANDA | MTAA | KANISA | HUDUMA ILIYOFANYIKA | KIASI TSH. |
|---|---|---|---|---|
| Misungwi | Mwakitolyo | Mwakitolyo | Ujenzi wa Nyumba ya Mchungaji | 3,500,000.00 |
| Maswa | Nyalikungu | Nyalikungu | Ujenzi wa Nyumba ya Mchungaji | 191,000.00 |
| Dutwa | Old Maswa | Old Maswa | Ujenzi wa Nyumba ya Mchungaji | 370,000.00 |
| Itilima | Itilima | Luguru Central | Ukarabati wa Nyumba ya Mchungaji | 779,800.00 |
| Mwanza | Kishiri | Kishiri | Ujenzi wa Msingi wa nyumba ya Mchungaji | 4,370,000.00 |
| Nkololo | Nyangokolwa | Nyangokolwa | Kukamilisha ujenzi wa Choo cha Kanisa | 470,000.00 |
| Nkololo | Nkololo | Nkololo | Ukamilishaji wa Nyumba ya Mchungaji | 700,000.00 |
| **JUMLA** | | | | **10,380.800.00** |

## 6. MAKANISA YALIYO JENGWA NA IDARA YA HUDUMA ZA WANAWAKE SNC KUANZIA 2016 – 2022.

| KANISA | MTAA | KANDA | WAHUSIKA NA KILICHOPO |
|---|---|---|---|
| Nyashigwe | Nyanguge | Jijini Mwanza | Jengo |
| Mbika | Mseki | Kahama | Jengo |
| Mwamoto | Kanadi | Nkololo | Jengo |
| Mwembeni | Kanadi | Nkololo | Jengo |
| Lusaka | Kanadi | Nkololo | Jengo |
| Kayenze | Butundwe | Geita | Shepherdess SNC – Jengo |
| Sayusayu | Maswa | Maswa | AWM JENGO |
| Nkungulu | Ngudu | Mwanza | Wanawake ATAPE Mwanza - Jengo |
| Chandulu | Ndagalu | Magu | AWM – Msingi |
| Mbugani | Nkololo | Nkololo | AWM – ujenzi unaendelea |
| Fumagila | Kishiri | Mwanza | AWM – Jengo |
| Jumla ni Makanisa 11 | | | |

## 7. MAKANISA YALIYO FADHILIWA NA AWM SNC WAKATI WA UJENZI.

1. Mwanyahina: Mifuko ya Sement 10 @ 20,000/= Tsh. 200,000/=
2. Bulyanaga: Mifuko ya Sementi 10 @ 20,000/= Tsh. 200,000/=
3. Mwanzagamba tulichangia Sh. 1,500,000/=
4. Mwambiti tulichangia sh. 1,500,000/= kupitia changizo tulilofanya kwenye Kongamano la 2021 Kanisani Mshikamano tukapata sh. 3,000,000/=. Hii ni Meatu.
5. Mbugani – Nkololo Mifuko ya Sementi 10 @ 20,000/= sh. 200,000/=. Jumla Idara tumefadhili Makanisa 5 Matano kwa kiasi cha Tsh. 3, 610,000/= Mungu atukuzwe.

## 8. MAENEO YA VIWANJA VYA MIRADI VILIVYONUNULIWA NA IDARA YA WANAWAKE – SNC 2016 – 2022.

Idara imefanikiwa kufanya yafuatayo:

- Kanda ya Geita mwaka 2004 Katoro tulinunua eneo la ukubwa wa Ekari 3 kwa kiasi cha Tsh. 35,000.00 Lengo ni kuanzisha kituo cha kulelea Watoto yatima. Kwa sasa kiko Field ya NGBF tangu itengwe. Eneo liko Mkoani Geita Wilayani Geita.
- Kanda ya Bariadi 2016 tulinunua eneo la ukubwa wa Ekari 8 Ngashanda Wilayani Bariadi Mjini Mkoa wa Simiyu kwa Thamani ya Tsh. 3,600,000.00. Lengo ni kuanzisha Shule ya Msingi ya Kiadventista Wa Sabato, eneo tayari limeshapimwa, taratibu za kupewa hati zinaendelea na Mikakati na Mipango ya uchoraji wa Ramani inakamilishwa ili Mikakati ya ujenzi ianze, eneo hili liko SNC.
- Kanda ya Geita Mwaka 2017 tulinunua eneo la ukubwa wa Ekari 6 Kasamwa Wilayani Geita, Mkoani Geita kwa thamani ya Tsh. 3,000,000.00 kwa lengo la kuanzisha kituo cha kulelea Watoto (Dumping Center) kwa sasa kiko eneo la Field ya NGBF tangu Field hiyo itengwe.
- Kanda ya Jiji la Mwanza Mwaka 2019 tulinunua eneo la ukubwa wa ¼ Robo Ekari Nyashigwe kwa Thamani ya Tsh. 3,300,000.00 Mtaani Nyanguge, lengo ni kuwajengea Nyumba ya Makazi ya kuishi Vijana 4 wakiume 3 na wa kike 1 wakiwa ni Walemavu na Wahitaji na Wanawake Kanda ya Jiji la Mwanza wamejitolea kuwahudumia mahitaji yao pindi utakapo kamilishwa ujenzi wa Nyumba hiyo na kuhamia wao watahudumiwa kikamilifu. Pia kwa sasa yule Mhitaji kijana wa kike mmoja alifariki mwaka 2021 Mwezi April baada ya kupatwa na ugonjwa wa Animonia akiwa anakinga maji ya Mvua ili yawasaidie kwa matumizi yao hapo wanapoishi. Eneo hili liko SNC.

### 9. HUDUMA KWA WAHITAJI NDANI YA KANISA KWA NJIA YA UJENZI NA UKARABATI KANDA YA ITILIMA.

Idara ya Wanawake Kanisa la Luguru Ginneri limemjengea Nyumba Mwanamke mmoja Bibi Kizee nyumba ya Matofali ya tope aina ya Slope na kuezeka juu Mabati ya kawaida na gharama yake ni Tsh. 200,000.00 yenye ukubwa wa Chumba kimoja cha kulala na Sebule.

### 10. MAFUNZO YA MASHAMBA DARASA NA BUSTANI ZA JIKONI ZA MBOGAMBOGA.

Idara ilifanikiwa kutuma wajumbe 3 Debora Ngisa, Ellen Mahera na Martha Zacharia ili kupata mafunzo yaliyo tolewa na shirika la ADRA. Wajumbe hawa wamefanikiwa kutoa mafunzo kwa baadhi ya Kanda na Mitaa na Makanisa. Waliofundishwa waliendelea kutoa mafunzo katika Makanisa na kwa watu mbali mbali kama ifuatavyo;

1. **Kanda ya Sengerema**: Wanawake wamefanikiwa kuwa na Bustani zao za jikoni majumbani mwao. Na upande wa mwambao wa ziwa Victoria katika Wilaya ya Buchosa Wanawake kwa Wanaume wamefanikiwa kuwa na mashamba ya Bustani za Mboga mboga na Bustani za jikoni ambazo zinawapatia mapato ya kujikimu katika familia zao.
2. **Kanda ya Bariadi**, Mkoani Simiyu
3. **Kanda ya Geita**, Mtaa wa Nyarugusu.
4. **Kanda ya Jiji la Mwanza**: Idara imefanikiwa katika mafunzo hayo ili watu waweze kujipatia ajira za kujiajiri kwa kilimo cha Bustani za mboga mboga na kujipatia kipato na kubadilisha maisha na mtazmo wa kizamani wa kutothamini mboga za majani kuwa sim lo sahihi katika maisha ya mwanadamu, ambapo ndio mpango sahihi wa Mungu Mwanzo 3:18.

| MTAA | IDADI YA BUSTANI | MATUMIZI |
|---|---|---|
| Sengerema | 18 | Bustani za Jikoni |
| Buchosa | 13 | Bustani za Biashara |
| Nyehunge | 7 | Bustani za Biashara |
| Kahunda | 8 | Bustani za Biashara |
| Ntuzu | 6 | Bustani za Biashara |
| Ntuzu | 18 | Bustani za Jikoni |
| Mwanza | 22 | Bustani za Biashara |
| Mwanza | 80 | Bustani za Jikoni |
| Nyarugusu | 2 | Bustani za Biashara |
| Nyarugusu | 1 | Bustani za Jikoni |

- *Jumla ya Bustani za Jikoni 117 + Jumla ya Bustani za Biashara 58 = Jumla ya Bustani zote ni 175.*

## 11. USAJILI WA MRADI WA CHUO.

Chuo cha Adventist Women Ministry VTC ni Chuo kinachoendeshwa na Idara ya Wanawake SNC kinachotoa mafunzo ya ufundi stadi katika Serikali ya Tanzania. Kilianzishwa mwaka 2004 March kimekuwa kikiendelea kutoa mafunzo yake bila usajili kwa miaka kadhaa, lakini ilipofika mwaka 2016 ndipo taratibu za usajili zilianza rasmi hatua moja baada ya nyingine mpaka kufikia usajili kamili. Hatua za usajili ni kama ifuatavyo:

- Kibali cha kuendelea kuendesha mafunzo (Barua).
- Application for Preliminary Registration No. VETA/MZ/AC/110/V0L/V/25 (Cheti cha majaribio).
- Certificate of Preliminary Registration (Cheti cha Matazamio) No. VET/MZA/PR/2017/C/064.
- Certificate of full Registration (Cheti cha kudumu) No. VET/MZA/FR/2020/C/098

## 12. SEMINA.

Idara imefanikiwa kufanya semina 1552 kwa kipindi hiki cha Miaka Sita.

## 13. KUGAWA KANDA.

Tuligawa Kanda 10 ili kurahisisha utendaji kazi kama ifuatavyo;

- Kanda ya Mwanza.
- Kanda ya Magu.
- Kanda ya Misungwi.
- Kanda ya Busega.
- Kanda ya Dutwa.
- Kanda ya Nkololo.
- Kanda ya Bariadi.
- Kanda ya Itilima.
- Kanda ya Maswa.
- Kanda ya Meatu.

MWISHO WA TAARIFA NA MUNGU AWABARIKI.

## MIPANGO KAZI YA IDARA YA WATOTO

1. Kugawa Kanda ili kurahisisha kuwahudumia watoto na kuwafikia kiurahisi tuligawa kanda 10 ambazo ni:
    - Kanda ya Mwanza
    - Kanda ya Magu
    - Kanda ya Misungwi
    - Kanda ya Busega
    - Kanda ya Dutwa
    - Kanda ya Nkololo
    - Kanda ya Bariadi
    - Kanda ya Itilima
    - Kanda ya Maswa
    - Kanda ya Meatu.
2. Watoto wawe na Sare za Idara ya Watoto.
3. Mahubiri ya Idara ya Watoto kwa njia ya Satelite yaliyorushwa toka Union ya Kusini Dar es salaam.
4. Mahubiri ya hadhara.
5. Kuwafikia Watoto walio kwenye mazingira magumu



## MIPANGO & MALENGO YA IDARA: UTEKELEZAJI

## MAHUBIRI

- Mahubiri ya Idara ya Watoto kwa njia ya Satellite toka Division ya ECD yaliyo fanyika kwa muda wa wiki mbili, tulikuwa na vituo viwili: Mabatini Kanisani na Buhongwa Kanisani.
- Tulifanikiwa kualika, na mahudhurio yalikuwa ni watu 1682 wastani wa kila siku walihudhuria watu 120 wakubwa kwa watoto katika kituo cha Mabatini.
- Kituo cha Buhongwa kanisani mahudhurio kwa ujumla ni 1281 ni sawa na wastani wa watu 91 kwa siku. Hatukufanikiwa kubatiza mwisho wa hayo mahubiri kwa sababu ya Semina za Kichungaji.
- Wachungaji wa Mitaa walikuwa Singida. Mahubiri ya hadhara yaliyofanyika kanda ya Jiji la Mwanza Kanisa la Nyamanoro walihubiri Watoto wenyewe kwa muda wa wiki Tatu na kubatiza watu 38 eneo la nyasaka Msumbiji Sokoni, kwa sasa limeshatengwa kuwa Kanisa liitwalo Nyasaka Msumbiji.
- Katika mahubiri ya Satellite yaliyofanyika katika uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, Mwezi May 2018 Watoto walishiriki kufanya program za Watoto, walionyesha safari ya Wana wa Israel walivyo zunguka jangwani muda wa Miaka Arobaini na pia Watoto walifanya halaiki ikionyesha Kanisa la Waadventista wa Sabato linatangaza injili kwa aina tatu:
    - Injili – Kanisa
    - Elimu – shule
    - Uponyaji – Hospitali
- Mahubiri ya hadhara Kanda ya Kahama Watoto Sita walisimama kuhubiri katika eneo la Kanisa la Nyasubi kwa muda wa wiki tatu na kufanikiwa kubatiza watu 66 ndani yake walio batizwa waliokuwa na umri wa miaka 13 – 14 walikuwa 14 na watu wazima walikuwa 52.

- Mahubiri ya hadhara Kanda ya Kahama Kanisa la Segese tulifanikiwa kuhubiri na kubatiza watu 47. Kwa sasa eneo hilo liko NGBF.
- Hivyo jumla ya watu walio batizwa kwenye mahubiri ya Idara ya Watoto ni 151 Mungu atukuzwe sana.



## KUWAFIKIA WATOTO WALIO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU

- Kanda ya Kahama mjini, tulikwenda katika kituo kimoja cha kulelea Watoto na kutoa msaada wa Sabuni, Sukari, Mafuta, Nguo, Viatu, Mwanasesere (Mdori) mmoja, Mchele kilo 30, Sabuni za unga, Biblia, Lesoni za Watoto 6 Vitabu vya nyimbo za Kristo vidogo 10 na pesa tasilimu sh. 75,000/=. Thamani ya vitu vyote na pesa tasilimu ilikuwa sh. 350,000/=, pesa hizi walichanga Watoto wenyewe na kupeleka kama moja ya Sadaka.
- Kuwafikia Watoto wa mazingira magumu kwa njia ya kuwaalika kuja Kanisani kuabudu nao. Kanisa la

Nyamanoro Mtaa wa Nyamanoro, Idara ya Watoto ilialika Watoto walioko kwenye kituo cha FTK cha kulelea Watoto kuja kuabudu nao na kula chakula nao kisha kuwapa vifaa vya mahitaji yao thamani ya Sh. 150,000/= kama vile Sabuni nk.

- Kanisa la Kirumba Idara ya Huduma za Watoto kila Sabato huenda kutoa huduma za kiroho na kimwili katika kituo cha TFK mahali wanapolelewa watoto walio kuwa katika mazingira magumu kama vile neno la Mungu, Chakula cha pamoja na mahitaji mbali mbali.



## MAKONGAMANO.

- Makongamano matatu (3) ya Idara ya Watoto Union ambalo moja lilifanyika Kahama katika Shule ya Mingas lililo husisha Walimu wa Idara ya Watoto, Viongozi wa VBS na Shule Sabato ya Watoto. La pili lilifanyika Nyegezi Kanisani Mwanza. Katika makongamano hayo mawili jumla ya Waalimu 151 walihitimu mafunzo ya uongozi ngazi ya kwanza na ya pili (I-II). Kongamano la Tatu lilifanyika Singida Ititi lililo husisha Watoto wenye Vipawa Maalumu ili kutiwa moyo waendeleze kukuza vipawa vyao na kujifunza nyimbo za Watoto na namna ya kuziimba kwa sauti zake. Jumla ya wajumbe waliohudhuria ni 1295.

- Semina za Walimu wa Idara ya huduma za Watoto kikanda na kimitaa zikihusisha pia Shule Sabato Watoto, VBS na pia Madarasa ya Watoto yapaswavyo kuandaliwa na utengenezaji wa vifaa au zana za Watoto. Tumefanikiwa kuendesha semina za Idara 802 Ki-kanda, ki-Mitaa na ki-Makanisa.

## MACHANGIZO.

Machangizo Mawili (2) yalifanywa na Idara ya Watoto ili kusaidia ujenzi wa kituo cha Mvuto Ititi Singida na ujenzi wa Kanisa la Mbugani Nkololo.

i. Kituo cha Mvuto Singida Ititi ni kiasi cha Sh. 108,550/=
ii. Kanisa la Mbugani Mtaa wa Nkololo kiasi cha sh. 46,400/=

Jumla Idara ya Watoto tumechangia kusaidia kazi ya Mungu kiasi cha Tsh. 154,950/=

*Mwisho wa Taarifa, Mungu awabariki.*

# TAARIFA YA IDARA YA ELIMU, UHURU WA DINI NA MAMBO YA KIJAMII.



**MWL. ISAACS MANYONYI**

MKURUGENZI WA IDARA
YA ELIMU, UHURU WA DINI
NA MAMBO YA KIJAMII.





MKUTANO MKUU WA NANE WA SNC (SESSION)
SEPTEMBA 22, 2022.

# IDARA YA ELIMU

## UTANGULIZI

Ninawashukuruni nyote kwa kadri tulivyoshirikiana katika kulisukuma gurudumu la kazi ya Bwana tangu mwaka 2016 hadi 2022 kwa mafanikio makubwa.

## MIPANGO YA IDARA 2016-2022.

1. Kuboresha taaluma katika taasisi/shule za Kanisa.
2. Kubadilisha na kuboresha taswira katika taasisi za elimu za kanisa-kuboresha miundombinu na majengo kama vile madarasa, mabweni, maktaba, mabwalo ya chakula,maabara, majengo ya ibada, nyumba za walimu, huduma za maji, huduma za umeme na vifaa vya ofisi
3. Kuongeza ufaulu daraja la kwanza na la pili Shule za sekondari
4. Kuhimiza na kuwezesha watumishi wa Kanisa kujiendeleza kitaaluma.
5. Uinjilisti: mkakati wa shule (walimu na wanafunzi) kushiriki TMI.
6. Kufanya semina za Idara ya elimu katika Makanisa, Mitaa na Kanda.
7. Kuanzisha shule za msingi za kanisa jiji la Mwanza na Mkoa wa Simiyu.
8. Kuhamasisha ujenzi wa shule za chekechea na Daycare Centres katika makanisa.
9. Kuwa na gazeti la idara ya Elimu litakalowafikia washiriki, ambao watapata taarifa za maendeleo ya shule za Kanisa kupitia gazeti hilo.

## MIPANGO & MALENGO YA IDARA-UTEKELEZAJI: -

- Tumeendelea kusisitiza na kuhimiza ujenzi wa shule za chekechea na Day care centres. Idara inatoa pongezi kwa makanisa na mitaa ambayo imeanzisha na kuendesha vituo hivi; Shamaliwa, Sayuni, Nyakato, Nyamanoro, Pasiansi, Buzuruga, Matongo, Kisesa, Ngulyati, Buhongwa, Kishiri, Bukaga, Mashiri, Mabatini, Majengo, Meatu, Mshikamano, Migato, Majengo Meatu,Nyakato, Majengo-Kidinda, Ngulyaati, Itubilo, Kirumba, Ntuzzu, Buswelu, Igombe, Nyegezi, Jerusalemu- Matongo, Sapiwi Nursery School, Igegu Nusery-Dutwa.




*Picha 1: Wanafunzi wa Day Care Centre ya kanisa la Nyakato.*

- Mitihani ya Biblia kwa Wanafunzi wa darasa la saba na kidato cha nne, Waadventista wa Sabato imeanzishwa tangu mwaka 2019. Imeongeza chachu ya ufundishwaji wa vipindi vya dini na usomaji wa Biblia.

- Teachers Conventions zimefanyika, kule Shinyanga Kanisa la Waadventista wa Sabato Lubaga, Walimu 116 walihudhuria toka Makanisa mbalimbali-2016, Rwanda Gahogo school-2017, Kitungwa, Morogoro 2018, na zile za ndani ya Conference-Pasiansi-2020, Ngulyati-2021 na Lamadi-2022.
- Teachers Convention iliyofanyika kule Gahogo School, Rwanda, Walimu 32 walihudhuria – 2017.
- Teachers Convention iliyofanyika Kitungwa Adventist Secondary School 2018, walimu 18 walihudhuria toka South Nyanza Conference.
- Progam za kubadilisha taswira katika tasisi zetu, Pamoja na kuboresha mazingira zimefanyika, ikiwa ni Pamoja na mabweni, mageti, Kampasi za shule na madarasa.
- Matokeo ya mitihani kidato cha nne na cha sita kwa wastani shule zetu zimefanya vizuri.
- Miongozo ya idara ya elimu kwa ajili ya waratibu wa elimu makanisani imeandaliwa.
- Idara imeandaa na kuchapisha kitabu kidogo kwa ajili ya walimu Waadventista, kitabu sasa kiko mikononi mwa walimu Waadventista katika shule zetu.
- Watumishi wapatao 36 wamejiendeleza katika ngazi za Diploma, Shahada ya kwanza uzamivu na hata umahiri. Watumishi hawa wamejiendeleza katika vyuo mbalimbali ikiwa ni Pamoja na Bugema Universtity, Adventist University of Africa, University of Arusha.
- Semina za idara ya Elimu zimefanyika katika Makanisa na Mitaa pamoja na kanda. Baadhi ya mitaa ilipofanyika semina ni Nyakato, Kirumba, Butimba, Lagangabilili, Itilima, Maswa, Meatu, Dutwa, Buhongwa, Bwanga, Pasiansi, Igelegele, Igoma, Isamilo, Nyanguge, Migato, Ngulyati, Nera, Buswelu, Buzuruga, Lamadi.

- Kuanzishwa kwa shule ya msingi Bupandagila Adventist English Medium, na sasa imetoa zao la pili la darasa la saba.
- Huduma za maji sasa zinapatikana kwa shule zote tatu baada ya zoezi la kuchimba visima kufanyika. Walianza Bupandagila, Ngulyati wakafuata na hatimaye Nyanza. Huduma hii ya maji imeongeza utulivu na kusaidia huduma zingine kufanyika kwa uzuri.
- Huduma za kiroho; ubatizo ulivyofanyika

| SHULE | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BUPANDAGILA | 80 | 121 | 129 | 84 | 100 | 140 | 26 |
| NGULYATI | 26 | 48 | 116 | 97 | 115 | 66 | 174 |
| NYANZA ADVE | 128 | 132 | 78 | 227 | 60 | 64 | 52 |
| JUMLA | 234 | 201 | 323 | 408 | 275 | 270 | 252 |

## UFAULU KITAALUMA

BUPANDAGILA SECONDARY SCHOOL

| MWAKA | I | II | III | IV | 0 | % | N/W* | N/M* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 5 | 24 | 46 | 7 | 0 | 82 | 4/75 | 273/3280 |
| 2017 | 5 | 21 | 42 | 13 | 0 | 81 | 4/68 | 306/3039 |
| 2018 | 5 | 13 | 25 | 5 | 0 | 48 | 5/70 | 314/3488 |
| 2019 | 8 | 27 | 28 | 2 | 0 | 65 | 5/100 | 294/3908 |
| 2020 | 18 | 23 | 9 | 0 | 0 | 50 | 3/116 | 196/3956 |
| 2021 | 12 | 19 | 13 | 1 | 0 | 45 | 5/123 | 326/4141 |

NYANZA ADVENTIST SECONDARY SCHOOL

| MWAKA | I | II | III | IV | 0 | % | N/W* | N/M* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 2 | 33 | 35 | 15 | 0 | 85 | 21/218 | 284/3280 |
| 2017 | 16 | 39 | 35 | 5 | 0 | 95 | 16/220 | 153/3039 |
| 2018 | 23 | 36 | 7 | 0 | 0 | 66 | 10/241 | 105/3488 |
| 2019 | 31 | 65 | 36 | 5 | 0 | 137 | 19/246 | 218/3908 |
| 2020 | 37 | 54 | 34 | 4 | 0 | 129 | 20/242 | 283/3956 |
| 2021 | 34 | 34 | 23 | 6 | 0 | 97 | 28/246 | 315/4141 |

NGULYATI SECONDARY SCHOOL

| MWAKA | I | II | III | IV | 0 | % | N/W* | N/M* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 0 | 7 | 14 | 25 | 0 | 46 | 8/75 | 519/3280 |
| 2017 | 0 | 10 | 19 | 11 | 0 | 40 | 6/68 | 391/3039 |
| 2018 | 2 | 16 | 14 | 12 | 2 | 44 | 6/70 | 435/3488 |
| 2019 | 3 | 14 | 12 | 6 | 0 | 35 | 3/50 | 109/1011 |
| 2020 | 6 | 20 | 11 | 4 | 0 | 41 | 6/116 | 377/3956 |
| 2021 | 3 | 22 | 10 | 2 | 0 | 37 | 4/31 | 154/854 |



*Picha 2: Watumishi wa shule ya Sekondari Ngulyati pamoja na viongozi wa Conference.*

## CHANGAMOTO.

1. Bado yapo makanisa ambayo hayahudumii wanafunzi nashuleni katika vipindi vya dini. Wanafunzi hujihudumia wenyewe au kuchanganywa na madhehebu mengine.
2. Kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa kiwanja kwa gharama sahihi, katika viunga vya mji wa Mwanza, na kusababisha lengo hili kutotimia.




ADMINISTRATION

# IDARA MAMBO YA JAMII NA UHURU WA KIDINI.

## SHUGHULI ZA IDARA YA MAMBO YA JAMII NA UHURU WA KIDINI.

- Kudumisha mawasiliano na viongozi wa taaasisi za kidini, serikali na mashirika mengine na kulitambulisha kanisa kwa taasisi hizo. Makanisa mengi wakishirikiana na wachungaji wamejitahidi kufanya mawasiliano na viongozi wa serikali ikiwa ni Pamoja na kuwaalika katika program zetu za kanisa kama vile ujenzi wa makanisa, makambi na mikutano mingine ya kanisa.
- Kutetea, kutoa mwongozo na mashauri na kuwasaidia wale wote wanaonyimwa fursa ya kuabudu na kuonyesha Imani yao
- Kutangaza, kuhimiza na kulinda zawadi aliyoitoa Mungu ya Uhuru wa Dini ambayo ni sehemu ya wajibu wetu wa kiunabii kama Waadventista wa Sabato na Msingi wa Kufanya uinjilisti.

## YALIYOFANYIKA.

Semina za Idara ya Mambo ya Jamii na Uhuru wa Kidini zimefanyika katika makanisa na mitaa ifuatayo: -

- Kirumba, Shamaliwa
- Migato, Nassa, Nyakato, Buswelu, Ntuzu, Misungwi.
- Isamilo, Maswa, Sola, Buzuruga, Buhongwa
- Ipililo, Isamilo, Gasuma, Magu, Old Maswa, Kishiri,
- Ngulyati, Kwimba, Buhungukila
- Dutwa, Lagangabilili, Migato.

**Mambo kumi ya Jamii yaliyojitokeza na kuifikia Ofisi na kuwekwa kama Kumbukumbu.**

1. Mwanafunzi (Binti) aitwaye Pendo Ntemi Kisuge wa Kijiji cha Mwaumatondo, Kata ya Mwaumatondo, Tarafa ya Nkololo kwa sababu ya kuipokea imani alipigwa na Mzazi, na hatimaye kufukuzwa nyumbani. Alikimbilia kwa mshiriki, Mzee wa kanisa na hatimaye akapata hifadhi kwa Mchungaji wa Mtaa. Hatimaye yuko Nyanza Sekondari Kidato cha Kwanza. (2020)
2. Mwezi March 2019, Mama Wande Paul wa Kijiji cha Luhala, Kata ya Mwankulwe, Mtaa wa Malya. Alifungwa jela miezi sita baada ya kushindwa kulipa fedha alizodhaminiwa kulipa faini kwa kuzuia binti yake asiende kupiga picha za darasa la saba siku ya Sabato. Idara iliwasiliana na wanawakike ambao walichangia Sh 100,000 chini ya Mama Martha Zakaria, na hatimaye Mama huyu alitoka jela baada ya kutumikia kifungo kwa wiki moja. Kesi bado iko mahakamani; inaendelea Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ngudu, TAKUKURU Na Polisi vimehusishwa katika kesi hii, ambayo ilikuwa na harufu ya rushwa, uvamizi wa viongozi wa kijji katika ibada, na kubadilisha kesi kutoka kesi ya jinai na kuwa kesi ya madai.
3. Mwanafunzi katika chuo cha utabibu 2017 Sengerema, aliyefanyiwa hila za kufukuzwa chuoni na kufutwa jina lake katika orodha ya watahiniwa wa mitihani ya mwisho ya Taifa kwa kuwa hakuwa amehudhuria vipindi vilivyofanyika siku ya Sabato. Kesi hii ilifikishwa hadi kwa Katibu mkuu wa wizara ya afya na kwa mshangao wa wengi(wanafunzi na uongozi wa chuo) mwanafunzi huyu aliruhusiwa kufanya mtihani kwa maelekezo kutoka wizarani jambo ambalo lilileta ushindi kwa kijana na kanisa kwa ujumla kwa namna mbingu zilivyoingilia kati

4. Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Simiyu kulazimishwa kukimbia mchakamchaka siku ya Jumamosi. Wanafunzi wawili walirundishwa nyumbani kwa kukaidi zoezi hili. Baada ya mawasiliano na Afisa Elimu wa Wilaya ya Bariadi walirudishwa shuleni kuendelea na masomo na kufanya mtihani wa Taifa.
5. Binti (Jina tunalihifadhi) wa Dutwa alilazimishwa kuolewa na Mwanaume asiye Mwadventista. Baada ya Mashauri kwa Mama Mzazi, huku taarifa zikipelekwa Polisi na ofisi ya Mkuu wa Mkoa Simiyu, Binti aliachwa huru.
6. Wanafunzi wa shule ya msingi, Mtaa waMwagala 2016, Waadventista wapatao 13 walichapwa viboko visivyokuwa na idadi kwa kuwa hawakwenda shuleni kufanya usafi siku ya Jumamosi. Suala hili lilifikishwa kwa mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya ya Maswa na kushughulikiwa na Afisa Elimu wa wilaya na wahusika waliomba radhi na kuonyesha ushirikiano mzuri na jambo hilo likaisha
7. Mwaka 2020, Wanafunzi wanaosoma kozi za utabibu Chuo cha Tandabui, Saba walipangiwa kufanya mitihani yao Practical siku ya Sabato na kutishiwa kurudia mwaka. Tunashukuru, kasheshe hiyo ilipita baada ya maridhiano na uongozi wa shule, waliruhusiwa kuifanya mitihani hiyo siku nyingine.
8. Baadhi ya washiriki wa Nera,2017 Kijiji Mbarika walizuiliwa kuchota maji katika kisima walichochimba wenyewe kwa sababu ya mambo ya dini na wivu. Habari zilienea kwamba kiliwekwa sumu. Hakukuwa na maafa yoyote yaliyotokea. Uongozi wa mambo ya jamii na uhuru wa dini ulifika kijijini hapo. Baadaye uongozi wa serikali ulikaa na pande zote mbili na jambo hilo likaisha.

9. Washiriki wawili wa Kijiji cha Mbarika walitulijwa/walitengwa na kijiji kwa kuwa hawakuandamana na wenzao kwenda kwa mganga kuleta mvua. Hata walipopigwa faini ya 20,000/= hawakutoa. Mwenyekiti wa chama cha uhuru wa dini alionana na uongozi wa Kijiji (mwenyekiti wa Kijiji na mtendaji) baadaye aliachiwa huru.
10. Washiriki katika mtaa wa Kanadi walisumbuliwa na sungusungu na kuchukuliwa vitu vyao, kesi ilienda hadi polisi na kurudishiwa baadhi ya vitu walivyochukuliwa

Kesi zingine zinazo husiana na Mambo ya Jamii na Uhuru wa Dini, Zilimalizika huko makanisani chini ya Wachungaji ambao ndio wenyeviti wa chama cha kutetea uhuru wa Dini katika makanisa mahalia.




*Pichani:Mama aliyefungwa jela, baada ya kutoka gerezani: Mchungaji wa Malampaka, Mchungaji wa Ngudu, Mkurugenzi wa Mambo ya jamii na uhuru wa dini na wazee wa kanisa*

**Mambo Ya Jamii wa Uhuru wa Kidini.**
Miaka ya 2020-2021 hatukuwa na matukio mengi yaliyojitokeza kuhusu uhuru wa dini.

Mara kwa mara kulijitokeza changamoto kwa Wanafunzi wanaosoma chuo cha Tandabui kupangiwa ratiba ya mtihani siku ya Jumamosi. Tuliongea na uongozi wa chuo na wakabadilishiwa ratiba.

## UTANGULIZI.

Ndugu wajumbe wa Mkutano Mkuu, nawasalimu katika Jina la Mwokozi wetu Yesu Kristo. Tunamshukuru Mungu kwa ulinzi na mibaraka aliyotukirimia tangu mwaka 2017 hadi leo tunapokutana, Jina la BWANA litukuzwe. Napenda kuwapatia taarifa fupi ya maendeleo ya shule yetu ya Bupandagila Sekondari.

## IDADI YA WANAFUNZI.

| MWAKA | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| IDADI | 387 | 360 | 312 | 242 | 228 | 235 |

## IDADI YA WAFANYAKAZI NA SIFA ZAO ZA KITAALUMA.

| TYPES OF WORK | G | D | C | F VI | F IV | S VII | T |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| TEACHERS | 12 | 04 | 00 | 00 | 00 | 00 | 16 |
| ACCOUNTANTS | 02 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 02 |
| CLINICIAN | 00 | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| LAB. ASSISTANT | 00 | 00 | 01 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| NURSES | 00 | 02 | 00 | 00 | 00 | 00 | 02 |
| SECRETARIAL | 00 | 00 | 01 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| DRIVER | 00 | 00 | 01 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| COOKS | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 02 | 02 |
| WATCHMEN | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 | 03 | 04 |
| S/KEEPER/LIBRARIAN | 00 | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| OFFICE ATTENDANT | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 | 01 |
| MATRON/PATRON | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 |
| IT | 00 | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| **TOTAL** | **14** | **09** | **03** | **00** | **01** | **06** | **33** |

*G – Graduate, D – Diploma, C – Certificate, F VI – Form Six, F IV – Form Four, S VII – Standard Seven, T - Total.*

## MALENGO.

KITAALUMA:
Kitaaluma tumeazimia kuboresha taaluma ya shule yetu kwa ufaulu wa alama za A, B na C.

**Mikakati**:
- Kumfanya Mungu kuwa wa kwanza.
- Kufanya mitihani ya shule zisizo za Serikali Mkoa wa Simiyu na Zone A kwa kufanya mitihani ya kujipima kwa vidato vya mitihani.
- Kujenga uwezo wa wanafunzi katika masomo ya Sayansi na Hisabati.
- Kuwajengea wanafunzi uwezo wa kujiamini na kuwa waaminifu pale wanapofanya mitihani yao.
- Kuendesha mazoezi ya wiki, mitihani ya mwezi, muhula na ya mwisho wa mwaka.
- Kufanya ziara za kitaaluma (study tours).
- Kuwa na zana na vifaa bora vya kufundishia za kutosha mahitaji ya shule.
- Kutilia mkazo wanafunzi kuzungumza lugha ya kiingereza.
- Kutoa motisha kwa walimu na wafanyakazi wasio walimu.
- Kuhamasisha, kusimamia taaluma na kuhimiza walimu kumaliza muhtasari (syllabus) mapema ifikapo au kabla ya mwezi Juni kwa madarasa ya mitihani na mwezi Septemba kwa madarasa mengine.
- Kuhimiza na kushiriki katika michezo mbalimbali ili kuimarisha afya ikijumuisha afya ya akili.
- Kuwa na program za kuwafundisha wanafunzi masomo ya ziada kwa nyakati za asubuhi saa 11:00-12:15 na alasiri saa 09:30-10:50.

- Kuondoa daraja la 3 na 4 katika mtihani wa Taifa kwa kidato cha pili, nne na sita kwa kuwafanya wanafunzi kupata madaraja ya 1 na 2 tu.
- Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanafaulu kwa kupata gredi A na B tu katika kila somo kwa kidato cha pili na nne na gredi A, B na C tu kwa kidato cha sita.
- Kufanya tathmini kila baada ya matokeo kutoka ili kubaini vikwazo vya kitaaluma na kuvitatua.
- Kuanzisha na kusimamia ipasavyo klabu mbalimali za masomo na kuhimiza Idara za masomo mbali mbali kufanya kazi zake kikamilifu.
- Kusajili kituo cha QT na cha watahiniwa wa kujitegemea.
- Kusajili somo la LITERATURE IN ENGLISH ili kupanua wigo wa ufaulu shuleni.

## MALEZI NA HUDUMA:

Katika malezi na huduma tumeazimia kuwa na malezi bora kwa wanafunzi hasa katika kuwafudisha kuwa na mwenendo mzuri na tabia njema inayoakisi sura ya Mungu katika maisha yao.

**Mikakati:**

- Kukuza na kuendeleza tabia bora ya wanafunzi ili kuwawezesha kuwa na amani na utulivu shuleni.
- Kuwawezesha wanafunzi kuhudhuria mikutano mbali mbali ya kiroho na maombi ya kila siku kulingana na ratiba ya shule na kanisa.
- Kukuza na kuendekeza nidhamu bora kwa wanafunzi.
- Kuhimiza wanafunzi kujenga tabia ya kujiamini nakujitawala kwa kufuata maadili mema.
- Kuwapatia wanafunzi huduma bora za chakula, malazi, umeme, usafri na huduma za afya.

- Kuonya kwa upendo wanafunzi wote wanaokwenda kinyume cha taratibu na kanuni za shule.

## UZALISHAJI MALI:

Tumeazimia kuwa na miradi ambayo itatusaidia kuongeza kipato

**Mikakati:**

- Kukusanya ada kwa wakati pamoja na kuinua na kuendeleza miradi ya uzalishaji mali hususani.
- Bustani kwa ajili ya kuzalisha mboga na matunda kwa ajili ya wanafunzi na wafanyakazi.
- Kuwa na mradi wa upandaji wa miti ya matunda.
- Kuwa na mradi wa ufugaji wa nyuki katika msitu wa shule

## MIUNDOMBINU:

Tumeazimia kujenga uwezo zaidi katika suala la miundo mbinu.

**Mikakati:**

- Kufanya ukarabati wa miundo mbinu ya shule.
- Kutengeneza barabara inayoingia shuleni (Nyakabindi - Bupandagila) kwa kushirikiana na mamlaka za serikali kama Halmashauri ya mji wa Bariadi na mkoa.

## UBORESHAJI WA MAZINGIRA:

Tumeazimia kuyafanya mazingira yetu kuwa bora zaidi kwa wanafunzi na wafanyakazi kwa ujumla:

**Mikakati:**

- Kupanda miti hasa ya matunda ndani ya eneo la shule.
- Kuboresha mwonekano wa mazingira yetu kwa kupanda maua.
- Kufanya usafi wa mazingira yetu ipasavyo.

## MICHEZO:
Tumeazimia kukaza fani za michezo mbalimbali ili kuimarisha ukakamavu, burudani, urafiki na mshikamano kwa watumishi na wanafunzi wetu.

**Mikakati:**
- Kuwa na ratiba ya michezo na kuifuata.
- Kununua vifaa vya michezo mfano jezi na mipira.
- Kuendelea kuboresha viwanja vya michezo.
- Kuimarisha mchakamchaka shuleni.
- Kuimarisha mashindano ya michezo shuleni (darasa kwa darasa, wanafunzi kwa watumishi) na michezo ya shule za nje.

## AFYA:
Tumeazimia kuendelea kutoa huduma bora za afya kwa jamii ya shule hasa wanafunzi wetu kwa kuwapatia chakula bora, malazi bora na kuwapatia matibabu pale wanapougua.

**Mikakati:**
- Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanakula chakula bora.
- Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanalala mahali safi na salama.
- Kuimarisha huduma katika zahanati ya shule yetu.
- Zahanati yetu kutoa huduma ya bima ya afya.

## RASILIMALI WATU:
Tumeazimia kuwa na wafanyakazi wa kutosha wenye sifa thabiti katika maeneo husika.

**Mikakati:**
- Kuajiri wafanyakazi wenye sifa stahiki katika kila eneo.

## MAMBO YA KIROHO:

Tumeazimia kuwafanya wanafunzi na watumishi kudumisha maisha ya kiroho kama yalivyo malengo ya uanzishwaji wa shule hii.

**Mikakati:**

- Kuwa na ibada mbalimbali kulingana na ratiba ya shule na kanisa na kuwa na program kabambe na semina mbalimbali zinazohusu mambo ya kiroho.
- Kuwa na mikutano ya makambi na majuma ya kusisitiza mambo ya kiroho shuleni.

## UTEKELEZAJI/MAFANIKIO:

### TAALUMA:

**Matokeo Ya Mitihani Ya Taifa:**

| KIDATO | | Madaraja (Divisions) | | | | | Jumla | Wilaya | Mkoa | Kitaifa | % I-III | % IV | Ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | 0 | | | | | | | |
| II | 2016 | 19 | 26 | 25 | 21 | - | 91 | 3/15 | - | - | 77 | 23 | - |
| | 2017 | 26 | 30 | 18 | 11 | - | 91 | 2/15 | - | - | 88 | 12 | 11% |
| | 2018 | 33 | 15 | 12 | 7 | - | 67 | 1/16 | - | - | 86.6 | 10.4 | -2% |
| | 2019 | 16 | 12 | 13 | 05 | - | 46 | 2/16 | - | - | 89.1 | 10.9 | 0.3% |
| | 2020 | 13 | 10 | 10 | 07 | - | 40 | 2/16 | - | - | 82.5 | 17.5 | -7% |
| | 2021 | 20 | 3 | 5 | 3 | - | 31 | 2/16 | - | - | 90.3 | 9.7 | 08% |
| IV | 2016 | 5 | 24 | 46 | 7 | - | 82 | 1/15 | 4/ 175 | 273/3280 | 91 | 8.5 | 1.2% |
| | 2017 | 5 | 21 | 42 | 13 | - | 81 | 2/15 | 4/ 168 | 306/3039 | 84 | 16 | -8% |
| | 2018 | 5 | 13 | 25 | 5 | - | 48 | 2/16 | 5/ 70 | 314/3488 | 90 | 10 | 38% |
| | 2019 | 08 | 27 | 28 | 02 | - | 65 | 2/16 | 5/100 | 294/3908 | 97 | 3 | 7% |
| | 2020 | 18 | 23 | 09 | - | - | 50 | 2/16 | 3/ 116 | 196/3956 | 100 | 100 | 18% |
| | 2021 | 21 | 19 | 13 | 1 | - | 45 | 2/16 | 5/123 | 326/4141 | 97 | 2.2 | 2.2 |
| | 2016 | - | 2 | 9 | - | 1 | 12 | 1/1 | 2/2 | 104/ 117 | 90 | - | -3% |
| | 2017 | - | 6 | 3 | - | - | 9 | 1/1 | 3/3 | 69/146 | 100 | - | 30% |
| | 2018 | 5 | 6 | 8 | - | - | 19 | 1/1 | 1/1 | 37/127 | 100 | - | 37% |
| | 2019 | 05 | 13 | 07 | - | - | 25 | 1/1 | 1/1 | 44/134 | 100 | - | 21% |
| | 2020 | 01 | 13 | 09 | - | - | 23 | 1/1 | 1/1 | 82/176 | 100 | - | -17% |
| | 2021 | 5 | 9 | 1 | - | - | 15 | 1/2 | 2/2 | 41/190 | 100 | - | 41% |

- Tumefanikiwa kununua vitabu vya kiada na ziada vya kufundishia na kujifunzia na kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la uhaba wa vitabu ili kufikia malengo ya kitaaluma tuliojiwekea. Aidha bado tunaendelea kununua vitabu vingine ili kufikia lengo la mwanafunzi mmoja kitabu kimoja.
- Pia tumefanikiwa kununua vifaa mbalimbali vya maabala ili kuwezesha masomo kwa vitendo kwa masomo ya sayansi. Hii imewezesha walimu kufundisha masomo haya kwa vitendo kwa wakati na wanafunzi kufanya mazoezi na ya mara kwa mara.
- Shule imefanikiwa kuwafundsha wanafunzi masomo ya ziada asubuhi saa 11:00-12:15 na alasiri saa 09:30-10:50.
- Vilevile tumefanikiwa kusajili kituo cha QT kwa kidato cha pili na cha watahiniwa wa kujitegemea yaani PC kwa kidato cha nne.
- Tumefanikiwa kusajili somo la LITETATURE IN ENGLISH ili kupanua wigo wa ufaulu shuleni. Mungu wetu atukuzwe.



## MIUNDO MBINU:
Katika eneo hili tumefanikiwa kufanya yafuatayo:

- Kukarabati miundo mbinu iliyopo hususani madarasa, mabweni na nyumba za watumishi.
- Ufuatiliaji wa matengenezo ya barabara toka Nyakabindi hadi shuleni kwa mamlaka zinazohusika serikalini.

## UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA SHULE:

- Tumefanikiwa kupanda miti katika eneo la shule na tunaendelea kupanda.
- Tunaendelea kuboresha usafi wa mazingira ya shule kwa kufanya ukaguzi wa mazingira yote kwa ujumla kila Ijumaa asubuhi saa 01:30 -02:00.

## MICHEZO:
Tumeendelea kukuza fani za michezo mbalimbali shuleni kwa kufanya yafuatayo:

- Kuwa na ratiba ya michezo kila Alhamisi na Jumapili na inafuatwa.
- Tumenunua vifaa vya michezo mfano mipira mipya kumi.
- Tumeendelea kuboresha viwanja vya michezo.
- Tumeimarisha mchakamchaka kila Jumapili asubihi saa 12:00-01:30.
- Tunaendelea kuimarisha mashindano ya michezo shuleni (darasa kwa darasa, wanafunzi kwa watumishi) na mchezo ya shule za nje.

## UZALISHAJI MALI:

- Shule inayo bustani ambayo inazalisha mboga kwa ajili ya matumizi ya shule.
- Shule ina mashine ya kusaga na kukoboa kwa ajili ya matumizi ya shule.

- Lori la shule linasafirisha mizigo na kuingiza kipato kwa shule.
- Shule ina mradi wa duka ambalo linaiigizia shule kipato.
- Tumefanikiwa kuwafanya wanafunzi kushiriki katika kazi za mikono na shughuli za uzalishaji mali kama vile kumwagilia bustani, kupanda miti hasa ya matunda.
- Shule ina mradi wa shamba unaoingizia shule kipato (chakula).
- Shule ina mradi wa saluni unaoingizia shule kipato.
- Shule imefanikiwa kuanzisha mradi wa nyuki katika msitu wa shule. Mpaka sasa shule imeshavuna asali awamu moja.



## HUDUMA YA MALEZI NA NIDHAMU:

Kwa ujumla tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kutoa malezi bora kwa wanafunzi wetu na kutoa huduma bora zaidi za unasihi ambazo zinawawezesha wanafunzi kukua vema kimwili, kiakili, kiroho na kijamii. Tabia na mienendo yao imekuwa ikirekebishwa kwa upendo na nidhamu yao imeimarika sana.

Kutokana na juhudi hizo ripoti ya 25/10/2020 ya ukaguzi wa serikali (Wathibiti Ubora wa Shule Kanda ya Magharibi) ulofanyika 20 hadi 21 Oktoba 2020 imeiweka shule katika ubora wa hali ya juu wa nidhamu kwa kutupatia daraja A.

## RASILIMALI WATU:

Shule imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwa wafanyakazi wenye sifa katika vitengo mbalimbali ambapo tumefanikiwa kuajiri wafanyakazi 33 kati yao walimu ni 17 na 16 ni kada zingine.

## AFYA

Tumefanikiwa kutoa huduma ya matibabu katika zahanati ya shule kwa wanafunzi na wafanyakazi wetu na pia jamii inayotuzunguka. Kwa sasa zahanati yetu inatoa tiba kwa watu ambao ni wanachama wa NHIF.

## MAMBO YA KIROHO:

- Tumefanikiwa kuwafanya wanafunzi kuwa na ibada mbalimbali na program zingine zinazofanyika hapa shuleni. Pia tumekuwa na mafundisho mbali mbali ya kiroho na majuma ya maombi ya shule na yale yatokayo ngazi za juu za kanisa letu.
- Tumefanikiwa kuwa na mikutano ya makambi yanayofanyika mara moja kila mwaka.

**Waliobatizwa Kuanzia Mwaka 2017 Hadi 2022**

| Mwaka | Idadi ya wanafunzi | Jumla ya waliobatizwa |
|---|---|---|
| 2017 | 387 | 100 |
| 2018 | 360 | 129 |
| 2019 | 312 | 84 |
| 2020 | 242 | 100 |
| 2021 | 228 | 140 |
| 2022 | 235 | 49 |

## CHANGAMOTO:

- Upungufu wa rasilimali fedha.
- Baadhi ya wazazi kutolipa ada kwa wakati.
- Kupanda kwa gharama za uendeshaji wa shule hasa mahitaji ya kila siku.
- Hali ya hewa kutokuwa rafiki kwa wazazi/walezi kwani idadi kubwa ya wazazi na walezi wanategemea kilimo (hasa pamba).

## MIPANGO ILIYOKO KWENYE UTEKELEZAJI:

- Kuendelea kutoa taaluma inayotukuka kwa kufuta daraja la tatu na nne kwa kidato cha pili, nne na sita kwa kuhakikisha kuwa wanafunzi wanafaulu kwa kupata gredi A na B kwa kidato cha pili na nne na gredi A,B na C kwa kidato cha sita.
- Kupaka rangi mabati ya shule katika madarasa kwa maana yamechakaa na kuendelea kukarabati nyumba za watumishi hasa zile za muda mrefu.
- Kuboresha ukumbi wa mikutano (auditorium) kwa kuweka feni.
- Kuzidi kuimarisha nidhamu ya wanafunzi.
- Kuongeza upandaji wa miti mbali mbali hasa ya matunda.

- Kuendelea kusimamia vyema ukusanyaji wa karo na fedha zingine kutoka miradi mbali mbali ya shule.
- Kuendelea kuwa na rasilimali watu ya kutosha wakati wote.
- Kuimarisha vyama vya vijana kama vile Wavumbuzi, Watafuta njia Mabalozi na vingine.
- Kuboresha na kusimamia ufundishaji wa somo la TEHAMA (Kompyuta) shuleni.
- Kuitangaza shule kwa njia mbalimbali mfano redioni, TVs makanisani, mikutanoni, vipeperushi, kuwatembelea wazazi wa wanafunzi na nyinginezo.

## MIPANGO YA MAENDELEO YA MIAKA MITANO IJAYO 2023 HADI 2027.

- Kuendeleza ujenzi wa ukumbi wa mikutano.
- Kujenga ofisi, choo na kibweta cha makambi eneo la ukumbi wa mikutano.
- Kujenga nyumba 03 za makazi kwa ajili ya wafanyakazi wa shule.
- Ujenzi wa maktaba ya kisasa.
- Ujenzi wa jengo la kisasa la utawala.
- Kuendeleza mradi wa ufugaji wa nyuki.
- Kuwa na kilimo cha umwagiliaji maji.
- Kuendelea kuboresha mazingira kwa kupanda miti.
- Kupaka rangi paa za majengo.

## MWISHO:

Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wenu katika kuendeleza utume wa kanisa kwa njia ya elimu (shule).

Mungu awabariki sana.

Ni mimi,
SOSTHENES MALEGESI MGUNDA
MKUU WA SHULE

## UTANGULIZI.

Tunamshukuru Baba yetu wa mbinguni kwa ulinzi wake na mibaraka ambayo ametupatia tangu tuanze mwaka 2016 hadi mwaka huu wa 2022.

Uongozi wa shule unashukuru pia ushirikiano ambao unapata toka kwa viongozi wetu wa kanisa pamoja na washiriki katika kuhakikisha kituo hiki kinasonga mbele. Jina la BWANA lihimidiwe.

## USAJILI WA WANAFUNZI 2011 – 2015.

| MWAKA | WAVULANA | WASICHANA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 2016 | 295 | 242 | 537 |
| 2017 | 313 | 295 | 608 |
| 2018 | 258 | 254 | 512 |
| 2019 | 286 | 252 | 538 |
| 2020 | 267 | 293 | 560 |
| 2021 | 525 | 244 | 496 |
| 2022 | 261 | 224 | 485 |

## WALIMU.

| MWAKA | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 2016 | 18 | 9 | 27 |
| 2017 | 17 | 9 | 26 |
| 2018 | 18 | 9 | 27 |
| 2019 | 18 | 9 | 27 |
| 2020 | 17 | 9 | 26 |
| 2021 | 17 | 9 | 26 |
| 2022 | 17 | 9 | 26 |

## WAFANYAKAZI WASIO WALIMU.

| MWAKA | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 2016 | 12 | 8 | 20 |
| 2017 | 12 | 8 | 22 |
| 2018 | 11 | 10 | 21 |
| 2019 | 11 | 10 | 21 |
| 2020 | 7 | 12 | 19 |
| 2021 | 7 | 12 | 19 |
| 2022 | 8 | 13 | 21 |

## TAALUMA.

Matokeo ya mitihani kidato cha pili na kidato cha nne.

| MWAKA | WANAFUNZI WALIOFANYA MTIHANI | AINA YA MTIHANI (KIDATO) | WALIO FAULU | WALIO SHINDWA | WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO |
|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 134 | II | 134 | - | - |
| | 85 | IV | | - | 70 |
| 2017 | 200 | II | 200 | - | - |
| | 95 | IV | | - | 85 |
| 2018 | 136 | II | 136 | - | - |
| | 66 | IV | | - | 66 |
| 2019 | 107 | II | 107 | - | - |
| | 137 | IV | | - | 131 |
| 2020 | 132 | II | 132 | - | - |
| | 129 | IV | | - | 124 |
| 2021 | 146 | II | 146 | - | - |
| | 97 | IV | | - | |

NB: Shule imefanikiwa kuanzisha masomo ya kidato cha tano na sita Julai, 2022.




*Picha 1: Wanafunzi wa Nyanza wakitoa huduma katika kanisa la Kirumba.*

## MAJENGO.

Tulianza na eneo la acre 15½.

- Vyumba vya madarasa viko 12.
- Mabweni ya wasichana 03 na wavulana 02.
- Jengo la utawala lipo.
- Maabara vyumba 3.
- Jengo la Ibada halijakamilika.

NB: Ujenzi wa uzio (fence) wa shule unaendelea ambapo imefikia 50%.

## MIRADI.

- Duka.
- Ufyatuaji matofali.
- Canteen.
